# Al-Kashif-Juzuu Ya Kumi Na Saba

# Al-Kashif-Juzuu Ya Kumi Na Saba



Muhammad Jawad Mughniyya

Kimetafsiriwa na
Hassan Ali Mwalupa

Al-Islam.org

**Author(s):**

Muhammad Jawad Mughniyya [1]

**Publisher(s):**

Al-Itrah Foundation [2]

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhudi ya miaka mingi sana ya watu waliojitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Get PDF [3] Get EPUB [4] Get MOBI [5]

**Translator(s):**

Hassan Ali Mwalupa [6]

# Utangulizi Wa Mchapishaji

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhudi ya miaka mingi sana ya watu waliojitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Kama lilivyo jina la Tafsiri ndivyo ilivyo Tafsiri yenyewe ambayo mwanachuoni huyu mahiri kabisa aliyeifafanua ni mtu aliyebobea katika fani zote ambazo mfasiri (Mfafanuzi) anatakiwa awe nazo.

Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya ameonesha cheche zake katika vitabu vingi alivyoviandika katika maudhui mbalimbali na hivyo kujipatia wasomaji wengi sana.

Msomi huyu, mwenye fikra huru na anayetetea kile anachokiamini, ni mtu mwenye mawazo mapana na kuyaangalia mambo kwa undani sana, kipaumbele chake ni katika maslahi ya umma huu na amejaribu sana kwenda na wakati.

Sifa kubwa pekee ya mwanachuoni huyu ni kuwa yeye hakujihusisha sana na kung'ang'ania madhehebu fulani tu, labda hii yatokana na wadhifa wake wa ukadhi aliokuwa nao katika nchi ya Lebanon ambayo ina madhehebu mengi, ambapo sula la madhehebu ni nyeti nchini humo, hata hivyo yeye aliweza kuamua matatizo ya watu kwenye ofisi yake kulingana na madhehebu yao pale walipomwendea.

Hiyo ilimsaidia sana hata kuweza kutoa kitabu kitwacho *Al-Fiqh a'laa madhaahabil-khamsah* (Fikhi ya madhehebu matano) yaani ya Hanafi, Maaliki, Shafi, Hambali na Shia (ambacho twataraji kitatoka kwa lugha ya kiswahili hivi karibuni Inshaallah).

Jambo lililotupa msukumo wa kukifasiri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ni zile faida nyingi atakazozipata msomaji na kujua mambo mengi na ya ajabu yaliyo mapya kwake ambayo si rahisi kuyapata kwa wafasiri wengine.

Msomaji atapata faida katika fani za Sayansi, Siasa, Historia, Mashairi, visa vizuri, na Saikolojia miongoni mwa mengine; ndiyo maana msomaji atashangaa kidogo anapoisoma Tafsiri hii atakapoona mwandishi amewataja na kuwanukuu watu kama kina Mfalme Edward, wanasayansi kama kina Enstein, wasanii kama Charlie Champlin (Mchekeshaji maarufu), na wengineo, hali inayoifanya tafsiri hii kuwa ni ya kipekee kabisa.

Mtindo alioutumia mwandishi ni sahali uliokusudiwa watu wa tabaka mbalimbali, wanavyuoni na watu wa kawaida.
Nia yetu ni kukigawanya kitabu hiki bure lakini tumelazimika kukiuza kwa bei nafuu ili kurudisha gharama za uchapishaji.

Mwisho: Shukrani kubwa iwaendee bila ya kuwataja watu waliojitolea usiku na mchana, jopo la wafasiri, wahariri, wachapaji, waliotupa moyo na kutoa maoni yao na walioisimamia ili kuhakikisha kwamba kitabu kimemfikia msomaji.

## Makosa Ya Chapa

Sikumbuki kama nimewahi kusoma kitabu kilichotoka kupigwa chapa, cha zamani au cha sasa, bila ya kukuta makosa ya chapa. Nafikiri sitasoma kitabu kisichokuwa hivyo. Nimejaribu sana kuliepuka hilo katika tungo zangu, lakini sikufanikiwa.

Nilikuwa sifikirii kama ninaweza kuona makosa haya katika maandishi ya msahafu mtukufu, kama yale yaliyo katika baadhi ya chapa; kwa mfano neno *yabswutu* kwa *swad*, badala ya *yabsutu* kwa sin, na katika chapa ya Tafsir Arrazi ya Misr ya mwaka 1935, Sura ya (2:146). Imeandikwa *La Ya'alamuun,* (hawajui) badala ya *Ya'alamuun* (wanajua). Mfano wa makosa haya hausameheki.

Katika Tafsir *Al-Manar,* chapa ya Pili, sura (5:212), imeandikwa *Fawqahum ila yawmil qiyama* badala ya *Fawqahum yawamal qiyama*. Hatuwezi kusema kosa hili ni kubwa zaidi kuliko lile.

Lakini mkosaji atatuletea udhuru kwa msemo mashuhuri huko kwetu Jabal amil 'Makosa ya chapa.'

Katika Tafsiri Majmau chapa ya Urfan, Sura (46:15), imeandikwa: *Hatta idha balagha arbai' na sanah* badala ya: Hattaidha balagha ashuddahu arbai ' na sanah"

Kusema hivi sio kama ninajitetea kutokana na makosa ya chapa atakayoyakuta msomaji katika kitabu hiki, ijapokuwa naomba msamaha kama litatokea hili, lakini makusudio yangu hasa ni kumwambia yule atakayefungua macho yake kwenye makosa ya matamko na kuufungia macho uzuri wa maana. Vilevile ninamwambia yule ambaye siku moja aliniambia: "Vitabu vyako vimejaa makosa ya chapa." Kama

kwamba hakuna kitu chochote katika vitabu hivyo isipokuwa makosa ya chapa tu. Wote hao ninawaambia: Mungu awasamehe na aniongoze mimi na nyinyi.

Vyovyote iwavyo, mimi ninaomba msamaha kutokana na makosa ya kifikra na ya chapa. Anasema Amirul Muminiin (a.s): "Watu wote ni wapungufu wenye kuchanganyikiwa, isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu." Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye mwenye jukumu la kunikubalia yale niliyoyapatia na kunisamehe niliyakosea, kwa jaha ya Mtume na kizazi chake, ziwashukie rehema na amani (Amin).

**MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYAH**

# Sura Ya Ishirini na Mmoja : Al - Anbiya

Imeshuka Makka Ina Aya 112

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu***

{اقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُعْرِضُونَ {1

***Imewakurubia watu hisabu yao nao wamo katika mughafala wanapuuza.***

{مَا يَأْتِيهِمْ مِنْ ذِكْرٍ مِنْ رَبِّهِمْ مُحْدَثٍ إِلَّا اسْتَمَعُوهُ وَهُمْ يَلْعَبُونَ {2

***Hawafikii dhikr mpya kutoka kwa Mola wao ila huisikiliza na huku wanaifanyia mchezo.***

{لَاهِيَةً قُلُوبُهُمْ ۗ وَأَسَرُّوا النَّجْوَى الَّذِينَ ظَلَمُوا هَلْ هَٰذَا إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ ۖ أَفَتَأْتُونَ السِّحْرَ وَأَنْتُمْ تُبْصِرُونَ {3

***Zimeghafilika nyoyo zao Na wale waliodhulumu hunog'ona kwa siri: Ni nani huyu isipokuwa ni mtu tu kama nyinyi. Mnauendea uchawi hali nanyi mnaona?***

{قَالَ رَبِّي يَعْلَمُ الْقَوْلَ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ {4

***Alisema: Mola wangu anajua yasemwayo mbinguni na ardhini na Yeye ni mwenye kusikia, mwenye kujua.***

{بَلْ قَالُوا أَضْغَاثُ أَحْلَامٍ بَلِ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ شَاعِرٌ فَلْيَأْتِنَا بِآيَةٍ كَمَا أُرْسِلَ الْأَوَّلُونَ {5

***Lakina walisema: Hizo ni ndoto za ovyo ovyo, bali amezizua, bali huyo ni mshairi. Basi atuletee ishara kama walivyotumwa wale wa mwanzo.***

{مَا آمَنَتْ قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا ۖ أَفَهُمْ يُؤْمِنُونَ {6

***Hawakuamini kabla yao watu wa mji tuliouangamiza. Je, wataamini hao.***

# Aya 1 – 6: Imewakurubia Watu Hisabu Yao

## Maana

**Imewakurubia watu hisabu yao nao wamo katika mughafala wanapu- uza.**

Makusudio ya hisabu hapa ni siku ya Kiyama, nayo iko karibu na kila mtu, kwa sababu itakuja tu, hata kama muda utakuwa mrefu. Maana yake yanafupishwa na kauli ya Imam Ali: "Usijisahau kwani wewe hujasahauliwa." Na akasema tena: "Usighafilke kwani wewe hujasahauliwa." Akasema tena: "Hatua fupi ilioje ya mtu aliye na siku moja tu ambayo hawezi kuizidisha, na mauti yaliyo na haraka yanamuandama mpaka aitoke"

**Hawafikii dhikr mpya kutoka kwa Mola wao ila huisikiliza na huku wanaifanyia mchezo.**

Wanaikabili haki kwa kuikadhibisha, nasaha za kejeli na hadhari za dharau. **Zimeghafilika nyoyo zao** na haki, hawajali kitu wala hawahisi majukumu ya kuulizwa hisabu na malipo; sawa na wanyama na wadudu.

**Na wale waliodhulumu hunog'ona kwa siri: Ni nani huyu isipokuwa ni mtu tu kama nyinyi.**

Washirikina walinong'onezana kuhusu aliyesilimu na kuongoka, kuwa huyo Muhammad, ni nani hata tumtii na kumfuata? Yeye si mtu tu kama watu wengine, anakula chakula na anatembea sokoni? Ama elimu na fadhila basi ni maneno bila maana na miujiza ni uchawi na kuvunga.

**Mnauendea uchawi hali nanyi mnaona?**

Mnauendea hapa, ina maana ya kukubali, na mnaona ni kwa maana ya mnajua. Si ajabu wao kuzikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu na dalili zake ambazo amekuja nazo Mtume mtukufu (s.a.w.). Kila mwenye kiburi hutafuta visingizio vya aina hii ikiwa hana hoja.

**Alisema: Mola wangu anajua yasemwayo mbinguni na ardhini na Yeye ni mwenye kusikia, mwenye kujua.**

Walimwambia Mtume (s.a.w.) kuwa yeye ni mchawi akawajibu kuwa Mwenyezi Mungu anajua ukweli wake na anajua kauli yao hii, kwa sababu hakifichiki kwake kitu chochote katika ardhi na katika mbingu. Atawahisabu na atawalipa vile mnavyostahiki.
Hakuna jawabu kwa anayeipinga haki isipokuwa kupelekwa kwenye mahakama ya uadilifu.

**Lakina walisema: Hizo ni ndoto za ovyo ovyo, bali amezizua, bali huyo ni mshairi.**

Waliikataa wanamangamanga haki wakatafuta visingizio vya kutumia, wakabaki tu. Mwenye *Majmaul-bayan* anasema: "Hivi ndivyo anavyokuwa yule Mwenye kuhemewa. Anasema ni mchawi, mara ni mshairi, mara anaota. Hana moja analolishikilia. Huku ndio kujipinga kwa dhahiri."

**Basi atuletee ishara kama walivyotumwa wale wa mwanzo.**

Washirkina walimwambia Muhammad (s.a.w.): Ukiwa wewe ni Mtume basi tuletee muujiza, kama vile ngamia wa Swaleh, fimbo ya Musa na miujiza mingineyo ya mitume waliopita. Ndio Mwenyezi Mungu akawajibu kwa kusema:

**Hawakuamini kabla yao watu wa mji tuliouangamiza.**

Maana ya jawabu hili ni kuwa, ni kweli kwamba mitume waliotangulia walikuja na miujiza, kama vile ngamia na fimbo, lakini watu wao hawakuwaamini, bali walikataa na wakamakadhibisha, ingawaje wao wenyewe ndio walioitaka. Kwa ajili hiyo tukawaangamiza.

Kwa hiyo inatakiwa enyi washirikina muangalie natija inayofungamana na miujiza sio muujiza wenyewe. Kwa sababu itawatokea hivyo hivyo, ikiwa Mwenyezi Mungu atawakubalia mapendekezo yenu.

**Je, wataamini hao.**

Yaani wale waliokuwa kabla yao hawakuamini miujiza waliyoipendekeza, vile vile hawa hawataamini miujiza wanayoipendekeza. Natija itakuwa ni kuangamizwa, kama walivyoangamizwa wa kwanza; ambapo hekima yake Mwenyezi Mungu ilipitisha kuwa waangamizwe kwa miujiza waliyoitaka.

{وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ إِلَّا رِجَالًا نُوحِي إِلَيْهِمْ ۖ فَاسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ {7

***Na hatukuwatuma kabla yako ila wanaume tuliowapa wahyi. Basi waulizeni wenye kumbukumbu,***

***ikiwa nyinyi hamjui.***

8{وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَمَا كَانُوا خَالِدِينَ}

***Na hatukuwafanya miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kuishi milele.***

9{ثُمَّ صَدَقْنَاهُمُ الْوَعْدَ فَأَنْجَيْنَاهُمْ وَمَنْ نَشَاءُ وَأَهْلَكْنَا الْمُسْرِفِينَ}

***Kisha tukawatimizia miadi na tukawaokoa wao na tuliowataka na tukawaangamiza waliopita mipaka.***

10{لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ ۖ أَفَلَا تَعْقِلُونَ}

***Hakika tumewateremshia Kitabu, ndani yake mna ukumbusho wenu. Je, hamtii akili?***

11{وَكَمْ قَصَمْنَا مِنْ قَرْيَةٍ كَانَتْ ظَالِمَةً وَأَنْشَأْنَا بَعْدَهَا قَوْمًا آخَرِينَ}

***Na miji mingapi iliyokuwa ikidhulumu tumeiteketeza na tukawaumba baada yao watu wengine.***

12{فَلَمَّا أَحَسُّوا بَأْسَنَا إِذَا هُمْ مِنْهَا يَرْكُضُونَ}

***Basi walipohisi adhabu yetu mara wakaanza kukimbia.***

13{لَا تَرْكُضُوا وَارْجِعُوا إِلَىٰ مَا أُتْرِفْتُمْ فِيهِ وَمَسَاكِنِكُمْ لَعَلَّكُمْ تُسْأَلُونَ}

***Msikimbie! Na rejeeni kwenye zile zile starehe zenu na maskani zenu mpate kusailiwa.***

14{قَالُوا يَا وَيْلَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ}

***Wakasema: Ole wetu! Hakika sisi tulikuwa madhalimu.***

15{فَمَا زَالَتْ تِلْكَ دَعْوَاهُمْ حَتَّىٰ جَعَلْنَاهُمْ حَصِيدًا خَامِدِينَ}

***Hakikuacha hicho kuwa kilio chao mpaka tukawafanya wamefyekwa wamezimika.***

# Aya 7 – 15: Waulizeni Wenye Kumbukumbu

## Maana

**Na hatukutuma kabla yako ila wanaume tuliowapa wahyi. Basi waulizeni wenye kumbukumbu, ikiwa nyinyi hamjui.**

Imekwishatangulia kwa herufi zake katika Juz. 14 (16:43).

**Na hatukuwafanya miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kuishi milele.**

wao wenyewe.

Manabii sio roho bila ya miili wala wao hawatakaa maisha hapa duniani. Wao ni kama watu wengine, hawana tofauti isipokuwa kwa kufikisha neno la Mungu na kwamba wao ni wakamilifu. Angalia Juz. 16 (20: 35) kifungu 'Hakika ya Utume'.

**Kisha tukawatimizia miadi na tukawaokoa wao na tuliowataka na tukawaangamiza waliopita mipaka.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anaishiria kwenye kauli yake hii pale aliposema:

{كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۚ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ {21

***"Mwenyezi Mungu amekwishaandika: Hakika nitashinda mimi na Mitume wangu."Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye kushinda."* (*58:21*).**

Na akasema tena:

{إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ {51

***"Hakika bila shaka tutawanusuru mitume wetu na walioamini katika maisha ya duniani na siku watakaposimama mashahidi."* (*40:51*).**

Kwa ufupi ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliwaahidi mitume na wau- mini kuokoka na makafiri kuangamia. Alitekeleza ahadi yake. Ni nani kuliko Mwenyezi Mungu katika utekelezaji ahadi?

## Muhammad Na Waarabu

**Hakika tumewateremshia Kitabu, ndani yake mna ukumbusho wenu. Je, hamtii akili?**

Kabla ya Muhammad (s.a.w.) na Qur'an waarabu hawakuwa ni chochote. Baada ya vitu viwili hivyo wakawa ni watu mashuhuri, ikatajwa historia namaendeleo yao, wakawa ni watu wa hali ya juu. Anasema: W.L. Dewarnet katika *Ensaiklopidia* yake ya Historia ya kisa cha maendeleo katika ulimwengu: "Muhammad ni mkuu miongoni mwa wakuu wa Historia. Aliwainua watu walioishi katika giza la ushenzi, anga ya joto na ukame wa jangwa, kwenye ustawi wa kiroho na kimaadili. Alifaulu kwenye lengo hili kwa namna ambayo hajawahi kuifikia kiongozi yeyote katika historia yote.

Alipoanza mwito wake miji ya waarabu ilikuwa ni jangwa tupu linalokaliwa na makabila ya waabudu mizimu yenye watu wachache wasiokuwa na umoja wowote. Lakini kufikia kufa kwake wakawa ni umma wenye mshikamano, wakiwa wamekiuka ubaguzi na upuuzi.

Wakawa juu ya uyahudi na ukiristo na dini ya nchiyake ikawa wazi na nyepesi. Ikajengeka misingi ya kijasiri, utukufu na uzalendo. Kwenye kizazi kimoja tu ikaweza kushinda vita mia moja na katika karne moja ikaweza kuanzisha dola kuu na kubakia hadi leo kuwa ni nguvu kuu ulimwenguni"

**Na miji mingapi iliyokuwa ikidhulumu tumeiteketeza na tukawaumba baada yao watu wengine.**

Haya ni makemeo na kiaga kwa wale wanaomkadhibisha Muhammad (s.a.w.) kwamba wao yatawapata yaliyowapata waliokuwa kabla yao katika umma zilizowakadhibisha mitume wao. Kisha Mwenyezi Mungu awalete wengine wasiokuwa na uhusiano wowote na walioangamizwa; awarithishe milki zao na majumba yao. Wajenge upya na wastarehe na kheri zake na baraka zake.

**Basi walipohisi adhabu yetu mara wakaanza kukimbia.**

Hii ni taswira ya hali ya washirikina inapowafikia adhabu kutoka mbinguni, wanajaribu kuikimbia, lakini wapi! Inawezekana vipi kuukimbia utawala wa Mwenyezi Mungu na hukumu yake? Kama hapo mwanzo wangelikimbilia kwa Mwenyezi Mungu wangelikuta amani. Ama kumkimbia yeye Mwenyezi Mungu ni sawa na mtu kukimbia kivuli chake.

**Msikimbie! Na rejeeni kwenye zile zile starehe zenu na maskani zenu mpate kusailiwa.**

Kabla ya kuteremshwa adhabu washirikina walikuwa hawajishughulishi na lolote zaidi ya mali na starehe zao, lakini ilipowashukia adhabu, nyoyo na akili zao zilipofuka na wakatupilia mbali kila kitu. Ndio Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akawaambia kwa kuwatahayariza: Mnaenda wapi? Rudini kwenye mali zenu na watoto wenu.

Leo mnaziacha na jana mlikuwa mkiziabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Haya ndio malipo ya anayeacha uongofu na asiongoke kwenye uongofu.

**Wakasema: Ole wetu! Hakika sisi tulikuwa madhalimu.**

Walitulia na starehe zao, wakaitikia matamanio yao na wakamtuhumu anayewapa nasaha, lakini walipoiona adhabu walijuta na wakaita ole wetu, lakini majuto ni mjuukuu hayarudishi yaliyopita.

**Hakikuacha hicho kuwa kilio chao mpaka tukawafanya wamefyekwa wamezimika.**

Wanalia ole wetu na adhabu iko kichwani mwao ikiendelea. Haikufaa mali wala jaha. Huo ndio mwisho wa wakosefu.

{وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لَاعِبِينَ {16

***Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yao kwa mchezo.***

{لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ لَهْوًا لَاتَّخَذْنَاهُ مِنْ لَدُنَّا إِنْ كُنَّا فَاعِلِينَ {17

***Kama tungelitaka kufanya mchezo tungelijifanyia sisi wenyewe, kama tungekuwa ni wafanyao mchezo.***

{بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ ۚ وَلَكُمُ الْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُونَ {18

***Bali tunaitupa haki juu ya batili ikaivunja na mara ikatoweka. Na ole wenu kwa mnayoyasifia .***

{وَلَهُ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَمَنْ عِنْدَهُ لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ وَلَا يَسْتَحْسِرُونَ {19

***Ni vyake vilivyoko mbinguni na ardhini na walioko mbele yake hawafanyi kiburi wakaacha kumwabudu wala hawachoki.***

{يُسَبِّحُونَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لَا يَفْتُرُونَ {20

***Wanamsabihi usiku na mchana wala hawanyog'onyei.***

{أَمِ اتَّخَذُوا آلِهَةً مِنَ الْأَرْضِ هُمْ يُنْشِرُونَ {21

***Au wamepata miungu katika ardhi inayofufua.***

{لَوْ كَانَ فِيهِمَا آلِهَةٌ إِلَّا اللَّهُ لَفَسَدَتَا ۚ فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ {22

***Lau wangelikuwemo humo miungu wengine isipokuwa Mwenyezi Mungu basi zingefisidika. Ametasika Mwenyezi Mungu, Mola wa arshi, na hayo wanayoyasifu.***

{لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ {23

***Yeye haulizwi kwa ayatendayo na wao ndio waulizwao kwa wayatendayo.***

# Aya 16 – 23: Je, Vitendo Vyake Mwenyezi Mungu Mtukufu Vina Malengo?

## Maana

**Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yao kwa mchezo.**

Umetangulia mfano wake katika Juz. 4 (3:191). Huko tumenukuu kauli kuhusiana na kuwa je, vitendo vya Mwenyezi Mungu vinakuwa na sababu ya malengo au kwake Mwenyezi Mungu hakuna ubaya wala hana wajibu wa chochote?

**Kama tungelitaka kufanya mchezo tungelijifanyia sisi wenyewe, kama tungekuwa ni wafanyao mchezo.**

Mchezo na upuuzi ni muhali kwa yule anayekiambia kitu kuwa na kikawa. Ndio maana Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: 'Lau tungelitaka ... kama tungekuwa ni wafanyao mchezo' yaani hatukataka wala hatufanyi. Lau angelitaka kufanya mchezo – kukadiria muhali sio muhali – angelijifanyia kwa namna yoyote inayolingana na cheo chake; sio katika namna ya waja; kama kucheza na wanawake na watoto.

**Bali tunaitupa haki juu ya batili ikaivunja na mara ikatoweka.**

Makusudio ya haki hapa ni ukweli na uhakika kwa mkabala wa mchezo alioukanusha Mwenyezi Mungu Mtukufu na makusudio ya batili hapa ni upuzi na mchezo.

Baada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kusema hatufanyi mchezo sasa anasema kuwa vitendo vyake kwake ni uhakika na ukweli si mchezo na upuzi; bali ukija upuzi na mchezo kutoka popote anauvunjilia mbali. Vipi ataliridhia lile asiloliridhia kwa mwingine?

**Na ole wenu kwa mnayoyasifia nayo Mwenyezi Mungu na kumbandika sifa za kutengeneza.**

**Ni vyake vilivyoko mbinguni na ardhini na walioko mbele yake hawafanyi kiburi wakaacha kumwabudu wala hawachoki.**

Wafasiri wanasema kuwa makusudio ya walioko mbele yake, ni Malaika. Tunavyofahamu sisi ni kuwa makusudio ni kila mwenye cheo na jaha mbele ya Mwenyezi Mungu, awe Malaika au mtu.

**Wanamsabihi usiku na mchana wala hawanyonyog'onyei.**

Yaani hawachoki, bali wanadumu kwenye twaa katika kauli na vitendo wala hawamtuhumu Mwenyezi Mungu kwa kumsawirisha au kumpa sifa za kutengeneza.

**Au wamepata miungu katika ardhi inayofufua.**

Yaani kila anayeabudiwa na washirikina, hawezi kuhui wafu wala hawafufui wafu walio makaburini, bali Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anayehui na kufisha.

**Lau wangelikuwemo humo miungu wengine isipokuwa Mwenyezi Mungu basi zingefisidika. Ametasika Mwenyezi Mungu, Mola wa arshi, na hayo wanayoyazua.**

Tazama tuliyoyaandika kwenye Juz. 5 (4:48) Kifungu 'Dalili ya umoja na utatu.'

**Mwenye kujua ni hoja kwa asiyejua Yeye hahojiwi kwa ayatendayo na wao ndio wanaohojiwa kwa wayatendayo.**

Baadhi wametoa dalili kwa Aya hii kwamba hakuna ubaya kwa Mungu wala hawajibikiwi na jambo lolote. Anaweza kumwadhibu mtiifu na kumlipa thawabu muasi. Lakini hii inapingana na uadilifu wake, hekima na rehema yake.

Usahihi hasa ni kuwa maana ya Aya ni Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kwa kuwa ni mwadilifu kwa dhati yake, haijuzu kwa yeyote kumwingilia kwa kauli yake na vitendo vyake. Kwa sababu haijuzu kuambiwa mwadilifu, kwa nini umefanya uadilifu? Na mkweli, kuambiwa kwa nini umesema kweli? Kama ambavyo haifai kwa asiyejua utabibu kumwambia tabibu hodari, kwa nini unatoa dawa hii?

Mfano wa maswali haya unafaa kwa aliye kifani wake. Ama asiyejua kitu, analotakiwa ni kufanya juhudi ya kumtafuta mjuzi na kuhakikisha ujuzi wake kutokana na dalili na alama. Akishapata uhakika basi inakuwa ni wajibu kwake kumfuata kwa yale aliyo na ujuzi nayo; sawa na mgonjwa anavyomfuata tabibu.

Walikwishasema wahenga: "Ajuaye ni hoja kwa asiyejua." Ikiwa mambo ni hivi kwa kiumbe pamoja na kiumbe mwenzake. Itakuwaje kwa kiumbe pamoja na muumba wa mbingu na ardhi?
Siku moja mwanafunzi alimuuliza mwalimu wake: "Kwa nini tuko na kwa nini tunaishi?"

Mwalimu akamwambia mwanafunzi wake: “Kwa nini ewe mwanangu unajilazimisha na mambo yasiyokuwa na mwanzo wala mwisho? Kwa nini usiamini dini ikastarehe nafsi yako na uawache yale usiyoyaweza, ufuate unayoyaweza? Wewe ni mmoja wa maelfu ya mamilioni ya watu na mji wako uanaoishi ni moja ya maelfu ya miji. Ardhi tunayoishi ni moja ya mamilioni ya sayari na ulimwengu ulio na sayari zote hizo, hatujui kuwa kuna mfano wake unaouzidia. Je, sehemu moja inaweza kudhibiti yote hayo? Je, tone moja linaweza kuihoji bahari?

Mwanangu! Mimi sisemi kuwa usifanye uchunguzi na kupeleleza, kwani kutafuta hakika ni miongoni mwa sababu za kupatikana binadamu, lakini maadamu akili yako ni ndogo kuweza kufahamu hakika hiyo, basi ngoja mpaka uzidi kupata ufahamu na utambuzi. Mwisho ukishindwa, liache jambo kama lilivyo. Kwa sababu udogo wa akili yako kufahamu jambo, haimaanishi kuwa jambo hilo ni mchezo na upuzi; isipokuwa inamaanisha kuwa hujalifahamu; kwa hiyo muachie aliyeumba vyote vilivyoko.”

أَمِ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ آلِهَةً ۖ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ ۖ هَٰذَا ذِكْرُ مَنْ مَعِيَ وَذِكْرُ مَنْ قَبْلِي ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ الْحَقَّ ۖ فَهُمْ مُعْرِضُونَ {24}

***Au wamejifanyia miungu mingine badala yake. Sema, leteni dalili yenu. Hii ni ukumbusho wa walio pamoja nami na ukumbusho wa waliokuwa kabla yangu. Lakini wengi wao hawajui haki kwa hiyo wanapuuza.***

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ {25}

***Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimpa wahyi kwamba hapana Mungu isipokuwa mimi, basi niabuduni mimi tu.***

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَٰنُ وَلَدًا ۗ سُبْحَانَهُ ۚ بَلْ عِبَادٌ مُكْرَمُونَ {26}

***Na wanasema, Mwingi wa rehema ana mwana! Ametakasika na hayo! Bali hao ni waja waliotukuzwa.***

لَا يَسْبِقُونَهُ بِالْقَوْلِ وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ {27}

***Hawamtangulii kwa neno nao wanafanya kwa amri yake.***

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ ارْتَضَىٰ وَهُمْ مِنْ خَشْيَتِهِ مُشْفِقُونَ {28}

***Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala hawamuombei yeyote ila yule anayemridhia. Nao kwa ajili ya kumwogopa wananyenyekea.***

{وَمَنْ يَقُلْ مِنْهُمْ إِنِّي إِلَٰهٌ مِنْ دُونِهِ فَذَٰلِكَ نَجْزِيهِ جَهَنَّمَ ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ {29

***Na yeyote miongoni mwao atakayesema: mimi ni mungu, badala yake, basi tutamlipa Jahannamu. Hivyo ndivyo tunavyowalipa madhalimu.***

# Aya 24 – 29: Leteni Dalili Zenu

## Maana

**Au wamejifanyia miungu mingine badala yake. Sema leteni dalili yenu.**

Kila mtu huwa anasema, mwenye kudai ni lazima alete ushahidi; hata kama yule anayeelekezewa madai ni mtu duni; sikwambii akiwa ni mshirika wa Mwenyezi Mungu katika viumbe vyake. Basi iko wapi dalili?

**Hii Qur'an ni ukumbusho wa walio pamoja nami** na **ukumbusho wa waliokuwa kabla yangu.**

Vitabu vyote vya mbinguni vinaamrisha Tawhid na kukataza shirki. Ikiwa shirki haina dalili ya kiakili wala ya kinakili, basi chimbuko lake ni ujinga na upofu.

**Lakini wengi wao hawajui haki kwa hiyo wanapuuza.** Hii ni kukemea ujinga wao na upotevu wao.

**Na hatukumtuma kabla yako Mtume yoyote ila tulimpa wahyi kwam- ba hapana Mungu isipokuwa mimi, basi niabuduni mimi tu.**

Aya hii ni ubainifu na tafsiri ya Aya iliyo kabla yake. Ya kwanza inasema kuwa hakuna athari yoyote ya shirki katika vitabu vya Mwenyezi Mungu na hii inasema kuwa hakutumwa mtume yeyote isipokuwa kwa ajili ya tawhidi na kumfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu katika ibada.

**Na wanasema, Mwingi wa rehema ana mwana. Ametakasika na hayo! Bali hao ni waja wa waliotukuzwa.**

Mayahudi au kikundi katika wao walisema kuwa Uzayr ni mwana wa Mungu, Wanaswara (wakiristo) wakasema Masih ni mwana wa Mungu; na baadhi ya makabila ya kiarabu yakasema kuwa Malaika ni mabinti wa Mungu.

Ndio Mwenyezi Mungu akawarudi wote hao, kwamba mliowataja ni waja sio watoto, tena wao wana daraja na cheo mbele ya Mola wao.

Ajabu ni yale yaliyoelezwa katika *Tafsiri At-Tabari*, akiwanukuu waliosema kuwa Malaika ni mabinti wa Mwenyezi Mungu: "Mwenyezi Mungu alimuoa jini akamzalia Malaika." Hili ameliashiria Mwenyezi Mungu katika kauli yake:

{وَجَعَلُوا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجِنَّةِ نَسَبًا ۚ {158

***"Na wameweka mahusiano ya nasaba baina Yake na majini" (37:158).***

Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akabainisha sababu ya daraja ya Uzayr, Masih na Malaika mbele yake, kwa kusema:

**Hawamtangulii kwa neno nao wanafanya kwa amri yake.**

Yaani wao hawatumii rai wala kiasi.

**Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao.**

Yaliyo mbele yao ni fumbo la vitendo vyao vya sasa na yaliyo nyuma yao ni vitendo vyao vilivyopita. Maana ni kuwa Yeye Mwenyezi Mungu anayajua vizuri matendo yao ya kheri na makusudio yao mazuri; naye atawalipa ujira wao kwa yale mazuri waliyoyafanya.

**Wala hawamuombei yeyote ila yule anayemridhia Yeye.**

Hii ni kumrudi yule anayemwabudu Mtume, walii au Malaika kwa tamaa ya kuombewa kwa Mungu. Kwa maana kwamba waja waliotukuzwa watawaombea wale wenye kuridhiwa na Mwenyezi Mungu sio washirikina walioghadhibikiwa.

**Nao kwa ajili ya kumwogopa wananyenyekea** pamoja na kuwa wana ikhlasi na vyeo mbele ya Mwenyezi Mungu.

**Na yeyote miongoni mwao atakayesema: mimi ni mungu, badala yake, basi tutamlipa Jahannamu. Hivyo ndivyo tunavyowalipa madhalimu.**

Hao waja wema waliotukuzwa, lau mmoja atadai kuwa yeye ni mungu badala ya Mwenyezi Mungu au ni mshirika wake, basi malipo yake yatakuwa ni Jahannamu, kama washirikina wengine, bila ya kuwa na tofauti yoyote.

أَوَلَمْ يَرَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ كَانَتَا رَتْقًا فَفَتَقْنَاهُمَا ۖ وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَاءِ كُلَّ شَيْءٍ حَيٍّ ۖ أَفَلَا يُؤْمِنُونَ
30}}

***Je, hao waliokufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha tukaziambua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai. Je, hawaamini?***

{وَجَعَلْنَا فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَنْ تَمِيدَ بِهِمْ وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجًا سُبُلًا لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ }31

***Na tukaweka katika ardhi milima ili isiwayumbishe. Na tukaweka humo upana wa njia ili wapate kuongoka.***

{وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ سَقْفًا مَحْفُوظًا ۖ وَهُمْ عَنْ آيَاتِهَا مُعْرِضُونَ }32

***Na tukaifanya mbingu kuwa sakafu iliyohifadhiwa, lakini wanazipuuza ishara.***

{وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۖ كُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ }33

***Na Yeye ndiye aliyeumba usiku na mchana na jua na mwezi. Kila kimoja katika anga vinaogoelea.***

{وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِنْ قَبْلِكَ الْخُلْدَ ۖ أَفَإِنْ مِتَّ فَهُمُ الْخَالِدُونَ }34

***Na hatukumjaalia mtu yeyote wa kabla yako kuishi milele. Je, ukifa wewe wao wataishi milelele?***

{كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ ۗ وَنَبْلُوكُمْ بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً ۖ وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ }35

***Kila nafsi itaonja mauti. Na tutawajaribu kwa mtihani wa shari na kheri na kwetu mtarejeshwa.***

{وَإِذَا رَآكَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوًا أَهَٰذَا الَّذِي يَذْكُرُ آلِهَتَكُمْ وَهُمْ بِذِكْرِ الرَّحْمَٰنِ هُمْ كَافِرُونَ }36

***Na wanapokuona wale ambao wamekufuru hawakufanyii ila mzaha: Je, huyu ndiye anayewataja miungu wenu? Na hao ndio wanaokataa dhikri ya Mwingi wa rehema.***

# Aya 30 – 36: Maji Ni Uhai

## Maana

**Je, hao waliokufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha tukazibandua?**

Mwanzoni mwa Juzuu ya kwanza tumefafanua maelezo yenye kichwa cha maneno 'Qur'an na sayansi,' tukasema kuwa Qur'an ni kitabu cha dini kinachomwongoza mtu kwenye ufanisi wake wa kidunia na akhera; na wala sio kitabu cha nadharia za falsafa, sayansi au falaki n.k.

Na kwamba kila Aya miongoni mwa aya za Qur'an za kilimwengu au za kihistoria, kama vile visa vya mitume, lengo lake ni kutupa mawaidha na mafunzo au kutuongoza kujua kuweko Mwenyezi Mungu, tuweze kumwamini.

Miongoni mwa Aya za kilimwengu ni hii tuliyo nayo. Humo Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ametaja mambo mawili: Kwanza, kwamba sayari za Jua, ikiwemo Jua, Ardhi, Mars, Jupita, Zohali, Zebaki n.k. Zote zilikuwa zimeshikana kama kitu kimoja, kisha Mwenyezi Mungu akazipambanua na kila moja akaifanya ni sayari peke yake.

Wataalamu wameikubali nadharia ya kubanduka Jua na Ardhi, lakini wakatofautiana katika namna ya kubanduka kwake. Qur'an nayo haikufafanua kuhusu aina ya kubanduka kwake. Nasi tunayanyamazia yale aliyoyanyamazia Mungu.

**Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai**.

Hili ni jambo la pili lilotajwa na Aya. Kwamba maji ndio chimbuko la kila kitu kinachokua; awe ni mtu, mnyama au mmea.

Katika Juz. 12 (11:7) Mwenyezi Mungu anasema: "Naye ndiye aliyeumba mbingu na ardhi katika siku sita na arshi yake ilikuwa juu ya maji." Huko tumezungumzia kuwa makusudio ya Arshi ni miliki yake na utawala wake na kwamba maji yalikuwako kabla ya kuumbwa mbingu na ardhi.

Miongoni mwa kauli za Ahlu bayt (a.s.) ni kuwa maji ndio ya kwanza kuumbwa na Mwenyezi Mungu. Ikiwa elimu hivi leo haijaugundua uhakika huu, lakini inawezekana ikaugundua kesho ya karibu au ya mbali.

Amenukuu Abul-hayan Al-andalusi katika *Bahrul-muhit*, kwamba Hamid amesoma: 'Tumejalia maji kuwa ni uhai wa kila kitu.' Kisomo hiki kinatilia nguvu kuwa maji ndiyo yaliyoumbwa mwanzo na ndio chimbuko la kwanza la kila kitu, na kwamba kila kitu kina uhai, kiwe kinakua au hakikui hata kama kwa dhahiri kinaonekana kimeganda.

**Je, hawaamini** baada ya dalili zote hizi na ubainifu?

**Na tukaweka katika ardhi milima ili isiwayumbishe. Na tukaweka humo upana wa njia ili wapate**

**kuongoka**.

Mahali pengine imesemwa:

{لِتَسْلُكُوا مِنْهَا سُبُلًا فِجَاجًا } 20

***"Ili mtembee humo katika njia pana"* (*71:20*)**

Imetangulizwa njia ndio ukaja upana. Maana yote nisawa.

Yaani Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ameweka njia pana ardhini ili watu wazitumie kwenye makusudio yao. Umetangulia mfano wake katika Juz. 14: (16:15).

**Na tukaifanya mbingu kuwa sakafu iliyohifadhiwa, lakini wanazipuuza ishara.**

Kuwa sakafu maana yake ni kama sakafu. Makusudio ya iliyohifadhiwa hapa ni kubakia sayari sehemu yake kwa nguvu ya mvutano. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anasema:

{وَيُمْسِكُ السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ}65

***"Na anazizuia mbingu zisianguke juu ardhi."* (*22:65*).**

Kuzuia kumetegemezwa kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu yeye ndio sababu ya sababu zote. Maana ni kuwa nidhamu hii ya undani katika kuumba mbingu ni dalili mkataa, kwa wenye akili, ya kuweko muumbji, umoja wake, uweza wake, ujuzi na hekima yake. Lakini watu wengi wanazipinga ishara za Mwenyezi Mungu na dalili zake wakipondokea kwenye hawa zao na ladha zao.

**Na Yeye ndiye aliyeumba usiku na mchana na jua na mwezi.**

Kila kimoja kati ya usiku, mchana, jua na mwezi kina uhusiano mkubwa na binadamu. Mchana ni wa kujishughulisha, usiku ni wa kupumzika na kutulia, jua na mwezi ni kwa ajili ya mwanga, hisabu na faida nyinginezo. Hayo yote ni neema kubwa kwa waja Wake na nguvu ya hoja ya ukuu wa usultani Wake.

**Kila kimoja katika anga vinaogoelea.**

Kila sayari inazunguka kwa vipimo na harakati zinazooana nayo.

Unaweza kuuliza: Ikiwa tutakadiria kusema kila kimoja basi tungesema 'kinaogelea,' sasa kuna wajihi gani wa kusema vinaogelea?

Wafasiri wameleta majibu mengi, lenye nguvu zaidi ni lile linalosema: Kila moja kati ya mwezi na jua kina matilai yake na mashukio yake. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu akarudisha dhamiri ya wingi kwa

kuzingatia hayo.

**Na hatukumjaalia mtu yeyote wa kabla yako kuishi milele. Je, ukifa wewe wao wataishi milelele?**

Tabrasi amesema: “Washirikina wa kikuraishi waliposhindwa na Muhammad (s.a.w.) walisema tumngoje afe, ndipo ikashuka Aya hii kuwajibu kuwa hakuna yeyote atakayeokoka na mauti. Je, mtume akifa nyinyi washirikina hamtakufa? Mfumo wa Aya haukatai aliyoyasema Tabrasi.

**Kila nafsi itaonja mauti**.

Hakuna wa kuyakimbia mauti. Mauti mazuri ni yale ya kufa shahidi kwa ajili ya kuitafuta haki na kuibatilisha batili.

**Na tutawajaribu kwa mtihani wa shari na kheri na kwetu mtarejeshwa**.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) huwapa mtihani waja wake kwa wanayoyapenda na wanayoyachukia, ili idhihiri hakika ya kila mtu. Yule atakayeshukuru wakati wa raha, akavumilia wakati wa shida, basi huyo ni katika waumini wenye ikhlasi na atakuwa na malipo ya thawabu. Na yule mwenye kukufuru na akajivuna, basi huyo ni katika wale waliothibitikiwa na adhabu.

Inasemekana kuwa Amirul-mu’minin, Ali, aliugua. Wenzake wakaja kumtazama na wakamuuliza: “Vipi hali yako ewe Amirul-muminin?” Akasema: “Ni shari tu.” Wakasema: “Maneno haya hayasemwi na mtu mfano wako!”

Akasema: “Mwenyezi Mungu anasema: Na tutawajaribu kwa mtihani wa shari na kheri. Kwa hiyo kheri ni afya na kujitosheleza na shari ni ufukara na ugonjwa.”

Pia Amirul-muminin amesema: “Ambaye dunia yake itamnyookea na asijue kuwa anafanyiwa vitimbi, basi imedanganyika akili yake.” Neno mtihani katika Aya ni kutilia mkazo neno tutawajaribu.

**Na wanapokuona wale ambao wamekufuru hawakufanyii ila mzaha: “Je, huyu ndiye anayewataja miungu wenu?.” Na hao ndio wanaokataa dhikri ya Mwingi wa rehema**.

Wamemkataa Mwenyezi Mungu wakaamini mawe. Mtume akawaita kwenye imani ya Mwenyezi Mungu mmoja aliye peke yake na waachane na mawe.

Lakini wakamfanyia masikhara yeye na mwito wake wa haki iliyo wazi, kwamba masanamu yao na mawe yao hayadhuru wala hayanufaishi.

Baadhi yao wamesema: “Hili ni jambo la ajabu kabisa.” Lakini hakuna ajabu, hii ni kawaida ya kila ambaye amechotwa na manufaa na masilahi ya kibinafsi na akakua katika malezi ya kuiga mazingira, mababa na mababu; ni sawa uigizaji huo uwe ni wa kuabudu mawe au kung’ang’ania rai bila ya elimu wala muongozo. Na nisawa malengo yawe ni mali au jaha. Wote hali moja.

{خُلِقَ الْإِنْسَانُ مِنْ عَجَلٍ ۚ سَأُرِيكُمْ آيَاتِي فَلَا تَسْتَعْجِلُونِ {37

***Mtu amaeumbwa na haraka. Nitawaonyesha ishara zangu, basi msiniharakishe.***

{وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَٰذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ {38

***Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi mnasema kweli?***

{لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ لَا يَكُفُّونَ عَنْ وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ ظُهُورِهِمْ وَلَا هُمْ يُنْصَرُونَ {39

***Lau wangelijua wale ambao wamekufuru wakati ambao hawatauzuia moto na nyuso zao wala migongo yao na wala hawatanusuriwa.***

{بَلْ تَأْتِيهِمْ بَغْتَةً فَتَبْهَتُهُمْ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ رَدَّهَا وَلَا هُمْ يُنْظَرُونَ {40

***Bali kitawafikia ghafla, na kitawashtua na wala hawataweza kukirudisha wala hawatapewa muda.***

{وَلَقَدِ اسْتُهْزِئَ بِرُسُلٍ مِنْ قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ {41

***Na hakika walifanyiwa stihzai Mitume kabla yako, kwa hiyo yakawazinga wale waliofanya miongoni mwao yale waliyokuwa wakiyafanyia sthizai.***

{قُلْ مَنْ يَكْلَؤُكُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ مِنَ الرَّحْمَٰنِ ۗ بَلْ هُمْ عَنْ ذِكْرِ رَبِّهِمْ مُعْرِضُونَ {42

***Sema ni nani atakayewalinda usiku na mchana na Mwingi wa rehema? Bali wao wanapuuza kumkumbuka Mola wao.***

{أَمْ لَهُمْ آلِهَةٌ تَمْنَعُهُمْ مِنْ دُونِنَا ۚ لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَ أَنْفُسِهِمْ وَلَا هُمْ مِنَّا يُصْحَبُونَ {43

***Au wao wana miungu watakaoweza kuwakinga nasi. Hao hawawezi kujinusuru wala hawatahifadhiwa nasi.***

بَلْ مَتَّعْنَا هَٰؤُلَاءِ وَآبَاءَهُمْ حَتَّىٰ طَالَ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ ۗ أَفَلَا يَرَوْنَ أَنَّا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا ۚ أَفَهُمُ الْغَالِبُونَ
{44}

***Bali tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka umri ukawa mrefu. Je, hawaoni kuwa tunaifikia ardhi tukiipunguza ncha zake; basi je, hao ni wenye kushinda?***

# Aya 37 – 44: Mtu Ameumbwa Na Haraka

## Lugha

Kuna tofauti baina ya haraka na upesi upesi (chapuchapu). Haraka ni kufanya jambo kabla ya wakati wake. Upesi upesi ni kulifanya jambo mara tu unapofika wakati wake bila ya ngojangoja. Kulifanya jambo upesi upesi kunasifika. Mwenyezi Mungu anasema:

> {وَيُسَارِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَأُولَٰئِكَ مِنَ الصَّالِحِينَ {114

***"Wanafanya upesiupeesi mambo ya kheri na hao ndio miongoni mwa watu wema." Juz.4*** **(*3:114*)**

Kuna kauli masuhuri isemayo: 'Haraka inatokana na shetani[1]

## Maana

**Mtu amaeumbwa na haraka. Nitawaonyesha ishara zangu, basi msini- harakishe.**

Mtume (s.a.w.) aliwahadharisha makafiri na matokeo ya ukafiri na akawahadharisha na adhabu ya Mwenyezi Mungu kama wakiendelea, lakini walizidi kiburi na inadi. Wakafanya masikhara ya kuharakisha adhabu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akawaambia, ngojeni mtaona ukweli wa Mtume wangu katika yale aliyowapa kiaga na akawahadharisha kuwa msiaharakie jambo ambalo litakuwa. Mara ngapi anayeharakia jambo likimfikia anatamani, lau lisingekuwa. Wafasiri wamesema, wakifafanua Aya hii, kuwa mtu ana maumbile ya kutaka haraka haraka, na kwamba hiyo iko katika mishipa yake na nyama yake.
Lakini kama ingelikuwa sawa hivyo, basi kusingepatikana utulivu wowote; bali kila mtu angelikuwa na haraka haraka katika kauli zake na vitendo vyake vyote, bila ya kubakia.

Ikiwa utamsifia mtu kwa haraka, kufuru au kukata tamaa n.k. utakuwa unafasiri silika yake katika baadhi ya hali zake, lakini sio kuwa ndio maumbile yake yote. Tumeyafafanua hayo kwa urefu, katika Juz. 12 (11:9) na Juz. 13 (14: 34).

**Na wanasema: "Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi mnasema kweli?**

Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 ( 7:70), Juz. 9 (7:107) na Juz. 12 (11: 32).

**Lau wangelijua wale ambao wamekufuru wakati ambao hawatauzuia moto na nyuso zao wala migongo yao na wala hawatanusuriwa.**

Makafiri wanaharakia adhabu na wao ni wadhaifu na wako duni kuweza kuizuia au kuweza kuikimbia. Watawezaje, nayo itawagubika kutoka juu yao hadi chini na mbele yao hadi nyuma?

**Bali kitawafikia ghafla, na kitawashtua na wala hawataweza kukirudisha wala hawatapewa muda.**

Kitakachowafikia ghafla ni Kiyama. Hakuna shaka kuwa kitawajia ghafla bila ya onyo lolote. Hiyo inatokana na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{يَسْأَلُكَ النَّاسُ عَنِ السَّاعَةِ ۖ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ اللَّهِ ۚ {63

***"Wanakuuliza kuhusu saa (ya Kiyama). Sema hakika elimu yake iko kwa Mwenyezi Mungu tu." (33:63).***

Ikiwa kitakuja kwa hali hii basi ni lazima kilete mshtuko na mashangao. Kwa hiyo hawataweza kukizuia wala hakitawapa muda wa kupanga mambo yao.

**Na hakika walifanyiwa stihzai Mitume kabla yako, kwa hiyo ya kawazinga wale waliofanya miongoni mwao yale waliyokuwa wakiyafanyia sthizai.**

Imetangulia Aya hii katika Juz. 7 (6:10).

**Sema, ni nani atakayewalinda usiku na mchana na Mwingi wa rehema.**

Kadiri mtu atakavyochukua hadhari na kujificha hawezi kujilinda na mambo ya ghafla, isipokuwa kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na tawfiki yake. Anawezaje kujilinda mtu na uwezo wa Mungu?

**Bali wao wanapuuza kumkumbuka Mola wao.**

Waliwafanyia sthizai Mitume wa Mwenyezi Mungu, wakajiaminisha na adhabu ya Mwenyezi Mungu na wakapuuza dhikri ya Mwenyezi Mungu; kwa nini? Kwa sababu wako kwenye starehe, wakiiona kuwa hiyo ni ngome ya kujihifadhi.

**Au wao wana miungu watakaoweza kuwakinga nasi,** kutokana na adhabu yetu tukitaka kuwaangamiza na kuwang'oa?

**Hao hawawezi kujinusuru wala hawatahifadhiwa nasi.**

Hao ni hao miungu wao. Kwa maana kwamba washirikina wanataka hifad- hi kwa masanamu, wakati

hayo yenyewe hayawezi kujisaidia, hayawezi kujinufaisha na chochote, yatawezaje kumsaidia mwingine?

Katika *Tafsirut-tabari* imeelezwa kuwa watu wa taawili wametofautiana katika neno *yusbihun*. Baada ya kunukuu kauli kadhaa, alichagua maana ya kuhifadhiwa. Maana haya ndiyo yanayoafikiana na kauli yake Mwenyezi Mungu katika (23:88).

**Bali tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka umri ukawa mrefu.**

Mwenyezi Mungu amewapa muda na maisha wakaghurika na muda wakawa wajeuri na wabaya; hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anawangoja na anawavuta polepole bila ya kujijua.

**Je, hawaoni kuwa tunaifikia ardhi tukiipunguza ncha zake. Basi je, hao ni wenye kushinda?**

Imetangulia pamoja na tafsiri yake katika Juz. 13: (13:41).

{قُلْ إِنَّمَا أُنْذِرُكُمْ بِالْوَحْيِ ۚ وَلَا يَسْمَعُ الصُّمُّ الدُّعَاءَ إِذَا مَا يُنْذَرُونَ {45

***Sema: Hakika mimi ninawaonya kwa wahyi tu. Na viziwi hawasikii mwito wanapoonywa.***

{وَلَئِنْ مَسَّتْهُمْ نَفْحَةٌ مِنْ عَذَابِ رَبِّكَ لَيَقُولُنَّ يَا وَيْلَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ {46

***Na watakapoguswa na mpulizo mmoja wa adhabu itokayo kwa Mola wako, bila shaka watasema: Ole wetu! Hakika tulikuwa ni wenye kudhulumu.***

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۖ وَإِنْ كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا ۗ وَكَفَىٰ بِنَا
{حَاسِبِينَ {47

***Na tutaweka mizani ya uadilifu kwa siku ya Kiyama. Basi nafsi yoyote haitadhulumiwa kitu. Hata ikiwa ni chembe ya khardali tutaileta. Nasi tunatosha kuwa wenye kuhisabu.***

{وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ وَهَارُونَ الْفُرْقَانَ وَضِيَاءً وَذِكْرًا لِلْمُتَّقِينَ {48

***Na hakika tulimpa Musa na Harun, upambanuzi, mwangaza na ukumbusho kwa wenye takua.***

{الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ بِالْغَيْبِ وَهُمْ مِنَ السَّاعَةِ مُشْفِقُونَ {49

***Ambao humwogopa Mola wao faraghani na wanaiogopa saa (ya Kiyama).***

{وَهَٰذَا ذِكْرٌ مُبَارَكٌ أَنْزَلْنَاهُ ۚ أَفَأَنْتُمْ لَهُ مُنْكِرُونَ {50

***Na huu ni ukumbusho uliobarikiwa ulioteremshwa. Basi je, mnaukataa?***

1. Waswahili nao wana misemo: 'Haraka haraka haina baraka' –Mtarjumu

# Aya 45 – 50: Nawaonya Kwa Wahyi

## Maana

**Sema: Hakika mimi ninawaonya kwa wahyi tu. Na viziwi hawasikii mwito wanapoonywa.**

Aya hii ni mfano wa kauli yake Mwenyezi Mungu:

{وَقُلْ إِنِّي أَنَا النَّذِيرُ الْمُبِينُ {89

***"Na, sema: Hakika mimi ni muonyaji niliye dhahiri." Juz. 14 (15:89).***

Mwenyezi Mungu anamwamrisha Mtume wake mtukufu awaambie washirikina kuwa mnakifanyia masikhara Kiyama na vituko vyake na habari hiyo ni wahyi wa Mwenyezi Mungu sio mawazo au njozi. Mimi nawahadharisha kwa amri ya Mwenyezi Mungu sio kwa amri yangu. Lakini mtawezaji kusikia hadhari na maonyo na kwenye masiko yenu kuna uziwi.
Kila asiyeitikia nasaha za Mwenyezi Mungu basi huyo ni kipofu na kizizwi, hata kama ana macho na masikio.

**Na watakapoguswa na mpulizo mmoja wa adhabu itokayo kwa Mola wako, bila shaka watasema: "Ole wetu! Hakika tulikuwa ni wenye kudhulumu.**

Hapo mwanzo walikuwa wanapoonywa kwa adhabu, wakifanya masikhara na mizaha, lakini itakapowagusa kidogo tu wataanza kulalamika na kunyenyekea huku wakisema: 'Ole wetu sisi tulikuwa madhalimu.' Umetangulia mfano wake katika sura hii Aya 14.

## Mizani Siku Ya Kiyama

**Na tutaweka mizani ya uadilifu kwa siku ya Kiyama. Basi nafsi yoyote haitadhulumiwa kitu. Hata ikiwa ni chembe ya khardali tutaileta. Nasi tunatosha kuwa wenye kuhisabu.**

Makusudio ya mizani hapa ni hukumu ya Mwenyezi Mungu na sharia yake. Maana ni kuwa Mwenyezi

Mungu (s.w.t.) anapima matendo ya waja kwa amri zake na makatazo yake. Ambaye atafanya matendo yake kulinga na na amri na makatazo yake, basi ni katika ambao mizani zao zitakuwa nzito.

Imam Jafar As-Sadiq (a.s.) aliulizwa kuhusu mizani za uadilifu, akasema ni manabii wa Mwenyezi Mungu na mawalii wake; yaani hukumu za Mwenyezi Mungu zinazofikishwa na mitume na mawalii katika waja wake.

Malipo yatakuwa kulingana na misingi hii; hazitapunguzwa thawabu za mwema hata chembe, pengine inawezekana kuzidishwa. Wala haitazidishwa adhabu ya muovu hata chembe, pengine inawezekana kupunguzwa.

**Nasi tunatosha kuwa wenye kuhisabu,** hatutaziki wala hakitupiti kitu kadiri idadi yake itakavyokuwa.

Mulla Sadra katika Kitabu *Al-asfar* anasema: "Uwezo wa Mwenyezi Mungu unafichua matendo yote ya waja wake na kipimo cha mema yao, maovu yao na thawabu zake na adhabu yake katika kitambo kidogo, naye ni mwepesi wa kuhisabu"

Kama ataizingatia Aya hii, mwenye kujaribu kuifuatishia Qur'an na sayansi, atasema kianzio cha fikra ya akili ya mashine ni Qur'an. Angalia kifungu cha 'Qur'an na sayansi' katika mwanzo wa Juzuu ya kwanza.

Mwenye *Al-Asfar* amezungumzia kwa urefu kuhusu mizani ya siku ya Kiyama. Kwa kuangalia uwezo wa mtungaji katika falsafa ya itikadi n.k. Tutachukukua baadhi ya ibara zake, kama ifuatavyo, pamoja na nyongeza kidogo kwa ajili ya ufafanuzi:

"Mizani ya Akhera ni ile ambayo hujulikana kwayo usahihi wa elimu, imani ya Mungu, sifa zake, vitendo vyake, malaika wake, mitume wake, vitabu vyake na siku ya mwisho.

Mizani hii ni Qur'an ambayo ameiteremsha mwalimu wa kwanza, ambaye ni Mwenyezi Mungu, kwa mwalimu wa tatu, ambaye ni Mtume, kupita kwa mwalimu wa pili ambaye ni Jibril.

Kwa hukumu ya Qur'an ndio hupimwa elimu ya mtu, akili yake, kauli na vitendo vyake vyote. Vile vile hujulikana mema yake na maovu yake. Ikiwa wema utazidi basi mwenyewe atakuwa ni katika wema na ikiwa uovu utazidi basi atakuwa katika waovu.

Ikiwa mema na maovu yatalingana, basi mwenyewe atangojea mpaka Mungu amuhukumie adhabu au msamaha, lakini upande wa hurumma ndio ulio na nguvu zaidi. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu"

Kisha akasema - mweneye *Al-asfar* – mahali pengine: "Kila kitu kina mizani isipokuwa neno: "*Lailaha illa-llah*, (Hapana Mola isipokuwa Allah) kwa sababu neno hilo la tawhid halina mkabala na jambo lolote isipokuwa shirk, na shirki haina mizani."

Akaendelea kusema tena mahali pengine: "Hakika Qur'an ni kama meza yenye aina kwa aina ya

vyakula, kuanzia vyakula halisi hadi maganda. Kile halisi ni hekima na dalili na kinahusika na wenye busara. Ama maganda ni ya walio mbumbumbu ambao ni kama wanyama; kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

{مَتَاعًا لَكُمْ وَلِأَنْعَامِكُمْ {32

***“Kwa ajili ya manufaa yenu na wanyama wenu.”* (*80:32*)**.

Kwa haraka haraka mtu anaweza akadhani kuwa ibara ya maganda ni kukikosea adabu Kitabu cha Mwenyezi Mungu na utukufu wake, lakini mwenye *Asfar* yuko zaidi ya dhana na shakashaka. Mwenye kuyachunguza na kuyataamali maneno yake atajua kuwa makusudio ya maganda ni watu wa hayo maganda, kama wale wanaoganda kwenye dhahiri ya maneno bila ya kuangalia undani wake, hawaoni mbali zaidi ya pua zao, kwa dalili ya yale aliyoyaeleza alipokuwa akifafanua Hadith ya Mtume isemayo: “Qur’an ina dhahiri na batini.”

Hadith hii ameifafanua kwa maneno marefu; miongoni mwa maneno hayo ni haya yafutayo: “Hakika Qur’an ina daraja kama vile watu ambao wako wenye akili na wasiokuwa na akili. Asiye na akili ni kama yule anayechukua mambo kijujuu. Ama roho ya Qur’an na siri yake haigundui isipokuwa mwenye akili na busara. Kwa hiyo mgawanyiko unakuja kutokana na wanavyoifahamu Qur’an sio Qur’an yenyewe.

**Na hakika tulimpa Musa na Harun, upambanuzi, mwangaza na ukumbusho kwa wenye takua**.

Makusudio ya upambanuzi hapa ni Tawrat, kama alivyoiteremsha Mwenyezi Mungu kwa Musa. Kila Kitabu cha mbinguni ni upambanuzi, kwa sababu kinapambanua uongofu na upotevu, ni mwangaza wa kuondoa giza la ujinga na ukafiri na ukumbusho kwa mwenye kuitafuta takua, kwa sababu kina mkumbusha kuhusu Mwenyezi Mungu na kumbainishia halali na haramu.

**Ambao humwogopa Mola wao faraghani na wanaiogopa saa (ya Kiyama).**

Haya ndiyo maelezo ya wenye takua, kwamba wao wanamcha Mwenyezi Mungu kwa siri kusiko na watu; sawa na vile wanavyomcha dhahiri. Kwa vile wana imani siku ya Kiyama, hisabu na malipo, huku wakiiogopa siku hiyo na kuifanyia kazi.

**Na huu ni ukumbusho uliobarikiwa ulioteremshwa**.

Ni ukumbusho kwa mwenye kutaka kukumbuka, ni mawaidha kwa mwenye kuwaidhika na ni kheri kwa mwenye kuamrika na maarisho yake na kukatatiza kwa makatazo yake.

**Basi je, mnaukataa?**

Na hali hoja na dalili zake ziko wazi.

{وَلَقَدْ آتَيْنَا إِبْرَاهِيمَ رُشْدَهُ مِنْ قَبْلُ وَكُنَّا بِهِ عَالِمِينَ {51

***Na hakika tulikwisha mpa Ibrahim uongofu wake zamani na tulikuwa tunamjua.***

{إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا هَٰذِهِ التَّمَاثِيلُ الَّتِي أَنْتُمْ لَهَا عَاكِفُونَ {52

***Alipomwambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu mnayoyanga'ng'ania?***

{قَالُوا وَجَدْنَا آبَاءَنَا لَهَا عَابِدِينَ {53

***Wakasema: Tumewakuta baba zetu wakiyaabudu.***

{قَالَ لَقَدْ كُنْتُمْ أَنْتُمْ وَآبَاؤُكُمْ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ {54

***Akasema: Hakika nyinyi na baba zenu mmekuwa kwenye upotofu ulio dhahiri.***

{قَالُوا أَجِئْتَنَا بِالْحَقِّ أَمْ أَنْتَ مِنَ اللَّاعِبِينَ {55

***Wakasema: Je, umetujia kwa haki au wewe ni katika wafanyao mchezo?***

{قَالَ بَلْ رَبُّكُمْ رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ الَّذِي فَطَرَهُنَّ وَأَنَا عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ {56

***Akasema: Bali Mola wenu ni Mola wa mbingu na ardhi ambaye ndiye aliyeziumba, na mimi ni katika wenye kuyashuhudia hayo.***

{وَتَاللَّهِ لَأَكِيدَنَّ أَصْنَامَكُمْ بَعْدَ أَنْ تُوَلُّوا مُدْبِرِينَ {57

***Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Nitayafanyia vitimbi masanamu yenu baada ya kunipa mgogo.***

{فَجَعَلَهُمْ جُذَاذًا إِلَّا كَبِيرًا لَهُمْ لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ يَرْجِعُونَ {58

***Basi akayavunja vipande vipande isipokuwa kubwa lao ili wao walirudie.***

{قَالُوا مَنْ فَعَلَ هَٰذَا بِآلِهَتِنَا إِنَّهُ لَمِنَ الظَّالِمِينَ {59

***Wakasema: Ni nani aliyeyafanyia haya miungu wetu? Hakika huyu ni katika madhalimu.***

{قَالُوا سَمِعْنَا فَتًى يَذْكُرُهُمْ يُقَالُ لَهُ إِبْرَاهِيمُ {60

***Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahim.***

# Aya 51-60: Ibrahim

## Maana

**Na hakika tulikwisha mpa Ibrahim uongofu wake zamani na tulikuwa tunamjua.**

Wametofautiana wafasiri kuhusu maana ya uongofu. Ikasemekana kuwa ni kuongoka kwenye utengenefu wa dini na dunia. Pia ikasemekana kuwa ni utume.

Kauli hii ndiyo yenye nguvu zaidi kwa dalili ya kauli 'zamani' maana yake ni kabla ya mitume waliokuja baada ya Ibrahim (a.s.); kama vile Musa (a.s.), Isa (a.s.) na Muhammad (s.a.w.). Pia kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu 'Na tulikuwa tunamjua' ambayo maana yake ni kauli yake:

{اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ {124

***"Mwenyezi Mungu diye Mjuzi zaidi wa kujua mahali anapoweka ujumbe wake." Juz. (6:124).***

Utume unatoka kwa Mungu, anamuhusisha nao mwenye kuustahiki, wala haupatikanai kwa bidii ya mtu; kama vile imani na takua. Ndio maana husemwa kuwa mumin, kuwa mcha Mungu, lakini haisemwi kuwa Mtume.

**Alipomwambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu mnayoyanga'ng'ania?**
Swali hili linaelekezwa kwa kila mwenye majukumu ya matendo yake na matumizi yake. Vipi mnavitukuza na kuviabudu visivyodhuru wala kunufaisha; na nyinyi mna akili na utambuzi?

**Wakasema: Tumewakuta baba zetu wakiyaabudu.**

Mantiki hii anaikimbilia kila mwenye kushindwa na hoja na dalili. Ukimuuliza kwa nini umefanya hivi, atasema: Fulani amefanya.

Hakuna la kuwaambia watu wa aina hii, isipokuwa kauli ya Nabii Ibrahim:

**Akasema: Hakika nyinyi na baba zenu mmekuwa kwenye upotofu ulio dhahiri.**

Na upotofu hauwezi kubadilika kuwa uongofu hata ukifuatwa na wengi.

**Wakasema: Je, umetujia kwa haki au wewe ni katika wafanyao mchezo?**

Walijitia mshangao kutokana na kauli ya Ibrahim, kwa vile wanawaona baba zao wametakaswa na makosa; si kwa lolote ila ni kwa kuwa ni baba zao tu.

Mantiki haya hawahusiki nao kaumu ya Ibrahim tu, wala washirikina wengine; bali kila mwenye kuigiza wengine kwa upofu, yuko sawa na waabudu masanamu.

**Akasema: Bali Mola wenu ni Mola wa mbingu na ardhi ambaye ndiye aliyeziumba,**

Mimi sifanyi mchezo wala sitii shaka. Vipi nifanye mchezo na kutia shakashaka na hali Yeye ndiye muumba wa mbingu na ardhi **na mimi ni katika wenye kuyashuhudia hayo?**

**Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Nitayafanyia vitimbi masanamu yenu baada ya kunipa mgogo.**

Ilivyo ni kwamba masanamu hayawezi kufanyiwa vitimbi, kwa sabau hayana hisia; isipokuwa wanaofanyiwa vitimbi ni waabudu masanamu, kwa hiyo kuyafanyia vitimbi ni majazi, sio hakika; isipokuwa yamefanywa ni nyenzo ya kufanyiwa vitimbi wanaoyaabudu.

**Basi akayavunja vipande vipande isipokuwa kubwa lao ili wao walirudie.**

Ibrahim aliyavunja masanamu yote na akaliacha lile kubwa lao, ili wale wanaoyaabudu waliulize, kwa nini halikuweza kuwatetea wenzake wadogo nalo lina nguvu? Makusudio yako wazi; nayo ni kuwa washirikina wazingatie kuwa masanamu haya ikiwa hayo yenyewe hayawezi kujitetea, basi ndio hayawezi kumtetea mwengine.

**Wakasema: Ni nani aliyeyafanyia haya miungu wetu? Hakika huyu ni katika madhalimu.**

Usawa ni kuwa waulize miungu yao imemfanyia nini aliyeyavunja? Lakini haya ndiyo mantiki ya kijinga na kuiga.

**Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahim.**

Hii inaashiria kauli ya Ibrahim (a.s.): “Nitayafanyia vitimbi masanamu yenu.”

Baada ya kuandika Juzuu ya sita, nilisoma kwenye mojawapo ya magazeti, kwamba wafukuaji, wamegundua mji wa kwanza wa Ibrahim, Uru. Ikabainika kwamba watu wake walikuwa wakiabudu nyota tatu: ndogo, wastani na kubwa.

Kwa hiyo mpangilio huu uliokuja katika Qur’an kupitia ulimi wa Ibrahim ndio mpangilio wa kimantiki ambao unafuatana na maisha ya wakati huo. Hivi ndivyo elimu inavyoleta dalili kila siku juu ya ukweli wa

Muhammad (s.a.w.) katika kila aliyoyaelezea.

{قَالُوا فَأْتُوا بِهِ عَلَىٰ أَعْيُنِ النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَشْهَدُونَ }61

***Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu, wapate kumshuhudia.***

{قَالُوا أَأَنْتَ فَعَلْتَ هَٰذَا بِآلِهَتِنَا يَا إِبْرَاهِيمُ }62

***Wakasema: Je, wewe ndiwe uliyeifanyia haya mingu yetu ewe Ibrahim?***

{قَالَ بَلْ فَعَلَهُ كَبِيرُهُمْ هَٰذَا فَاسْأَلُوهُمْ إِنْ كَانُوا يَنْطِقُونَ }63

***Akasema: Bali ameyafanya hayo mkubwa wao huyu. Basi waulizeni ikiwa wanatamka.***

{فَرَجَعُوا إِلَىٰ أَنْفُسِهِمْ فَقَالُوا إِنَّكُمْ أَنْتُمُ الظَّالِمُونَ }64

***Basi wakajirudi nafsi zao. Wakasema: Hakika nyinyi ndio madhalimu.***

{ثُمَّ نُكِسُوا عَلَىٰ رُءُوسِهِمْ لَقَدْ عَلِمْتَ مَا هَٰؤُلَاءِ يَنْطِقُونَ }65

***Kisha wakasimamia vichwa vyao. Wewe unajua kwamba hawa hawasemi.***

{قَالَ أَفَتَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكُمْ شَيْئًا وَلَا يَضُرُّكُمْ }66

***Akasema: Basi nyinyi mnaabudu badala ya Mwenyezi Mungu visivyo wanufaisha kitu wala kuwadhuru?***

{أُفٍّ لَكُمْ وَلِمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۖ أَفَلَا تَعْقِلُونَ }67

***Kefule yenu na mnavyoviabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Basi hamtii akili?***

{قَالُوا حَرِّقُوهُ وَانْصُرُوا آلِهَتَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ فَاعِلِينَ }68

***Wakasema: Mchomeni na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo.***

{قُلْنَا يَا نَارُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ {69

***Tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!***

{وَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَخْسَرِينَ {70

***Na wakamtakia ubaya, lakini tukawafanya wao ndio wenye kupata hasara.***

# Aya 61 – 70: Wakasema: Mleteni

## Maana

**Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu, wapate kumshuhudia.**

Walitaka wamsaili na kumhukumu mbele ya watu wamshuhudie; kisha waone adhabu itakayompata.

**Wakasema: Je, wewe ndiwe uliyeifanyia haya mingu yetu ewe Ibrahim?**

Walimleta na wakaanza kumhoji. Akasema:

**Bali ameyafanya hayo mkubwa wao huyu. Basi waulizeni ikiwa wanatamka.**
Kutamka ni katika hali ya kukadiria; ikiwa hawa wana hisia basi aliyefanya ni mkubwa wao. Mfano kusema: ikiwa Mwenyezi Mungu ana mtoto, basi mimi ni wa mwanzo wa wenye kumwabudu.

Kwa ujumla ni kwamba makusudio ni kuwanyamazisha kwa hoja, na kwamba masanamu haya, kama yangekuwa ni Mungu yangelikuwa na utambuzi, kusema na kumvunajilia mbali anayetaka kuyafanyia ubaya.

**Basi wakajirudi nafsi zao.**

Baada ya kusikia aliyoyasema Ibrahim (a.s.) waliulizana: Vipi tuabudu mawe na kutarajia kheri na kuhofia shari yake na hayo yenyewe hayawezi kujikinga na madhara.

**Wakasema: Hakika nyinyi ndio madhalimu.**

Waliishia kukiri kuwa wao wako katika ujinga, lakini mara tu wakarudia kwenye hali yao ya mwanzo.

**Kisha wakasimamia vichwa vyao.**

Makusudio ya kusimamia vichwa hapa ni kurudi kwenye uovu wao. Neno lililotumika ni *nukisu* lenye

maana ya kuweka kichwa chini miguu juu. Yaani kumpa silaha adui yako akuue nayo, au kumpa hoja mtu kutokana na vitendo vyako au kauli yako; kama walivyofanya kaumu ya Ibrahim, waliposema:

**Wewe unajua kwamba hawa hawasemi.**

Ikiwa hawasemi, basi vipi mnawaabudu. At–Tabariy anasema: "Kupindua jambo ni kulifanya kichwa chini miguu juu na kupindua hoja ni kuifanya hoja ya hasimu wako ndio hoja yako; kama walivyofanya kaumu ya Ibrahim."

**Akasema: Basi nyinyi mnaabudu badala ya Mwenyezi Mungu visivyo wanufaisha kitu wala kuwadhuru?**

Nyinyi mnajua kuwa haya masanamu hayana utambuzi wala matamshi, hayadhuru wala hayanufaishi, basi vipi mnayaabudu?

**Kefule yenu na na mnavyoviabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Basi hamtii akili?**

Utafanya nini na watu wanaong'ang'ania upotevu na wao wanajua kuwa huo ni upotevu. Hakuna cha kuwafanya isipokuwa kuwaaambia: poteleeni mbali, enyi mnaofanana na watu na wala sio watu.

**Wakasema: Mchomeni na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo.**

Wanusuruni miungu, lakini miungu yenyewe haiwezi kujinusuru, na bado ni miungu tu! Ni sawa na yule aliyesema: 'Huyo ni paa hata kama ameruka angani.' Huko ndiko kuweka kichwa chini miguu juu.

**Tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!**

Walisema na Mwenyezi Mungu naye akasema. Wala hakuna mwenye kurudisha kauli yake.

Unaweza kuuliza: Kwa kawaida moto unaunguza, vipi uwe baridi.

Jibu: Mwenye kuleta athari wa kwanza kwa kila kilichpo ni Mwenyezi Mungu ambaye umetukuka ukuu wake. Yote hutokana na Yeye, na kwake zinaishia nyenzo zote, ziwe ni sharti, sababu au chochote. Kuunguza kunatokana na moto, moto unatokana na kuni, kuni ni maumbile yaliyotokana na neno lake.

Yeye ndiye aliyeumba moto ambao unaunguza, lakini kwa sharti ya kutouambia 'kuwa baridi.' Kwa hiyo kama atauambia hivyo utakuwa kama alivyosema. Kwa maneno mengine ni kuwa kuunguza kwake na kuwa baridi kwake kunafuta matakwa ya Mungu kutokana na kuumba kwake na kuufanya uweko.

**Na wakamtakia ubaya, lakini tukawafanya wao ndio wenye kupata hasara.**

Waliwasha moto ili umchome Ibrahim, lakini ukawa ni muujiza mkubwa na dalili ya kuthibitisha ukweli wake na utume wake:

{وَمَكَرُوا وَمَكَرَ اللَّهُ ۖ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَاكِرِينَ {54

***“Na wakapanga hila; na Mwenyezi Mungu akapanga hila; na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa kupanga hila” Juz. 3*** (***3:54***).

Katika baadhi ya tafsiri za zamani, imeelezwa kuwa Namrud alipoona moto haumuathiri Ibrahim, aliamuru mali zake zichukuliwe na yeye mwenyewe atolewe nchini.

Ibrahim akasema: Mkichukua mali zangu basi nirudishieni umri wangu nilioumaliza kwenye nchi yenu. Wakaenda mahakamani, hakimu akatoa hukumu ya kunyang’anyawa mali Ibrahim na Namrud amrudishie umri wake. Hapo akasalimu amri na akamwacha Ibrahim na mali zake. Hekaya hii hatukuinukuu kwa kuamini kuwa ni kwali hivyo; isipokuwa inaonyesha kuwa kila mtu ana haki ya umri wake alioumaliza kwa sharti ya kuwa ameutumia kwenye halali.

{وَنَجَّيْنَاهُ وَلُوطًا إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي بَارَكْنَا فِيهَا لِلْعَالَمِينَ {71

***Na tukamwokoa yeye na Lut tukawapeleka kwenye ardhi tuliyoibariki, kwa ajili ya walimwengu wote.***

{وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً ۖ وَكُلًّا جَعَلْنَا صَالِحِينَ {72

***Naye tukampa Is-haq na Yakub kuwa ni zawadi. Na wote tukawajaalia wawe watu wema.***

{وَجَعَلْنَاهُمْ أَئِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِمْ فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَإِقَامَ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءَ الزَّكَاةِ ۖ وَكَانُوا لَنَا عَابِدِينَ {73

***Na tukawafanya maimamu wakiongoza kwa amri yetu. Na tukawapa wahyi watende kheri na wasimamishe Swala na watoe Zaka na walikuwa wanatuabudu sisi.***

{وَلُوطًا آتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا وَنَجَّيْنَاهُ مِنَ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ تَعْمَلُ الْخَبَائِثَ ۗ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمَ سَوْءٍ فَاسِقِينَ {74

***Na Lut tukampa hukumu na elimu na tukamwokoa na ule mji uliokuwa ukifanya maovu. Hakika hao walikuwa wabaya, mafasiki.***

{وَأَدْخَلْنَاهُ فِي رَحْمَتِنَا ۖ إِنَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ {75

***Na tukamwingiza katika rehema zetu. Hakika yeye ni miongoni mwa walio wema.***

{وَنُوحًا إِذْ نَادَىٰ مِنْ قَبْلُ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ {76

***Na Nuh alipoita zamani, nasi tukamwitikia na tukamwokoa yeye na watu wake kutokana na shida kubwa.***

{وَنَصَرْنَاهُ مِنَ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمَ سَوْءٍ فَأَغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ {77

***Na tukamnusuru na watu waliozikadhibisha Ishara zetu. Hakika hao walikuwa watu wabaya. Basi tukawagharikisha wote.***

# Aya 71 – 77: Tukamwokoa Yeye Na Lut

## Maana

**Na tukamwokoa yeye na Lut tukawapeleka kwenye ardhi tuliyoibariki, kwa ajili ya walimwengu wote.**

Makusudio ya aliyeokolewa hapa ni Ibrahim (a.s.). Lut ni mtoto wa kaka yake. Katika Tafsiri imelezwa kuwa Ibrahim aliondoka akaelekea nchi ya Sham, ambayo ndani ilikuwako Palestina.

Vyovyote iwavyo ni kwamba makusudio ni kumfananisha Muhammad (s.a.w.) na kaumu yake pamoja na Ibrahim (a.s.) na kaumu yake.

Kaumu zote mbili ziliabudu masanamu, zikakataa mwito wa nabii wao na kujaribu kumuua. Manabii wote wawili Mungu aliwaokoa na kuwatengenezea njia ya hijra na kuwaneemesha kwa hijra hiyo.

**Naye tukampa Is-haq na Yakub kuwa ni zawadi.**

Is-haq ni mtoto wa Ibrahim wa kumzaa, na Yakub ni mjukuu naye ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

**Na wote tukawajaalia wawe watu wema.**

Ibrahim, Is-haq , wote walikuwa wema.

**Na tukawafanya maimamu wakiongoza kwa amri yetu. Na tukawapa wahyi watende kheri na wasimamishe Swala na watoe Zaka na walikuwa wanatuabudu sisi.**

Maimamu ndio viongozi wa dini ambao amewateua Mwenyezi Mungu, kuwaongoza waja. Sifa yao kuu

ni kwamba wao wanaongoza watu kama alivyoamrisha Mungu, si kama wanavyoamrisha wake zao, watoto wao au wakwe zao; wanahimiza kufanya kheri sio chuki za utaifa; na kumfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu peke yake sio mwenginewe.

**Na Lut tukampa hukumu na elimu na tukamwokoa na ule mji uliokuwa ukifanya maovu. Hakika hao walikuwa wabaya, mafasiki. Na tukamwingiza katika rehema zetu. Hakika yeye ni miongoni mwa walio wema.**

Tazama tafsiri yake katika Juz. 8 (7: 80) na Juz 12 (11:77).

**Na Nuh alipoita zamani, nasi tukamwitikia na tukamwokoa yeye na watu wake kutokana na shida kubwa. Na tukamnusuru na watu waliozikadhibisha Ishara zetu. Hakika hao walikuwa watu wabaya. Basi tukawagharikisha wote.**

Kisa cha Nuh kimetangulia katika Juz. 12 (11:25).

{وَدَاوُودَ وَسُلَيْمَانَ إِذْ يَحْكُمَانِ فِي الْحَرْثِ إِذْ نَفَشَتْ فِيهِ غَنَمُ الْقَوْمِ وَكُنَّا لِحُكْمِهِمْ شَاهِدِينَ {78

***Na Daud na Suleiman walipohukumu juu ya shamba, walipolisha humo mbuzi wa watu usiku. Na sisi tulikuwa wenye kushuhudia hukumu yao.***

{فَفَهَّمْنَاهَا سُلَيْمَانَ ۚ وَكُلًّا آتَيْنَا حُكْمًا وَعِلْمًا ۚ وَسَخَّرْنَا مَعَ دَاوُودَ الْجِبَالَ يُسَبِّحْنَ وَالطَّيْرَ ۚ وَكُنَّا فَاعِلِينَ {79

***Tukamfahamisha Suleiman na kila mmoja wao tukampa hukumu na elimu. Na tuliifanya milima na ndege kuwa pamoja na Daud imnyenyekee na imsabihi (Mwenyezi Mungu). Na sisi tulikuwa ni wenye kuifanya.***

{وَعَلَّمْنَاهُ صَنْعَةَ لَبُوسٍ لَكُمْ لِتُحْصِنَكُمْ مِنْ بَأْسِكُمْ ۖ فَهَلْ أَنْتُمْ شَاكِرُونَ {80

***Na tukamfundisha kutengeneza mavazi ya vita ili kuwakinga katika mapigano yenu. Je, mtakuwa wenye kushukuru?***

{وَلِسُلَيْمَانَ الرِّيحَ عَاصِفَةً تَجْرِي بِأَمْرِهِ إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي بَارَكْنَا فِيهَا ۚ وَكُنَّا بِكُلِّ شَيْءٍ عَالِمِينَ {81

***Na upepo mkali kwa ajili ya Suleiman, wendao kwa amri yake, katika ardhi tuliyoibariki. Na sisi ndio tunaojua kila kitu.***

{وَمِنَ الشَّيَاطِينِ مَنْ يَغُوصُونَ لَهُ وَيَعْمَلُونَ عَمَلًا دُونَ ذَٰلِكَ ۖ وَكُنَّا لَهُمْ حَافِظِينَ {82

***Na katika mashetani kuna wanompigia mbizi na kufanya kazi nyinginezo; Nasi tulikuwa walinzi wao.***

# Aya 78 – 82: Daud Na Suleiman

## Maana

**Na Daud na Suleiman walipohukumu juu ya shamba, walipolisha humo mbuzi wa watu usiku. Na sisi tulikuwa wenye kushuhudia hukumu yao.**

Kuna riwaya iliyo mashuhuri midomoni mwa wapokezi, kwamba watu wawili walikwenda kuamuliwa kwa Daud. Mmoja alikuwa na mimea na wa pili alikuwa na mifugo ya mbuzi na kondoo. Mwenye shamba akasema wanyama wa huyu bwana wamelisha kwenye mimea yangu usiku. Baada ya kumthibitikia hilo, Daud alitoa hukumu kuwa wanyama wawe wa mwenye shamba.

Suleiman alipojua hivyo akasema, ni vizuri mwenye shamba awachukue wanyama, anufaike nao lakini wasiwe wake kabisa, na mwenye wanyama achukue ardhi aishghulikie mpaka iwe kama ilivyokuwa kabla ya kuliwa. Kisha bada ya hapo kila mmoja achukue mali yake. Daud akapendezewa na hukumu ya mwanawe na akaitumia.

Dhahiri ya Aya inaafikiana na riwaya hii. Imethibiti kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) kwamba yeye amesema: "Linaloafikiana na Qur'an lichukueni na linalokhalifiana nalo liacheni."

Unaweza kuuliza: Kila mmoja kati ya Daud na Suleiman ni Nabii na Nabii ni maasumu; hasa katika hukumu ya sharia na hukumu ya sawa, sasa je kuna wajihi gani wa kupingana hukumu mbili hizi?

Baadhi wamejibu kuwa kauli ya Daud ilikuwa ni upatanishi sio hukumu. Lakini ijulikane kuwa upatanishi unakuwa kwa baadhi ya mali sio yote na Daud hakumbakishia mfugaji hata mnyama mmoja.

Wengine wakasema kuwa kila mmoja kati ya manabii wawili hao alihukumu kwa ijitihadi yake. Kauli hii vile vile ina kasoro; kwamba Nabii anatumia ijitihadi kama ulama wengine na inajulikana kuwa rai ya ijtihadi inakuwa kwa kukosekana nukuu (*Nass*) na ilivyo ni kuwa kauli ya Nabii ni nukuu ya haki; na kwamba ijitihadi ina uwezekano wa kupatia na kukosea, jambo ambalo haliswihi kwa maasumu.

Jamaa wamesema kuwa hukumu ilikuwa kama alivyopitisha Daud; kisha ikabadilishwa (*naskh*), na kauli ya Suleiman[1]

Kauli hii ina nguvu zaidi kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**Tukamfahamisha Suleiman na kila mmoja wao tukampa hukumu na elimu.**

Hapo Mwenyezi Mungu anashudia kuwa kila mmoja ni mjuzi wa hukumu. Kwa hiyo basi kauli yake Mwenyezi Mungu 'Tukamfahamisha Suleiman' ni kwamba yeye alimpelekea wahyi wa kubadilisha hukumu ya baba yake. Mafaqihi wametofautiana kuwa je mwenye mifugo atalipa kilichoharibiwa na wanyama wake?

Maliki na Shafi wamesema kuwa atalipa kilichoharibiwa usiku sio mchana. Abu Hanifa akasema halipi kwa hali yoyote; iwe usiku au mchana.

Jamaa katika mafaqihi wa kishia wamesema kama alivyosema Maliki na Shafi na wahakiki katika wao wakasema kuwa litakaloangaliwa ni hali ya uzembe wa mfugaji au la; sio hali ya kuwa usiku au mchana. Ikiwa mfugaji atazembea au kufanya makusudi, basi atalipa. Na ikiwa atajichunga na asipuuze, ikatokea bahati mbaya basi hatalipa.

**Na tuliifanya milima na ndege kuwa pamoja na Daud imnyenyekee na imsabihi** (**Mwenyezi Mungu**). **Na sisi tulikuwa ni wenye kuifanya**.

Imekuwa mashuhuri kuwa Daud alikuwa na sauti nyororo. Majaribio yamethibitisha kuwa wanyama wengi wanaburudika na aina fulani ya nyimbo na muziki[2]. Niliwahi kusoma kwenye gazeti kwamba nyoka aliwahi kutoka kwenye tundu yake ili astarehe na nyimbo za Ummu Kulthum, katika moja ya hafla yake. Nyimbo ilipokwisha akarudi sehemu yake.

Ama tasbibih ya mlima ni kwa njia ya majazi na kusifia zaidi tu; kama kusema: Amelichekesha na kuliliza jiwe. Au inawezekana ni kiuhakika hasa. Kwa sababu yule aliyeweza kuufanya moto kuwa baridi na salama kwa Ibrahim, ndiye anaweza pia kulifanya jabali litoe tasbih pamoja na Daud.

Angalia Aya 69 ya Sura hii tuliyo nayo.

**Na tukamfundisha kutengeneza mavazi ya vita ili kuwakinga katika mapigano yenu**. **Je, mtakuwa wenye kushukuru?**

Makusudio ya mavazi ya vita hapa ni deraya. Aya inaonyesha kuwa Daud ndiye mtu wa kwanza kutengeneza deraya.

Kuna riwaya inayoelezea kwamba sababu ya hilo ni kuwa Daud alikuwa ni mfalme wa Israil na alikuwa ana desturi ya kupita mitaani kujulia hali za watu, bila ya yeye kujulikana. Siku moja akakutana na mtu akamuuliza kuhusu sera za mfalme Daud.

Yule mtu akasema: Ana sera nzuri sana, kama asingekuwa anakula kwenye hazina ya serikali. Daud akaapa kuwa kuanzia siku hiyo hatakula kitu isipokuwa kilichotokana na mikono yake na jasho lake.

Alipojua Mwenyezi Mungu ikhlasi yake na ukweli wa nia yake, alimalainishia chuma na kumfundisha kutengeneza deraya.

Iwe sahihi riwaya hii au la, ni kwamba inaashria wajibu wa kufanya bidii kubwa kuchunga masilahi ya watu na mali zao. Kuna Hadith mutawatir kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu, Muhammad (s.a.w.), alifariki akiwa ameweka rahani deraya yake kwa sababu ya kukopa kiasi fulani cha shayir, huku zikiwa mali za Bara arabu zote ziko mikononi mwake.

**Na upepo mkali kwa ajili ya Suleiman, wendao kwa amri yake, kati- ka ardhi tuliyoibariki. Na sisi ndio tunaojua kila kitu.**

Dhahiri ya Aya hii inafahamisha kuwa upepo ulikuwa ukimchukua Suleiman kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Wala hakuna haja ya kuleta taawili, maadamu akili inakubaliana na dhahiri hiyo.
Aya iliyo wazi zaidi ya hii ni ile isemayo: "Na Suleiman tukamtiishia upepo mwendo wake asubuhi ni mwezi mmoja na mwendo wake jioni yake ni mwezi mmoja." (34:12) Yaani asubuhi unakwenda mwendo wa mwezi mmoja kwa kusafiri na ngamia na jioni vile vile.

Makusudio ya ardhi iliyobarikiwa ni ile iliyotajwa kwenye Aya ya 71 ya Sura hii.

Unaweza kuuliza: Hapa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema upepo mkali na mahali pengine anasema: pole pole: "Na tukamtiishia upepo uendao polepole kwa amri yake." (38:36). Je, kuna wajihi gani wa Aya zote mbili?

Jibu: Huwa mara unakwenda kwa kasi na mara nyingine polepole kulin- gana na amri yake; sawa na gari au ndege.

**Na katika mashetani kuna wanompigia mbizi baharini na kumtolea lulu na marijani.**

Makusudio ya mashetani hapa ni majini

**Na kufanya kazi nyinginezo;** kama kujenga mihirabu na picha:

{يَعْمَلُونَ لَهُ مَا يَشَاءُ مِنْ مَحَارِيبَ وَتَمَاثِيلَ وَجِفَانٍ كَالْجَوَابِ وَقُدُورٍ رَاسِيَاتٍ ۚ {13

***"Wakimfanyia alipendalo, kama mihrabu na picha na masinia makubwa, kama hodhi na masufuria makubwa yasiyoondolewa mahali pake." (34:13).***

**Nasi tulikuwa walinzi wao,** kwamba wasitoroke na kufanya ukorofi. Hatuna la kuongeza zaidi ya ulivyothibisha wahyi kuwepo majini na kwamba wao walimtumikia Suleiman na akili hailikatai hilo. Kwa hiyo basi hakuna haja yoyote ya kuleta taawili na kuyazungusha maneno. Imam Ali (a.s.) amesema: "Lau kama mtu angeliweza la kumfanya adumu ulimwenguni au kuhepa mauti, basi angelikuwa Suleiman ambaye alitiishiwa ufalme, majini watu, utume na heshima kuu."

{وَأَيُّوبَ إِذْ نَادَىٰ رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ الضُّرُّ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ {83

***Na Ayyub aliopomlingania Mola wake: Hakika mimi imenigusa dhara, nawe ndiye unayerehemu zaidi kuliko wanaorehemu.***

{فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَكَشَفْنَا مَا بِهِ مِنْ ضُرٍّ ۚ وَآتَيْنَاهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُمْ مَعَهُمْ رَحْمَةً مِنْ عِنْدِنَا وَذِكْرَىٰ لِلْعَابِدِينَ {84

***Basi tukamkubalia na tukamuondolea dhara na tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao kuwa ni rehema itokayo kwetu na ukumbusho kwa wafanyao ibada.***

{وَإِسْمَاعِيلَ وَإِدْرِيسَ وَذَا الْكِفْلِ ۖ كُلٌّ مِنَ الصَّابِرِينَ {85

***Na Isamil na Idris na Dhulkifl, wote walikuwa miongoni mwa wanaosubiri.***

{وَأَدْخَلْنَاهُمْ فِي رَحْمَتِنَا ۖ إِنَّهُمْ مِنَ الصَّالِحِينَ {86

***Na tukawaingiza katika rehema yetu. Hakika wao ni katika watu wema.***

وَذَا النُّونِ إِذْ ذَهَبَ مُغَاضِبًا فَظَنَّ أَنْ لَنْ نَقْدِرَ عَلَيْهِ فَنَادَىٰ فِي الظُّلُمَاتِ أَنْ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ
{الظَّالِمِينَ {87

***Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhabika na akadhani kuwa hatutamdhikisha. Basi aliita katika giza kwamba: Hapana Mola isipokuwa wewe, umetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa madhalimu.***

{فَاسْتَجَبْنَا لَهُ وَنَجَّيْنَاهُ مِنَ الْغَمِّ ۚ وَكَذَٰلِكَ نُنْجِي الْمُؤْمِنِينَ {88

***Basi tukamkubalia na tukamwokoa kutokana na ghamu. Kama hivyo tunawaokoa wenye kuamini.***

{وَزَكَرِيَّا إِذْ نَادَىٰ رَبَّهُ رَبِّ لَا تَذَرْنِي فَرْدًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِينَ {89

***Na Zakaria alipomwita Mola wake: Ewe Mola wangu! Usiniwache peke yangu na wewe ndiye mbora wa wanaorithi.***

فَاسْتَجَبْنَا لَهُ وَوَهَبْنَا لَهُ يَحْيَىٰ وَأَصْلَحْنَا لَهُ زَوْجَهُ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا يُسَارِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ۖ وَكَانُوا
{لَنَا خَاشِعِينَ {90

***Basi tukamwitikia na tukampa Yahya na tukamponyeshea mkewe. Hakika wao walikuwa wepesi kufanya kheri na wakituomba kwa hofu na walikuwa wakitunyenyekea.***

{وَالَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهَا مِنْ رُوحِنَا وَجَعَلْنَاهَا وَابْنَهَا آيَةً لِلْعَالَمِينَ {91

***Na mwanamke aliyelinda tupu yake na tukampulizia katika roho yetu na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni ishara kwa walimwengu.***

1. Kama ilivyo katika baadhi ya hukumu kwenye Qur'an –Mtarjumu.
2. Pia waswahili wana msemo wakitaka kuusifia wimbo husema: "Wimbo uliomtoa nyoka pangoni" –Mtarjumu.

# Aya 83 – 91: Na Ayyub Aliopomlingania Mola Wake

## Maana

**Na Ayyub aliopomlingania Mola wake: Hakika mimi imenigusa dhara, nawe ndiye unayerehemu zaidi kuliko wanaorehemu. Basi tukamkubalia na tukamuondolea dhara.**

Makusudio ya dhara ni madhara ya nafsi, kama vile maradhi, kutokana na neno la kiarabu *dhurr*.

Likisomwa *dharr* ndio linakuwa na maana ya madhara ya kila kitu. Wafasiri na wapokezi wengi wamepokea riwaya nyingi zinazomuhusu Ayyub. Tunalolifahamu sisi, kutokana na Aya zinazomzungumzia kwa uwazi na kwa ishara hapa na pia katika Sura Swad (38), ni kwamba Ayyub alikuwa na afya yake nzuri akiwa hana matatizo yoyote. Kisha mabalaa yakaanza kumwandama kila upande, akawa ni wa kupigiwa mifano.

Masaibu yalimpata yeye mwenyewe binafsi; akavumilia uvumilivu wa kiungwana; na akabakia na yakini yake na kumtegemea kwake Mwenyezi Mungu. Huzuni wala machungu hayakumfanya aache kumtii Mwenyezi Mungu. Lakini muda ulivyomzidi na machungu nayo yakazidi, alimshtakia

Mwenyezi Mungu mambo yake kwa maneno mawili tu: "Imenigusa dhara, nawe ndiye unayerehemu zaidi kuliko wanaorehemu," na wala hakulalamika kwa kusema balaa gani hii iliyoniandama.

Ndipo Mwenyezi Mungu akamwitikia maombi yake na akamuondolea mabalaa na kumrudisha katika hali nzuri zaidi ya alivyokuwa.

**Na tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao kuwa ni rehema itokayo kwetu na ukumbusho**

**kwa wafanyao ibada.**

Mwenyezi Mungu alimruzuku watoto na wajukuu zaidi ya wale aliowakosa, ikiwa ni rehema na malipo ya uvumilivu wake; na pia kukumbusha kwamba mwenye kuwa na subra na uvumilivu kama wa Ayyub, basi mwisho wake utakuwa kama wa Ayyub. Mwenyezi Mungu amehusisha kuwataja wenye kuabudu kwa kuashiria kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na mwenye subra aliye na ikhlasi kwa kauli yake na vitendo vyake.

Huu ndio ujumla wa maelezo ya Aya zinazofungamana na Ayyub; bila ya kuingilia ufafanuzi walioutaja wapokezi na wasimulizi. Kwani huo hauam- batani na itikadi wala uhai kwa mbali wala karibu. Miongoni mwa njia za Qur'an ni kukitaja kisa kwa yale yaliyo na mazingatio yenye kunufaisha na mawaidha ya kukanya.

**Na Isamil Na Idris Na Dhulkifl, wote walikuwa miongoni mwa wanao- subiri. Na tukawaingiza katika rehema yetu. Hakika wao ni katika watu wema.**

Ismail alifanya subra ya kukubali kuchinjwa na akawa na uvumilivu wa kukaa katika nchi isiyokuwa na mimea wala kinywewa. Idris tumemueleza katika Juz. 16 (19:56).

Ama Dhulkifl wengi wamesema alikuwa Mtume; na baadhi wakasema alikuwa ni mja mwema tu na sio Mtume. Sisi tunaamini kwamba yeye ni miongoni mwa waliokuwa na subira na waja wema, kwa kufuata Qur'an ilivyosema, na wala hatutaulizwa zaidi ya hayo.

**Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhabika na akadhani kuwa hatutamdhikisha. Basi aliita katika giza kwamba: Hapana Mola isipokuwa wewe, umetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa madhalimu.**

Dhun-Nun ni Yunus. Maana ya neno '*Nun*" ni samaki. Mwenyezi Mungu anasema:

{فَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تَكُنْ كَصَاحِبِ الْحُوتِ{48

***"Na vumilia hukumu ya Mola wako wala usiwe kama sahibu wa samaki" (68:48).***

Hali ameghadhibika ni kuwaghadhibikia watu wake. Neno kudhikishwa limefasiriwa kutokana na neno *Naqdira alyh*; kama lilivyotumika mahali pengine:

{وَمَنْ قُدِرَ عَلَيْهِ رِزْقُهُ{7

***"Na yule ambaye imekuwa dhiki riziki yake" (65:7).***

Makusudio ya katika giza hapa ni ndani ya tumbo la samaki.

Maana kwa ujumla ni: kumbuka ewe Muhammad habari ya Yunus alipowalingania watu wake, lakini hawakumwitikia mwito wake, akawaondokea kwa kuwakasirikia, akadhani kuwa hatutamdhikisha kwa kumzuia n.k. Alipomezwa na samaki akataka uokovu kutoka kwetu, **basi tukamkubalia na tukamwokoa kutokana na ghamu. Kama hivyo tunawaokoa wenye kuamini.**

Makusudio ya ghamu hapa ni tumbo la samaki; na kuokoka, ni kutolewa humo hadi kwenye nchi kavu. Umetangulia mfano wake katika Juz. 11 (10:98).

**Na Zakaria alipomwita Mola wake: Ewe Mola wangu! Usiniwache peke yangu na wewe ndiye mbora wa wanaorithi. Basi tukamwitikia na tukampa Yahya na tukamponyeshea mkewe.**

Umetangulia mfano wake katika Juz. 3 ( 3: 38) na Juz. 16 (19:7).

**Hakika wao walikuwa wepesi kufanya kheri na wakituomba kwa hofu na walikuwa wakitunyenyekea.**

Wao ni Zakariya, mkewe na Yahya au wale Mitume waliotangulia kutajwa. Wote walifanya kheri kwa kutaka thawabu za Mwenyezi Mungu na kuhofia adhabu yake na walikuwa wakimfuata Mwenyezi Mungu katika kila jambo.

**Na mwanamke aliyelinda tupu yake na tukampulizia katika roho yetu na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni ishara kwa walimwengu.**
Umetangulia mfano wake katika Juz. 3 (3: 45) na Juz. 16 (19: 16).

{إِنَّ هَٰذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ {92

***Hakika umma wenu huu ni umma mmoja, na mimi ni Mola wenu kwa hivyo niabuduni.***

{وَتَقَطَّعُوا أَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ ۖ كُلٌّ إِلَيْنَا رَاجِعُونَ {93

***Na wakalivunja jambo lao baina yao. Wote watarejea kwetu.***

{فَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا كُفْرَانَ لِسَعْيِهِ وَإِنَّا لَهُ كَاتِبُونَ {94

***Na atendaye mema naye ni mumin, basi haitakataliwa bidii yake na hakika sisi tutamwandikia.***

{وَحَرَامٌ عَلَىٰ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا أَنَّهُمْ لَا يَرْجِعُونَ {95

***Na ni haramu kwa mji tuliouangamiza kwamba wao hawatarejea.***

96{حَتَّىٰ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُمْ مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ}

***Mpaka watakapofunguliwa Juju na Majuju, wakawa wanateremka kutoka kila mlima.***

97{وَاقْتَرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ فَإِذَا هِيَ شَاخِصَةٌ أَبْصَارُ الَّذِينَ كَفَرُوا يَا وَيْلَنَا قَدْ كُنَّا فِي غَفْلَةٍ مِنْ هَٰذَا بَلْ كُنَّا ظَالِمِينَ}

***Na miadi ya haki itakaribia, ndipo yatakapokodoka macho ya wale waliokufuru. Ole wetu! Hakika tulikuwa tumeghafilika na haya, bali tulikuwa ni wenye kudhulumu.***

98{إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ أَنْتُمْ لَهَا وَارِدُونَ}

***Hakika nyinyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannam, mtaifikia.***

99{لَوْ كَانَ هَٰؤُلَاءِ آلِهَةً مَا وَرَدُوهَا ۖ وَكُلٌّ فِيهَا خَالِدُونَ}

***Lau haya yangelikuwa ni miungu yasingeliingia na wote watadumu humo.***

100{لَهُمْ فِيهَا زَفِيرٌ وَهُمْ فِيهَا لَا يَسْمَعُونَ}

***Lao humo ni kupiga mayowe na wala hawatasikika.***

# Aya 92 – 100: Umma Mmoja

## Maana

**Hakika umma wenu huu ni umma mmoja, na mimi ni Mola wenu kwa hiyo niabuduni.**

## Lugha

Maana ya neno umma ni watu wenye lugha moja na historia moja. Kisha neno hili likawa linatumika zaidi kwa maana ya dini na mila. Maana haya ndiyo yaliyokusudiwa hapa.

Umma wenu huu ni itikadi ya mitume ambayo ni tawhid pamoja na kufuata amri za Mwenyezi Mungu kwa kauli na vitendo. Msemo ‘wenu’ unaelekezwa kwa watu wote.

Maana ni kuwa enyi watu wote! Shikeni dini ya Tawhidi waliyokuwa nayo Mitume na mumwabudu Mungu mmoja aliye peke na mumfanyie ikhlasi katika kauli na vitendo.

**Na wakalivunja jambo lao baina yao.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliwaamrisha wote wawe kwenye itikadi ya tawhidi, lakini wakagawanyika wakawa makundi ya wakana Mungu na washirikina. Hata wale wafuasi wa Mitume nao wanatukanana na kujitenga na wengine; bali hata wafuasi wa Mtume mmoja nao ni hivyo hivyo.

**Wote watarejea kwetu.**

Haya ni makemeo na hadhari kwa wale wanaofarikiana wakawa vikundi.

**Na atendaye mema naye ni mumin, basi haitakataliwa bidii yake na hakika sisi tutamwandikia.**

Imani pamoja na matendo mema ni njia ya Peponi na imani bila ya matendo haifai chochote. Hiyo ni kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِنْ قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيمَانِهَا خَيْرًا ۗ {158

***“Basi mtu haitamfaa imani yake ambaye hakuamini zamani, au hakuchuma kheri kwa imani yake.” Juz. 8*** **(*6:158*).**

Ama matendo mema bila ya imani, humnufaisha mtendaji kwa namna moja au nyingine na huenda ikamfaa huko Akhera kwa kupunguziwa adhabu. Tumeyafafanua hayo katika Juz. 4 (3:158) kwenye kifungu ‘kafiri na amali njema’ Pia Umepita mfano wake katika Juz. 14 (16: 97)

**Na ni haramu kwa mji tuliouangamiza kwamba wao hawatarejea.**

Aya hii ni jawabu la swali la kukadiria, kwamba je, washirikina katika watu wa kijiji kilichoangamizwa na Mwenyezi Mungu kwa kufuru yao, watarudishwa tena kuwa hai na kuadhibiwa huko Akhera, kama walivyoadhibiwa duniani?

Ndio akajibu Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kuwa watu wote, kesho watarejea kwa Mwenyezi Mungu; hata wale walioangamizwa duniani kwa dhambi zao na ni muhali kukosa kurejea kwa Mwenyezi Mungu baada ya mauti; bali hakuna budi lazima watafufuliwa.

Swali la pili, je inafaa kuadhibiwa akhera baada ya kuadhibiwa duniani? Huko si ni kuadhibu mara mbili kwa kosa moja?

Jibu: Hapana! Kuadhibiwa kwao duniani kulikuwa ni kwa ajili ya kuwakadhibisha kwao Mitume waliowajia na miujuza; kama zinavyofahamisha Aya hizi zifuatazo na nyinginginezo mfano wake:

{وَقَوْمَ نُوحٍ لَمَّا كَذَّبُوا الرُّسُلَ أَغْرَقْنَاهُمْ {37

*“Na kaumu ya Nuh walipowakadhibisha Mitume tuliwagharikisha”* (*25:37*)

{كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَأَصْحَابُ الرَّسِّ وَثَمُودُ {12

{وَعَادٌ وَفِرْعَوْنُ وَإِخْوَانُ لُوطٍ {13

{وَأَصْحَابُ الْأَيْكَةِ وَقَوْمُ تُبَّعٍ ۚ كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ وَعِيدِ {14

***“Kabla yao walikadhibisha kamu ya Nuh na watu wa Rassi na Thamud na A’d na Firauni na ndugu wa Lut na watu wa vichakani na kaumu ya Tubbai, wote waliwakadhibisha Mitume, kwa hiyo kiaga kikathibitika juu yao.”*** **(*50: 12-14*).**

Ama adhabu ya Akhera ni ya ukafiri wenyewe na madhambi mengineyo; kama dhulm**a n.k.**
Kwa hiyo adhabu zinakuwa nyingi kutokana na dhambi kuwa aina nyingi, sio kwa dhambi moja.

**Mpaka watakapofunguliwa Juju na Majuju, wakawa wanateremka kutoka kila mlima.**

Katika Juz. 16 (18: 94) tuliwanukuu baadhi ya wafasiri wakisema kuwa Juju ni wa Tatars na Majuju ni Wamongoli. Vile vile tumesema huko kuwa ukuta wa Juju na Majuju hauko tena. Kwa hiyo basi makusudio ya kufunguliwa Juju na Majuju ni kuenea kwao katika mabara.

Vyovyote iwavyo sisi hatujawahi kusoma ya kutegemewa kuhusu Juju na Majuju, si katika tafsiri wala mahali penginepo. Kwa hiyo tutasimama kwenye dhahiri ya nukuu ya Qur’an tu na ufafanuzi tutawachia wengine.

**Na miadi ya haki itakaribia, ndipo yatakapokodoka macho ya wale waliokufuru.**

Makusudio ya miadi ya haki hapa ni Kiyama, hapo akili za waliokufuru zitapotea na macho yatatoka kutokana na vituko vya siku hiyo. Umetangulia mfano wake katika Juz. 13 (14: 42).

**Ole wetu! Hakika tulikuwa tumeghafilika na haya, bali tulikuwa wenye kudhulumu.**

Yaani watasema hivyo. Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 (7:5) na katika juzuu na Sura hii tuliyo nayo Aya 14 na 46.

**Hakika nyinyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannam, mtaifikia.**

Hapa wanaambiwa washirikina wa Makka. Makusudio ya mnayoyaabudu ni masanamu yao. Maana ni

kuwa, enyi washirikina! Nyinyi na masanamu yenu mtakutana kwenye Jahannamu kesho. Kuna Hadithi isemayo: “Mtu yuko pamoja na anayempenda.”

Unaweza kuuliza: Kuna faida gani ya kutiwa masanamu kwenye Jahannamu na ni mawe yasiyokuwa na utambuzi wala hisiya?

Wafasiri wamejibu kuwa lengo ni kuwazidishia masikitiko wale wanaoyaabudu, kila watakapoyaona karibu nao. Lakini jawabu hili ni kiasi cha kuchukulia uzuri na hisia tu. Lilio bora ni kuicha Aya nyingine ijibu:

{فَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ ۖ {24

***“Basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, uliowekewa makafiri.” Juz. 1*** **(*2:24*).**

Kuna riwaya isemayo kuwa Ibn Az-Zab'ariy – mmoja wa washirkina wa kikuraishi na mshairi wao – aliingilia Aya hii kama mayahudi wanamwabudu Uzayr na wanaswara (wakristo) wanamwabudu Masihi na hawa wawili ni watu wa Peponi, kama anavyosema Muhammad, sasa vipi aseme kila kinachoabudiwa ni kuni?

Mtume akamjibu: Ni ujinga ulioje wako wewe kutojua lugha ya watu wako. Kwani huoni herufi *ma* (ambayo) ni ya visivyo na akili?

Zaidi ya hayo maneno yanawahusu washirikina wa kikurashi, kama tulivyotangulia kusema nao wanaabudu masanamu.

**Lau haya yangelikuwa ni miungu yasingeliingia na wote watadumu humo.**

Haya ni ishara ya masanamu. Maana ya Aya yako wazi, kwamba lau masanamu yangelikuwa miungu yasingeliiingia motoni. Ni kama kusema: Lau ungelikuwa mwaminifu usingelifanya khiyana, lakini umefanya khiyana kwahiyo wewe si mwaminifu. Mfano huu katika mantiki unaitwa kutoa dalili kwa kipimo cha kuvua (*istithnaiyy*).

**Lao humo ni kupiga mayowe na wala hawatasikika.**

Hapa anaambiwa kila mkosaji, awe mwislamu au kafiri. Humo ni humo ndani ya Jahannam. Maana ni kuwa kila mkosaji atakuwa katika Jahannam akilalama kwa machungu; hatasikia neno la upole wala huruma, bali atakayemuona atamtahayariza na kumsema:

{وَقِيلَ لِلظَّالِمِينَ ذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ {24

***“Na wenye kudhulumu wataambiwa onjeni yale mliyokuwa mkiyachuma.”*** **(*39:24*).**

{إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ أُولَٰئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُونَ} 101

***Hakika wale ambao umewatangulia wema kutoka kwetu, hao watatenganishwa na hayo.***

{لَا يَسْمَعُونَ حَسِيسَهَا ۖ وَهُمْ فِي مَا اشْتَهَتْ أَنْفُسُهُمْ خَالِدُونَ} 102

***Hawatasikia mvumo wake. Nao watudumu katika yale ambayo nafsi zao zinayatamani.***

{لَا يَحْزُنُهُمُ الْفَزَعُ الْأَكْبَرُ وَتَتَلَقَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ هَٰذَا يَوْمُكُمُ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ} 103

***Hiyo fazaa kubwa haitawahuzunisha. Na Malaika watawapokea: Hii ndiyo siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa.***

{يَوْمَ نَطْوِي السَّمَاءَ كَطَيِّ السِّجِلِّ لِلْكُتُبِ ۚ كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُعِيدُهُ ۚ وَعْدًا عَلَيْنَا ۚ إِنَّا كُنَّا فَاعِلِينَ} 104

***Siku tutakapozikunja mbingu mkunjo wa karatasi za vitabu. Kama tulivyoanza umbo la mwanzo tutalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu yetu. Hakika sisi ni wenye kufanya.***

{وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ} 105

***Na hakika tulikwishaandika katika Zaburi baada ya ukumbusho kuwa Ardhi watairithi waja wangu walio wema.***

{إِنَّ فِي هَٰذَا لَبَلَاغًا لِقَوْمٍ عَابِدِينَ} 106

***Hakika katika haya kuna ujumbe kwa wafanyao ibada.***

{وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ} 107

***Na hatukukutuma ila uwe ni rehema kwa walimwengu.***

# Aya 101 – 107: Ardhi Watarithi Waja Wangu Walio Wema

## Maana

**Hakika wale ambao umewatangulia wema kutoka kwetu, hao watatenganishwa na hayo.**

Mwenyezi Mungu aliwaahidi wenye takua kuamiliana nao kwa wema. Miongoni mwa wema huo ni kuokoka na moto.

**Hawatasikia mvumo wake.**

Hii ni kusisitiza watakavyokuwa mbali nao.

**Nao watudumu katika yale ambayo nafsi zao zinayatamani.**
Watasalimika na adhabu ya Mwenyezi Mungu wakineemeshwa kwenye Pepo yake.

**Hiyo fazaa kubwa haitawahuzunisha, sikwambii ndogo tena.**

Kwani fazaa zina daraja, kuanzia machungu ya kukata roho, upweke wa kaburini, kisha kutoka makaburini kwa ajili ya hisabu hadi kuingia Jahannam.

**Na Malaika watawapokea: Hii ndiyo siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa.**

Malaika watawapokea kwa takrima na kuwaambia kuwa Mwenyezi Mungu amewakusanya kwenye siku hii aliyowaahidi kwa ufalme wa daima na neema isiyokatika. Aya hizi tatu zinafupilizwa na neno:

{هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَانِ إِلَّا الْإِحْسَانُ} 60

***"Je, malipo ya hisani si ni hisani tu."*** (***55:60***)

Au neno:

{لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۖ} 26

***"Kwa wafanyao wema ni wema." Juz.11*** (***10:26***).

**Siku tutakapozikunja mbingu mkunjo wa karatasi za vitabu.**

Makusudio ya vitabu hapa ni maandishi ya matamko yanayoayaandikwa kwenye karatasi. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) atazikunja sayari, siku ya Kiyama, pamoja na ukubwa na wingi wake; kama inavyokunjwa karatasi yenye maandishi; kiasi ambacho kila sayari itafanana na herufi au neno lilo kwenye karatasi.

**Kama tulivyoanza umbo la mwanzo tutalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu yetu. Hakika sisi ni wenye kufanya.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amefananisha ufufuo na kuumba kwa kwanza; kwamba, kama kulivyowezekana kwa kwanza, basi kwa pili pia kuunawezekana. Si muhali kwa Mwenyezi Mungu kutekeleza ahadi yake.

Hilo halimshindi Mwenyezi Mungu; kwani mwenye kuumba ulimwengu basi hawezi kushindwa kuurudisha tena baada ya kuharibika na kutawanyika:

{وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ۚ}27

***"Na Yeye ndiye anayeanzisha uumbaji, kisha ataurudisha. Na hilo ni jepesi zaidi kwake" (30:27).***

## Tena Mahdi Anayengojewa

**Na hakika tulikwishaandika katika Zaburi baada ya ukumbusho kuwa Ardhi watairithi waja wangu walio wema.**

Zaburi ni kitabu cha Daud na ukumbusho ni vitabu vya mbinguni vilivyotangulia; kama vile vitabu vya Ibrahim na Musa. Maana yake ni kuwa utawala wa dunia, ingawaje hivi sasa uko mikononi mwa mataghuti waovu, lakini Mwenyezi Mungu atauhamisha uende kwa walio wema. Hilo halina budi. Hapo amani na uadilifu utaenea ardhini na watu wote wataneemeka na kheri za Ardhi na baraka zake.

Kuna Hadithi nyingi zenye maana ya Aya hii; miongoni mwazo ni ile aliy- oipokea Abu Daud katika Kitabu cha Sunan, ambacho ni mojawapo ya Sahihi sita: "Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu:

Lau haitabakia katika dunia isipokuwa siku moja tu, basi Mwenyezi Mungu angeliirefusha siku hiyo mpaka amtume mtu kutoka katika watu wa nyumba yangu (Ahlu bayt) jina lake linafanana na jina langu, na jina la baba yake ni kama la baba yangu, ataijaza ardhi uadilifu baada ya kujazwa dhulma na jeuri"[1]

Kanuni ya maisha hailikatai hilo, bali inalithibitisha na kulisisitiza. Ikiwa nguvu hivi sasa ziko mikononi mwa unyama wenye kudhuru wa umoja wa mataifa, baraza la usalama n.k. basi hakuna litakalozuia, siku moja kugeuka nguvu hiyo kutoka mikononi mwa madhalimu waovu hadi kwa watu wa haki na uadilifu; bali maumbile yanapenda kujikomboa na dhulma.

Pia kuna misingi isemayo: “Kila kilicho katika ardhi kina harakati, kama ilivyo na harakati ardhi na kwamba kudumu hali ni muhali.” Yote hayo yanapelekea kuwa hatimaye nguvu zitakuwa mikononi mwa wema wanao- faa.

**Hakika katika haya kuna ujumbe kwa wafanyao ibada.**

Haya ni haya ya kuwa ardhi itarithiwa na waja wema; hata kama ni baada ya muda. Makusudio ya wafanyao ibada hapa ni wale wanaopata mawaidha kwa kuzingatia na kunufaika na maonyo.

**Na hatukukutuma ila uwe ni rehema kwa walimwengu.**

Maneno yanaelekezwa kwa Muhammad (s.a.w.). Risala yake ni rehema kwa wa mwanzo na wa mwisho. Huko nyuma tumeeleza mara nyingi kuhusu misingi ya risala hiyo na mafunzo yake.

Inatosha, kuthibitisha hilo, kauli za mwenye risala hiyo; kama vile: “Hakumwamini Mwenyezi Mungu yule ambaye watu hawamwamini. Likikuhuzunisha ovu na likakufurahisha jema, basi wewe ni mumin.”

Ni kwa hisia hizi ndio uadilifu utasimama, amani kuenea na maisha kuwa bora. Tumezungumzia kwa ufafanuzi kuhusu hilo katika Juz. 7 (6:92).

{قُلْ إِنَّمَا يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۖ فَهَلْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ {108

***Sema: Hakika umeletwa wahyi kwangu ya kwamba hakika Mungu wenu ni Mungu mmoja tu. Je nyinyi mmesilimu?***

{فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُلْ آذَنْتُكُمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ ۖ وَإِنْ أَدْرِي أَقَرِيبٌ أَمْ بَعِيدٌ مَا تُوعَدُونَ {109

***Kama wakikataa, basi sema: Nimewatangazia sawasawa. Wala sijui yako karibu au mbali hayo mliyoahidiwa.***

{إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ مِنَ الْقَوْلِ وَيَعْلَمُ مَا تَكْتُمُونَ {110

***Hakika Yeye anajua kauli ya dhahiri na anajua mnayoyaficha.***

{وَإِنْ أَدْرِي لَعَلَّهُ فِتْنَةٌ لَكُمْ وَمَتَاعٌ إِلَىٰ حِينٍ {111

***Wala sijui pengine huu ni mtihani tu kwenu na starehe mpaka muda kidogo.***

{قَالَ رَبِّ احْكُمْ بِالْحَقِّ ۗ وَرَبُّنَا الرَّحْمَٰنُ الْمُسْتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ 112}

***Akasema: Mola wangu! Hukumu kwa haki. Na Mola wetu ni Mwingi wa rehema aombwaye msaada juu ya mnayoyasifia.***

1. Tumezungumzia kuhusu Mahdi anayengojewa katika Juz. 1( 2:127 - 129) na Juz. 15 (17: 58)

# Aya 108 – 112: Hakika Mungu Wenu Ni Mmoja Tu

## Maana

**Sema: Hakika umeletwa wahyi kwangu ya kwamba hakika Mungu wenu ni Mungu mmoja tu. Je nyinyi mmesilimu?**

Mwenyezi Mungu alimwarisha Mtume wake awaambie washirikina kuwa Mwenyezi Mungu ameniletea wahyi kwamba Yeye ni mmoja tu hana mshirika katika kuumba kwake na wala katika ujuzi wake.

Ulimwengu huu na maajabu yake na kanuni zake unashuhudia kwa uwazi juu ya umoja, uweza na ukuu wake Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Basi kwa nini hamuamini na kufuata amri yake? Kwanini mnadanganyika kuacha kumwabudu Yeye na kwenda kuabudu mawe yasiyodhuru wala kunufaisha?

**Kama wakikataa, basi sema: Nimewatangazia sawasawa.**

Baada ya kuwalazimu hoja ya kufikisha na maonyo, Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume wake mtukufu awaambie kuwa nimekishatekeleza wajibu wangu na nikafikisha risala ya Mola wangu. Kwa hiyo haukubaki udhuru wowote kwenu.

**Wala sijui yako karibu au mbali hayo mliyoahidiwa.**

Mimi nina yakini na adhabu yenu, kwa sababu Mwenyezi Mungu ameiahadi na kuwahadhirisha nayo, na ahadi yake Mwenyezi Mungu ni ya kweli na adhabu yake pia ni kali zaidi, lakini sijui itakuwa lini. Ni sawa iwe karibu au mbali, lakini ina wakati wake. Ngojeni nami niko pamoja nanyi katika wenye kungojea.

**Hakika Yeye anajua kauli ya dhahiri na anajua mnayoyaficha.**

Umetangulia mfano wake katika Juz. 16 (20:7).

**Wala sijui pengine huu ni mtihani tu kwenu na starehe mpaka muda kidogo.**

Sijui kuna hekima gani ya kupewa kwenu muda na kucheleweshewa adhabu. Je Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ametaka kumdhirisha kila mmoja hakika yake, aweze kutubia mwema na aendelee mouvu au ametaka mustarehe siku zilizobakia kwenye umri wenu? Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye.

**Akasema (Muhammad): Mola wangu! Hukumu kwa haki.**

Yaani idhihirishe haki na uwanusuru watu wake kwa wale wanaoipinga.

**Na Mola wetu ni Mwingi wa rehema aombwaye msaada juu ya mnayoyasema kuwa masanamu yenu ni miungu na madai yenu kwangu kuwa ni mzushi.**

“Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wewe ni mtukufu kwa kila anayekuzulia. Wema ni wa yule anayekufuata, akachukua athari yako na akamwambia mzushi, kama vile ulivyosema wewe:

**Na Mola wetu ni Mwingi wa rehema aombwaye msaada juu ya mnayoyasifia.**”

# Sura Ya Ishirini Na Mbili: Al-Hajj

Baadhi ya Aya zake zimeshuka Makka na nyingine Madina. Ina Aya 78.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.***

{يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمْ ۚ إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ {1

***Enyi watu! Mcheni Mola wenu. Hakika tetemeko la saa ni jambo kuu.***

{يَوْمَ تَرَوْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّا أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ سُكَارَىٰ وَمَا هُمْ بِسُكَارَىٰ
وَلَٰكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ {2

***Siku mtakapoiona, kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshae na kila mwenye mimba ataiharibu mimba yake. Na utawaona watu wamelewa, na kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali.***

{وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّبِعُ كُلَّ شَيْطَانٍ مَرِيدٍ {3

*Na miongoni mwa watu kuna anayejadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya elimu na anamfuata kila shetani muasi.*

{كُتِبَ عَلَيْهِ أَنَّهُ مَنْ تَوَلَّاهُ فَأَنَّهُ يُضِلُّهُ وَيَهْدِيهِ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ} 4

***Ameandikiwa kwamba anayemtawalisha shetani, basi huyo hakika atampoteza na atamwongoza katika adhabu ya moto mkali.***

{يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِنَ الْبَعْثِ فَإِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ مِنْ مُضْغَةٍ مُخَلَّقَةٍ وَغَيْرِ مُخَلَّقَةٍ لِنُبَيِّنَ لَكُمْ ۚ وَنُقِرُّ فِي الْأَرْحَامِ مَا نَشَاءُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُسَمًّى ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِتَبْلُغُوا أَشُدَّكُمْ ۖ وَمِنْكُمْ مَنْ يُتَوَفَّىٰ وَمِنْكُمْ مَنْ يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِنْ بَعْدِ عِلْمٍ شَيْئًا ۚ وَتَرَى الْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ وَأَنْبَتَتْ مِنْ كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ} 5

***Enyi watu! Ikiwa mna shaka ya kufufuliwa, basi kwa hakika tuliwaumba kutokana na udongo kisha kutokana na tone kisha kutokana na pande la damu kisha kutokana na pande la nyama lenye umbo na lisilokuwa na umbo. Ili tuwabainishie. Na tunaliweka katika matumbo ya kizazi mpaka muda uliowekwa. Kisha tunawatoa hali ya kuwa mtoto mchanga kisha mfikie kukomaa kwenu. Na wapo miongoni mwenu wanaokufa na wapo miongoni mwenu wanorudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa hata asijue kitu baada ya kuwa anakijua. Na unaiona ardhi imekufa, lakini tunapoyateremsha maji juu yake, husisimka na kututumka na kumea kila aina ya mimea mizuri.***

{ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّهُ يُحْيِي الْمَوْتَىٰ وَأَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ} 6

***Hayo ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu ni haki na kwamba hakika yeye ndiye Mwenye kuhuisha wafu na kwamba hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.***

{وَأَنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ لَا رَيْبَ فِيهَا وَأَنَّ اللَّهَ يَبْعَثُ مَنْ فِي الْقُبُورِ} 7 Na kwamba saa itakuja hapana sha

***ka kwa hilo, na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini.***

# Aya 1 – 7: Ufufuo

## Maana

Katika Aya hizi kuna kutahadharisha kuhusu siku ya Kiyama pamoja na kuashiria vitu na shida za siku hiyo. Vile vile kuwashutumu wale walioghafilika nacho; kisha kutoa dalili ya ufufuo.
Ufafanuzi ni kama ufuatavyo:

**1. Enyi watu! Mcheni Mola wenu. Hakika tetemeko la saa ni jambo kuu.**

Makusudio ya saa ni siku ya Kiyama. Kimeitwa hivyo kwa sababu kila mtu atakifikia; kama anavyosema Mulla Sadra katika kitabu *Al–Asfar*.

Maana ya tetemeko la kiyama ni kuharibika ulimwengu ikiwa ni pamoa na ardhi yake na mbingu yake. Hizo zitachanganyika na pia bara na bahari na vizuizi vitaondoka. Miili itatoka makakburini kama picha isiyo na roho.

**Siku mtakapoiona, kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshae na kila mwenye mimba ataiharibu mimba yake. Na utawaona watu wamelewa, na kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali.**

Hiki ni kinaya cha vituko vya siku ya Kiyama na shida zake; ambapo hakutakuwa na mnyonyeshaji wala mwenye mimba sku hiyo. Yaani, lau angelikuwako mwenye kunyonyesha basi angelimsau mwanawe na mwenye mimba angelizaa. Na watu wote watagongana huku na huko kama walevi.

## Mjadala Wakijinga Na Upotevu

**2. Na miongoni mwa watu wako wanaojadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya elimu.**

Mtu yeyote atakuwa ni mmoja wapo kati ya wawili: Ama atakuwa hajui au atakuwa ni mjuzi. Huyo mjuzi naye yuko katika hali mbili: Ama atakuwa ni mwenye insafu au atakuwa mpotevu. Mwenye insafu ni yule anayesema yale anayoyajua na kuyanyamazia asiyoyajua. Mwenyezi Mungu ameueleza wadhifa wa asiyejua kwa kusema:

{فَاسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ {7

***"Basi waulizeni wenye kumbukumbu, ikiwa nyinyi hamjui."* (*21:7*).**

Ikiwa atauepuka wadhifa huu, basi atakuwa amehusika na kauli ya Imam Ali (a.s.): "Yu mjinga, anatangatanga gizani bila ya mwongozo."

Huu ndio ujinga alioukusudia Mwenyezi Mungu kwenye kauli yake hii na pia kauli itakayokuja kwenye Aya ya 8 ya Sura hii: "Na katika watu wapo wanaojadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ilmu wala

uongufu wala Kitabu chenye nuru.”

Hajui njia ya kumjua Mwenyezi Mungu, lakini anabishana kuhusu Mungu, huku akisema: lau Mwenyezi Mungu angelikuwako tungelimuona. Kwa mantiki haya, anataka kufasiri mada kwa isiyokuwa mada, kuona kwa macho kile kinachonekana kwa akili tu na kumgusa kwa mkono muumba wa mbingu na ardhi.

Huyu hana tofauti na yule anayetaka kufanya mtihani wa nadhariya ya ‘ushahidi ni wa mwenye kudai na kiapo ni kwa mwenye kukanusha’ kwenye kiwanda. Au kutaka kufanya mtihani wa kuendesha gari kutokana na hisia zake.

Wakati nikiandika maelezo haya nimekumbuka tulipokua Najaf tukisoma, kiasi cha miaka arobaini iliyopita. Siku moja tulipokuwa kwenye darasa tukisiliza mhadhara wa mwalimu, mmoja wa wanafunzi akamkatiza mwalimu na akatoa ushahidi usiokuwa na uhusiano wowote na maudhui kwa umbali wala karibu. Basi mwalimu akaachana naye akawaangalia wanafunzi wengine na akasema:

“Hapo zamani kulikuwa na mtu mmoja mwenye akili punguani, jina lake ni Bau. Siku moja alipita barabarani akaona watu wamekusanyika. Akauliza, kulikoni? Akaambiwa fulani ameanguka kutoka juu ya nyumba, amaevunjikavunjika viungo hatujui kama ataishi na watu wake hawana la kufanya.
Basi Bau akasema: “Mimi nina suluhisho, mfungeni kamba mumkaze sawasawa kisha avutwe mpaka juu ya nyumba kule alikotokea, atapona tu.” Watu walipomcheka, alitoa hoja kwamba mwaka jana fulani alianguka kisimani, wakamfunga kamba na wakamtoa, akasalimika.”

Mantiki haya hasa ndiyo ya yule anayekana kuweko Mungu kwa vile hamuoni. Ulimwengu huu na nidhamu yake anauona, lakini bado anadai kuwa haufahamishi kuwako aliyeutengeneza na kuuwekea nidhamu.

Sisi tunaamini ushahidi na majaribio, lakini tunaamini vilievile kuwa majaribio haya hayawezi kuwa kwenye kila kitu, bali yanakuwa kwenye baadhi ya vitu vya kimaada. Ama vitu vya kiroho na vya kibinadamu vina njia nyingine ya kujua.

Tunasema hivi tukiwa na uhakika kwamba hivi viwili vinakwenda pamoja vikikamilishana na kwamba mtu anahitajia maada. Misimamo kama vile haki na kheri haina budi iwe na athari inayoonekana, vinginevyo ingelikuwa ni matamshi tu yasiyokuwa na maana yoyote.

Lakini hii haimaanishi kuwa ndio njia ya maarifa peke yake; bali inatofautiana kwa kutofautiana vitu. Kwa hiyo ushahidi na majaribio ni sababu ya kujua vitu vya kimaada na akili ni sababu ya kujua vinginevyo visivyokuwa maada.

Tumezungumzia kuhusu maarifa na sababu zake katika Juz. 1(2:3–5)

Kwa ufupi ni kuwa mwenye kusema: Simwamini Mungu mpaka nimuone, amekiri yeye mwenyewe kwamba hataki kumwamini Mwenyezi Mungu, hata kama ataletewa dalili elfu na moja. Maana yake ni

kuwa anakubali kuwa yeye ni mjinga mwenye kiburi.

Kwa sababu Mwenyezi Mungu hawezi kuonekana kwa macho na kwamba njia ya kujua haikomei kwenye macho tu. Mwenyezi Mungu anamtaka binadamu afanye utafiti, uchunguzi, mjadala na mdahalo, lakini kielimu na kuchunga haki, sio kiujinga na kiupofu.

**Na anamfuata kila shetani muasi**.

Kila anayeweza kuvunga na kuficha hakika yake, basi huyo ni shetani. Shetani asi ni yule ambaye vitendo vyake na kauli zake zote zimejaa ufisadi. Shetani huyu akiingia kwenye akili ya mtu tu humuongoza kwenye upotevu na maangamizi. Hii ndio maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu:

**Ameandikiwa kwamba anayemtawalisha shetani, basi huyo hakika atampoteza na atamwongoza katika adhabu ya moto mkali**.

Upotevu na adhabu ya moto hawezi kuepukana nayo yule mwenye kufuata wapotevu na wafisadi, ambao wanayapotoa maneno ya Mwenyezi Mungu, wakihalalisha na kuharamisha kwa hawa zao na matakwa yao.

**3 Enyi watu ikiwa mna shaka ya kufufuliwa, basi kwa hakika tuliwaumba kutokana na udongo**.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kumhadharisha yule anayebishana kuhusu Mwenyezi Mungu bila ya elimu, sasa anataja dalili za ufufuo ambao mjinga anauifikiria kuwa hauwezekani.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amezileta dalili hizi kwa mifano yenye kuhisiwa, nayo ni kuwa: Hakika Mwenyezi Mungu amemuumba mtu kutokana na mchanga moja kwa moja, au kupitia kitu kingine.

Alimuumba Adam, baba wa watu, moja kwa moja kutokana na mchanga na akatuumba sisi wana wa Adam kupitia kitu kingine. Kila mmoja wenu anakuwa kutokana na manii na damu navyo vinatokana na chakula ambacho kinatokana na mchanga na maji. Kwa hiyo mchanga ndio msingi wa kupatikana mtu, **kisha kutokana na tone** la manii; kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

{أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِنْ مَنِيٍّ يُمْنَىٰ {37

***"Je, hakuwa ni tone la manii lililoshushwa?"* (*75:37*)**.

**Kisha kutokana na pande la damu**. Tone la manii linageuka kuwa kipande cha damu iliyoganda, **kisha kutokana na pande la nyama**. Pande la damu nalo linabadilika kuwa pande la nyama **lenye umbo na lisilokuwa na umbo**. Yaani baadhi yake imetimia umbo na sehemu haijatimia. **Ili tuwabainishie** uwezo wetu wa kufufua na mengineyo.

**Na tunaliweka katika matumbo ya kizazi mpaka muda uliowekwa** wa kuzaliwa mtoto.

**Kisha tunawatoa hali ya kuwa mtoto mchanga kisha mfikie kukomaa kwenu**. Kukomaa ni kukamilika mtu nguvu za kimwili na kiakili.

**Na wapo miongoni mwenu wanaokufa** kabla ya kukomaa au baada ya kukomaa kabla ya uzee na umri mbaya.

**Na wapo miongoni mwenu wanorudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa hata asijue kitu baada ya kuwa anakijua**.

Ni uzee na ukongwe, udhaifu wa kimwili, kiakili na kumbukumbu. Inapodhoofika akili matamanio yanachukua nafasi na kuzidi kufanya mambo ya kipuuzi.

Mabadiliko haya ya kukua kwa binadamu, kutoka hali duni hadi hali ya juu; kutoka mchanga hadi manii, kisha pande la damu, la nyama, utoto hadi kukomaa, yanafahamisha waziwazi kwamba binadamu ana nguvu na maandalizi yatakayompeleka kwenye ukamilifu na ubora, ikiwa hakutakuwa na vizuizi vya kuzuia kufikia lengo hili.

**Na unaiona ardhi imekufa, lakini tunapoyateremsha maji juu yake, husisimka na kututumka na kumea kila aina ya mimea mizuri**.

Maji yakishuka kwenye ardhi iliyokufa hutaharaki na kupumua kwa uhai, kisha inatoa aina kwa aina za mimea inayovutia macho na yenye ladha kwa walaji.

Hakuna mwenye shaka kwamba ardhi ni maandalizi ya kuukabili uhai, lakini mpaka kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu kila kitu kinaishia kwenye kauli yake 'kuwa na kinakuwa' Baadhi ya masufi wanasema: Makusudio ya ardhi iliyokufa ni ujinga, maji ni elimu na aina mbalimbali za mimea ni sifa za ukamilifu za Mwenyezi Mungu.

**Hayo ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu ni haki na kwamba hakika yeye ndiye Mwenye kuhuisha wafu na kwamba hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu na kwamba saa itakuja hapana shaka kwa hilo na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini**.

Hayo ni ishara ya mambo yalivyo. Maana ya kuwa Mwenyezi Mungu ni haki ni kwamba hukumu na ufalme ni wake yeye peke yake bila ya kushirikiana na yeyote na kwamba hakuna kupatikana isipokuwa kutokana na yeye.

Hiyo ikiwa na maana kwamba yeye ndiye mwanzishaji na mrudishaji na ufufuo utakuwako tu kama ulivyokuwako uumbaji; bali huo uumbaji ni nyenzo na njia ya kufikia ufufuo ambao ndio lengo la malengo yote.

Kwa sababu mtu anarejea kwa muumba wake kuhisabiwa na kulipwa na pia hapo ndio pa kubakia, lakini kule kuumbwa kwa kwanza kuliisha. Kwisha ni nyenzo ya kubakia.

Hapa ndio tunakuta tafsiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu:

{وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ {56

***“Na sikuumba majini na watu ila waniabudu.” (51:56).***

Yametangulia maelezo ya ufufuo katika Aya kadhaa; miongoni mwazo ni: Juz. 1 (2:28-29) kifungu cha 'Ufufuo,' Juz. 5 (4:85-87) kifungu cha 'Njia mabalimbali za kuthibitisha marejeo (ufufuo) na Juz. 13 (13: 5-7) kifungu cha 'Wanaoamini maada na maisha baada ya mauti.'

{وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُنِيرٍ {8

***Na katika watu wapo wanaojadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ilimu wala uongufu wala Kitabu chenye nuru.***

{ثَانِيَ عِطْفِهِ لِيُضِلَّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ۖ لَهُ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ ۖ وَنُذِيقُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَذَابَ الْحَرِيقِ {9

***Anayegeuza shingo yake ili awapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu. Duniani atapata hizaya na siku ya Kiyama tutamuonjesha adhabu ya kuungua.***

{ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمَتْ يَدَاكَ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ لِلْعَبِيدِ {10

***Hayo ni kwa sababu ya iliyotanguliza mikono yako na kwamba Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja.***

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ ۖ فَإِنْ أَصَابَهُ خَيْرٌ اطْمَأَنَّ بِهِ ۖ وَإِنْ أَصَابَتْهُ فِتْنَةٌ انْقَلَبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ خَسِرَ الدُّنْيَا
{وَالْآخِرَةَ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ {11

***Na katika watu wapo wanaomwabudu Mwenyezi Mungu ukingoni. Ikimfika kheri hutulia kwayo, na ukimfikia msukosuko hugeuza uso wake. Amepata hasara ya dunia na Akhera; hiyo ndiyo hasara iliyo wazi.***

{يَدْعُو مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُ وَمَا لَا يَنْفَعُهُ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَالُ الْبَعِيدُ {12

***Anaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, kile kisichomdhuru wala kumnufaisha. Huko ndiko kupotelea mbali.***

{يَدْعُو لَمَنْ ضَرُّهُ أَقْرَبُ مِنْ نَفْعِهِ ۚ لَبِئْسَ الْمَوْلَىٰ وَلَبِئْسَ الْعَشِيرُ {13

***Anamuomba yule ambaye hakika dhara iko karibu zaidi kuliko nafuu yake. Hakika ni mlinzi mbaya na ni rafiki mbaya.***

{إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ {14

***Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza wale walioamini na wakatenda mema katika bustani zipitazo mito chini yake. Hakika Mwenyezi Mungu hufanya ayatakayo.***

# Aya 8 – 14: Sababu Ya Maarifa Katika Aya Moja

## Maana

**Na katika watu wapo wanaojadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ilimu wala uongufu wala Kitabu chenye nuru**.

Wewe unaona hii ndiyo haki na ile ni batili, lakini ni lipi lililokujulisha kwamba rai yako ni sahihi na salama? Una dhamana gani ya usahihi huo? Inawezekekana kuwa ile unayoiona ni haki kumbe ni batili na ile unayoiona ni batili kumbe ni haki.
Hakuna njia ya kujua maarifa sahihi isipokuwa kwa kurejea kwenye chimbuko lake na sababu iliyotokana nayo. Ikiwa sababu ni sahihi basi maarifa nayo yatakuwa sahihi; vinginevyo yatakuwa batili. Kwa sababu tawi lina- fuata shina.

Swali linarudi tena: Je, ni ipi hiyo sababu ya maarifa sahihi? Utaitambuaje? Jamaa katika wanafalsafa wanasema kuwa sababu ya maarifa sahihi inakuwa kwenye majaribio ya hisia tu. Wengine wakasema ni akili; na hisia ni vyombo tu. Ama Qur'an, katika Aya tunayoifasiri, imetaja sababu tatu za maarifa: Kwanza ni majaribio ya hisiya yaliyotajwa kwa neno 'ilimu' Ya pili ni akili iliyoitwa 'Uongofu' Ya tatu ni Wahyi iliyokusudiwa kwenye neno 'Kitabu chenye nuru'.

Majaribo ya hisia yanakuwa ni sababu ya kujua vitu vya kimaada tu. Kwa sababu ndivyo vinavyoweza kuhisiwa na kufanyiwa majaribio. Tena majaribio haya huwa yanahitajia akili, kwa sababu hisia haziwezi kutambua kitu ila kwa msaada wa akili.

Ni akili pekee ndiyo inayoweza kujua na kuthibitisha kuweko Mungu. Ama utume unathibitika kwa akili na kwa miujiza. Ukitaka ibara ya ndani zaidi sema: Utume unathibitika kwa miujiza inayothibitishwa na akili na kuikubali kuwa imetoka mbinguni sio ardhini.

Ama wahyi ni sababu ya kujua kila uliyokuja nayo. Wahyi ndio njia pekee ya kujua mambo ya ghaibu; kama majini, Malaika, Kiyama, namna ya hisabu na na malipo kwenye ufufuo n.k.

**Anayegeuza shingo yake ili awapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu. Duniani atapata hizaya, na siku ya Kiyama tutamuonjesha adhabu ya kuungua.**

Kugeuza shingo ni kinaya cha kiburi.

Yeye hajui kitu, anajadili kuhusu Mungu bila ya ujuzi, ana kiburi kinachomuhadaa na ni mpotevu na mpotezaji. Hakuna malipo ya wajinga weneye kiburi isipokuwa kudharaulika na kupuuzwa na watu na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hayo ni kwa sababu ya iliyotanguliza mikono yako na kwamba Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja. Kwa sababu amewaondolea udhu– ru kwa kuwapa akili, kuwapelekea mitume na akateremsha vitabu.

**Na katika watu wapo wanaomwabudu Mwenyezi Mungu ukingoni.**

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amemtaja anayemkufuru Mwenyezi Mungu na kumjadili bila ya elimu. Hapa anamtaja yule anayemwabudu Mwenyezi Mungu ukingoni.

Wafasiri wametofautiana katika makusudio ya kabudu ukingoni. Kuna waliosema kuwa ni kumwabudu Mwenyezi Mungu pamoja na shaka katika dini. Wengine wakasema ni kumwabudu kwa ulimi tu sio kwa moyo na kauli nyingine.

Hakuna haja ya kutofautiana huku wakati Mwenyezi Mungu amekwisha mbainisha anayemwabudu ukingoni kwa kusema:

**Ikimfika kheri hutulia kwayo na ukimfikia msukosuko hugeuza uso wake.**

Makusudio ya kheri hapa ni mambo ya kufurahisha na misukosuko ni madhara. Kutulia ni kuwa na raha na kuendelea na ibada, na kugeuza uso ni kurtadi dini. Maana ni kuwa anayemwabudu Mwenyezi Mungu ukingoni ni yule anayeweka sharti kwa ibada yake, mpaka apate kitu ndio anaabudu vinginevyo humkufuru Mungu, vitabu vyake na mitume yake.

Na yoyote mwenye kumkufuru basi malipo yake ni Jahannam na ni mwisho mbaya.

**Amepata hasara ya dunia na Akhera; hiyo ndiyo hasara iliyo wazi.**

Amepata hasara ya nyumba mbili: ambapo mwanzo ni balaa na madhara. Pili, atafika kwa Mola wake akiwa anamkufuru. Kuna hasara kubwa zaidi ya ufukara duniani na adhabu akhera.

Ufafanuzi zaidi wa Aya hii ni riwaya inayosema kwamba baadhi ya mabedui walikuwa wakifika kwa Mtume (s.a.w.) wakihama kutoka ubeduini kwao.

Basi mmoja wao akiwa na mali nyingi huswali na kufunga. Akipatwa na masaibu au akicheleweshewa sadaka basi huritadi. Nimeyashuhudia yanayofanana na haya nilipokuwa nikiishi na baadhi ya wanakijiji.

Baada ya hayo, hakika mumin wa kweli ni yule anayemfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu na kumtegemea katika hali zote; anakuwa na subira wakati wa shida na anashukuru wakati wa raha.

Katika *Nahjul balagha* kuna maelezo haya: "Haiwi kweli imani ya mja mpaka yawe yaliyo mikononi mwa Mwenyezi Mungu anayategemea zaidi kuliko yaliyo mikononi mwake."

**Anaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, kile kisichomdhuru wala kumnufaisha. Huko ndiko kupotelea mbali.**

Maana ya Aya hii yametangulia kwenye Aya nyingi, yenyewe pia iko wazi.

**Anamuomba yule ambaye hakika dhara iko karibu zaidi kuliko nafuu yake. Hakika ni mlinzi mbaya na ni rafiki mbaya.**

Unaweza kuuliza kuwa katika Aya ya kwanza Mwenyezi Mungu amekanusha kuweko manufaa na madhara kwa yale wanayoyaabudu washirikina, kisha katika Aya hii anathibitisha kuweko manufaa ya mbali na madhara ya karibu. Je, kuna wajihi gani baina ya Aya mbili hizi?

Jibu: makusudio ya chenye kuabudia katika Aya ya kwanza ni mawe; hayanufaishi wala hayadhuru. Na makusudio katika Aya ya pili ni kuwatii viongozi mataghuti na kuwataka usaidizi kwa kukusudia kupata faida na manufaa, na ukubwa wa manufaa ya duniani si chochote kulinganisha na ghadhabu za Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

Kwa maneno mengine ni kwamba wao wanamtii kiumbe kwa kumuasi muumba kwa ajili ya manufaa ya dunia, hawajui kwamba adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali na kubwa zaidi.

**Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza wale walioamini na wakatenda mema katika bustani zipitazo mito chini yake.**

Aya iko wazi na pia imekwishatangulia katika Juz. 1 (2: 25).

**Hakika Mwenyezi Mungu hufanya ayatakayo** katika kuwapa thawabu wema na kuwaadhibu waovu. Na amekwishapitisha kuwa waliofanya mema atawalipa mema na wabaya atawalipa ubaya kutona na waliyoyafanya.

مَنْ كَانَ يَظُنُّ أَنْ لَنْ يَنْصُرَهُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ فَلْيَمْدُدْ بِسَبَبٍ إِلَى السَّمَاءِ ثُمَّ لْيَقْطَعْ فَلْيَنْظُرْ هَلْ يُذْهِبَنَّ كَيْدُهُ مَا يَغِيظُ {15}

***Anayedhani kwamba Mwenyezi Mungu hatamnusuru katika dunia na Akhera, basi na afunge***

***kamba mbinguni kisha aikate, aone je, hila yake itaondoa yale yaliyomghadhabisha?***

{وَكَذَٰلِكَ أَنْزَلْنَاهُ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ وَأَنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يُرِيدُ {16

***Na namna hiyo tumeiteremsha kuwa ni Aya zilizo wazi na kwamba Mwenyezi Mungu humuongoza anayetaka.***

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّابِئِينَ وَالنَّصَارَىٰ وَالْمَجُوسَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا إِنَّ اللَّهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ إِنَّ
{اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ {17

***Hakika wale ambao wameamini na ambao ni mayahudi na wasabai na wanaswara na wamajusi na wale washirikishao, hakika Mwenyezi Mungu atawapambanua siku ya Kiyama. Hakika Mwenyezi Mungu ni shahidi juu ya kila kitu.***

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ وَالدَّوَابُّ
{وَكَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ ۖ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ ۗ وَمَنْ يُهِنِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُكْرِمٍ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ۩ {18

***Je huoni kuwa vinamsujudia Mwenyezi Mungu vilivyo mbinguni na vilivyo ardhini na jua na mwezi na nyota na milima na miti na wanyama na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahili adhabu. Na anayetwezwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumheshimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.***

# Aya 15 -18: Ajinyonge

## Lugha

Wengi wamesema kuwa makusudio ya mbingu hapa ni dari ya nyumba, kukata ni kujinyonga na hila yake ni huko kujinyonga kwake. Kwa hiyo maana yatakuwa: Anayedhani kwamba Mwenyezi Mungu hatamnusuru katika dunia na Akhera, basi na afunge kitanzi ajinyonge aone je huko kujinyonga kutamuondolea ghadhabu yake?

## Maana

Wafasiri wengi wamesema kuwa dhamiri ya 'hawatamnusuru' inamrudia Muhammad (s.a.w.) na maana yawe: Anayedhani katika washirikina kuwa Mwenyezi Mungu hatamnusuru Mtume wake Muhammad

(s.a.w.), basi na amnyonge aone kama Mwenyezi Mungu hatamnusuru Mtume wake.

Lakini dhahiri ya mfumo wa Aya inaonyesha kuwa dhamiri inamrudia huyo anayedhani, kwa sababu Muhammad (s.a.w.) hakutajwa katika Aya. Na maana yanakuwa:

Ambaye ameshukiwa na balaa na akachukia kadha ya Mwenyezi Mungu na kadari yake, akakata tamaa kwamba Mwenyezi Mungu atamsaidia duniani na kumpa thawabu akhera kwa sababu ya kuvumilia kwake, atakayekuwa hivyo basi hatakuwa na la kufanya isipokuwa kujinyonga kwa kujifunga kamba kwenye dari ya nyumba yake; kisha aangalie je, hilo ndilo suluhisho?

Mwenye akili anapotokewa na balaa, hufanya juhudi na bidii kuiondoa huku akitaka msaada kwa Mwenyezi Mungu, akifaulu ni sawa, la sivyo humwachia Mwenyezi Mungu mambo yote huku akingoja fursa.

**Na namna hiyo tumeiteremsha kuwa ni Aya zilizo wazi na kwamba Mwenyezi Mungu humuongoza anayetaka.**

Dhamiri katika iliyoteremshwa inarudia Qur'an. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) humwongoza anayetaka kuongoka kwa Kitabu chake na humwongoza kwenye wema wa nyumba mbili yule anayetafuta mwongozo kwake na kwa Mtume wake.

Na mwenye kutafuta upotevu na ufisadi ataipata njia yake kwa wafisadi na wapotevu.

**Hakika wale ambao wameamini na ambao ni mayahudi na wasabai na wanaswara na wamajusi na wale washirikishao, hakika Mwenyezi Mungu atawapambanua siku ya Kiyama. Hakika Mwenyezi Mungu ni shahidi juu ya kila kitu.**

Wasabai wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, lakini wanaamini kuwa baadhi ya nyota zina athari katika kheri na shari, wamajusi wanaabudu moto kwa kusema kuwa kheri inatokana na nuru na shari inatokana na giza na wanaswara ni wakristo.

Mwenyezi Mungu anayajua makundi yote haya sita na atayapambanua kesho siku ya Kiyama na kumlipa kila mmoja kwa vile alivyofanya. Kafiri atamwingiza motoni na mumin atamwingiza Peponi. Umetangulia mfano wa Aya hii katika Juz. 1 (2:117).

**Je huoni kuwa vinamsujudia Mwenyezi Mungu vilivyo mbinguni na vilivyo ardhini na jua na mwezi na nyota na milima na miti na wanyama.**

Wamesema jamaa katika wafasiri kwamba makusudio ya kusujudi wanyama mimea n.k. Ni kutii amri yake na kwamba yeye anawafanyia vile atakavyo.

Katika Juz. 15 (17:44) tumeeleza kuwa makusudio ya kusujudi vitu visivyo na harakati, miti na mimea ni kule kufahamisha kwake kuweko muumba wake na utukufu wake. Mulla Sadra katika kitabu *Al-Asfar*

anasema: “Vitu vyote vina akili, vinamfahamu Mola wake na kumjua muumba wake, vinasikia maneno yake na kufuata amri yake”

Haya hayako mbali, akili inakubali na dhahiri ya nukuu inalithibitisha. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

{وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَٰكِنْ لَا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ ۗ {44

***“Na hapana kila kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake, lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake.” Juz. 15 (17:44).***

Sayansi itagundua hakika hii hivi karibuni au baadaye.

**Na wengi miongoni mwa watu** wanamwamini na wanamsujudia. **Na wengi** miongoni mwao **imewastahili adhabu.**

Hao ni wale waliomkufuru Mwenyezi Mungu wanaowadharau wale wanaomwamini Mungu. Ilikuwa inafaa kwa mwenye kitabu *Al-Asfar*, awavue wanaomkana Mungu katika viumbe.

**Na anayetwezwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumheshimu.**

Kabisa! Hakuna wa kumuinua aliyeangushwa na kudhalilishwa na Mwenyezi Mungu, wala hakuna wa kumdhalilisha aliyetukuzwa na kuenziwa na Mwenyezi Mungu, na hakuna utukufu mbele ya Mwenyezi Mungu ila kwa wenye takua.

**Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo** kuwatukuza wema na kuwatweza wapotevu na wafisadi.

Baada ya hayo. Hakika Mwenyezi Mungu ana desturi katika viumbe vyake haiachi; nayo ni kuwa mwenye kufuata nji ya maangamizi ataangamia, na mwenye kufuata njia ya usalama atasalimika. Njia ya usalama mbele ya Mwenyezi Mungu ni imani ya kweli na matendo mema; na njia ya kufedheheka na kupuuzwa ni unafiki na ufisadi katika ardhi.

{هَٰذَانِ خَصْمَانِ اخْتَصَمُوا فِي رَبِّهِمْ ۖ فَالَّذِينَ كَفَرُوا قُطِّعَتْ لَهُمْ ثِيَابٌ مِنْ نَارٍ يُصَبُّ مِنْ فَوْقِ رُءُوسِهِمُ الْحَمِيمُ {19

***Hawa mahasimu wawili waliohasimiana kwa ajili ya Mola wao. Basi waliokufuru watakatiwa nguo za moto na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yanayochemka.***

{يُصْهَرُ بِهِ مَا فِي بُطُونِهِمْ وَالْجُلُودُ {20

***Kwayo vitayeyushwa vilivyo matumboni mwao na ngozi.***

{وَلَهُمْ مَقَامِعُ مِنْ حَدِيدٍ} 21

***Na yatakuwako makomeo ya chuma kwa ajili yao.***

{كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ} 22

***Kila wanapotaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo; na onjeni adhabu ya kuungua.***

{إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۖ وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ} 23

***Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walioamini na wakatenda mema katika bustani zipitiwazo na mito chini yake. Watapambwa humo kwa vikuku vya dhahabu na lulu na mavazi yao humo ni hariri.***

{وَهُدُوا إِلَى الطَّيِّبِ مِنَ الْقَوْلِ وَهُدُوا إِلَىٰ صِرَاطِ الْحَمِيدِ} 24

***Na wataongozwa kwenye maneno mazuri na kuongozwa kwenye njia ya mwenye kuhimidiwa.***

{إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ الَّذِي جَعَلْنَاهُ لِلنَّاسِ سَوَاءً الْعَاكِفُ فِيهِ وَالْبَادِ ۚ وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍ بِظُلْمٍ نُذِقْهُ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ} 25

***Hakika wale waliokufuru na wakawazuilia njia ya Mwenyezi Mungu na Msikiti mtakatifu ambao tumeufanya kwa ajili ya watu wote sawa sawa, kwa wakaao humo na wageni. Na kila atakayefanya upotofu humo kwa dhulma tutamwonjesha adhabu chungu.***

# Aya 19 – 25: Mahasimu Wawili

## Maana

**Hawa mahasimu wawili waliohasimiana kwa ajili ya Mola wao.**

Kuna maelezo katika *Tafsir At-Tabari* kwamba Abu dharr alikuwa akiapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba

Aya hii imeshuka kwa ajili ya watu sita katika makuraishi; watatu miongoni mwao ni waumini nao ni Hamza bin Abdul-Muttalib, Ali bin Abu Twalib na Ubayda bin Al-Harith.

Na watatu ni katika washirikina nao ni: Utba na Shayba, watoto wa Rabia na Walid bin Utba. Uhasama baina yao ulikuwa katika vita vya Badr walipobariziana; na Mwenyezi Mungu akawapa nusra waumini kuwashinda washirikina.

Jamaa katika wafasiri wamesema kwamba makusudio ya waliohasimiana ni kikundi cha waumini na kikundi cha makafiri ambao ni mayahudi, wanaswara, wasabai, majusi na washirikina. Kwa sababu wote hao wametajwa katika Aya iliyotangulia na kila kundi linasema lina haki kuliko jingine.

Vyovyvote iwavyo ni kwamba uhasama katika dini unatokea baina ya wanaoamini.

**Basi waliokufuru watakatiwa nguo za moto na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yanayochemka. Kwayo vitayeyushwa vilivyo matumboni mwao na ngozi. Na yatakuwako makomeo ya chuma kwa ajili yao. Kila wanapotaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo, na onjeni adhabu ya kuungua.**

Baada ya Mwenyezi Mungu kuashiria uhasama wa waumini na makafiri anataja kwamba mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu mwisho wake ni Peponi na mwenye kumkufuru mwisho wake ni Jahannam, mwisho mbaya kabisa.
Na kwamba watu wake watavaa kivazi cha moto na watamiminiwa maji ya moto ambayo yatayeyusha mafuta, nyama matumbo na ngozi. Pia nguzo za chuma zitakuwa vichwani mwao kuwazuia kutoka kila wanapojaribu kukimbia. Inawezekena kukimbia hukumu ya Mwenyezi Mungu na matakwa yake? Umepita mfano wake katika Juz. 13 (14: 49 – 50) kifungu cha 'Jahannam na silaha za maangamizi'

**Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walioamini na wakatenda mema katika bustani zipitiwazo na mito chini yake. Watapambwa humo kwa vikuku vya dhahabu na lulu na mavazi yao humo ni hariri.**

Makafiri watakuwa na mavazi ya moto, makomeo ya chuma, maji ya moto na waumini wenye ikhlasi watapata pepo yenye neema, mito yenye kinywaji cha ladha, nguo za hariri na vipambo vya dhahabu na lulu.

**Na wataongozwa kwenye maneno mazuri.**

Baada ya Mwenyezi Mungu kuashiria kwenye chakula na kinywaji chao, anataja kauli zao ambazo ni nzuri; mfano *Alhamdulillah*. **Na kuongozwa kwenye njia ya mwenye kuhimidiwa.** Hiyo ni njia yenye kunyooka waliyoifuata katika maisha ya dunia, ikawapeleka kwenye neema ya Akhera.

**Hakika wale waliokufuru na wakawazuilia njia ya Mwenyezi Mungu na Msikiti mtakatifu ambao tumeufanya kwa ajili ya watu wote sawa- sawa, kwa wakaao humo na wageni.**

Washirikina wa kikuraishi walikuwa wakiwazuilia watu kuiingia kwenye Uislamu, kuhiji na kufanya umra kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu ambayo ameifanya ni mahali pa kuendewa na watu na mahali pa amani. Umepita mfano wake katika Juz. 1 (2:125).

**Na kila atakayefanya upotofu humo kwa dhulma tutamwonjesha adhabu chungu.**

Yaani atakayeacha yale aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu na akamfanyia uovu anayeikusudia nyumba ya Mwenyezi Mungu tukufu, basi Mungu atamwadhibu adhabu kubwa.

{وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَاهِيمَ مَكَانَ الْبَيْتِ أَنْ لَا تُشْرِكْ بِي شَيْئًا وَطَهِّرْ بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ {26

***Na tulipomwekea Ibrahim mahala penye ile nyumba kwamba usinishirikishe na chochote na uitwaharishe nyumba yangu kwa ajili ya wanozunguka na wakaazi na wanaorukui na wanaosujudi.***

{وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ {27

***Na watangazie watu Hijja; watakujia kwa miguu na juu ya kila mnyama aliyekonda kutoka kila njia ya mbali.***

لِيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ فِي أَيَّامٍ مَعْلُومَاتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِنْ بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ ۖ فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطْعِمُوا
{الْبَائِسَ الْفَقِيرَ {28

***Ili washuhudie manufaa yao na walitaje jina la Mwenyezi Mungu katika siku maalum juu ya wanyama hawa aliowaruzuku.***

{ثُمَّ لْيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ {29

***Basi kuleni katika hao na mumlishe mwenye shida aliye fukara, kisha wajisafishe taka zao na watimize nadhiri zao na waizunguke sana nyumba ya kale.***

# Aya 26 -29: Itwaharishe Nyumba Yangu

## Maana

**Na tulipomwekea Ibrahim mahala penye ile nyumba kwamba usin- ishirikishe na chochote na uitwaharishe nyumba yangu kwa ajili ya wanozunguka na wakaazi na wanaorukui na wanaosujudi**.

Makusudio ya wakaazi ni wakaazi wa Makka na viunga vyake; na wanorukui wakisujudi ni wanaoswali.

Makuraishi walikuwa wakiabudu masanamu na wakisimamia Al-Kaaba. Baada ya Mwenyezi Mungu kumtuma Muhammad (s.a.w.) walianza kuwa na uadui naye na kila anayemwamini, tena wakawazuilia waislamu kuizunguka (tawaf) na kuswali hapo; kama ilivyoelezwa kwenye Aya iliyotangulia. Pamoja na hayo Makuraishi walikuwa wakidai kwamba wako kwenye dini ya Ibrahim (a.s.).

Ndio Mwenyezi Mungu akabatilisha madai yao haya, kwamba yeye ndiye mwenye nyumba hiyo na alimpa wahyi kuwa aijenge na aifanye ni mahsusi kwa ibada ya wanaompwekesha Mungu wanaokaa hapo na wanaopita na pia kuwaweka mbali nayo washirikina na mizimu yao.

Haya ndio maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu 'Na uitwaharishe nyumba yangu' lakini makuraishi waliipindua Aya, wakaijaza masanamu nyumba ya Mwenyezi Mungu, wakaihalalishia washirikina na wafisadi na wakawazulia nayo watu wa tawhid na wema.

**Na watangazie watu Hijja; watakujia kwa miguu na juu ya kila mnyama aliyekonda kutoka kila njia ya mbali**.

Mwenyezi Mungu alimwamrisha kipenzi chake awaite watu kuhiji kwenye msikiti mtakatifu baada ya kusimamisha misingi yake na kutimia jengo. Akamwahidi kuwa watu watamwitikia na watamjia kwa kila hali; kutembea kwa miguu na kupanda ngamia au farasi waliokonda tena kutoka mbali, sikwambii karibu.

**Ili washuhudie manufaa yao**.

Hijja ni ibada pekee inayochanganya manufaa ya kidini na ya kidunia. Ama ya kidini ni kumtii Mwenyezi Mungu kwa kutekeleza faradhi ya Hijja, kutubia na kutambua haiba ya Mwenyezi Mungu na utukufu. Ibn Al- Arabi anasema katika Kitabu *Futuhatul- Makkiyya*:

"Siku moja nilikuwa nikitufu Al-Kaaba nikaiona kama kwamba imenyanyuka kutoka ardhini, wallah, ikaniambia maneno niliyoyasikia: njoo uone nitakavyokufanyia, mara ngapi hadhi yangu unaiweka chini na ya binadamu unaiinua juu?.

Nasi tunasema kwa uhakika: hakuna yeyote anayefanya *sa'yi* au *tawaf* katika nyumba ya Mwenyezi Mungu kwa ikhlas ila atahisi aina ya kitu kama hiki.

**Na walitaje jina la Mwenyezi Mungu katika siku maalum juu ya wanyama howa aliowaruzuku,** ambao ni ngamia ng'ombe na mbuzi na kondoo.

Kumtaja Mwenyezi Mungu kwenye wanyama ni kinaya cha kuchinja, kwa sababu kusoma *Bismillah* ni wajibu katika kuchinja. Makusudio ya siku maalum ni siku za kuchinja katika Hijja, kama inavyofahamisha Aya.

Mafakihi wametofautiana katika idadi ya siku hizo: Shia wamesema ni nne, mwanzo wake ni siku ya Idul-adh'ha na mwisho wake ni tarehe kumi na tatu ya Dhul-hijja. Mafakihi wa madhehbu mengine wamesema ni tatu kwa kuishia tarehe kumi na mbili. Ufafanuzi uko katika kitabu chetu *Alfiqh ala madhahibil-khamsa*[1]

Razi anasema kuwa maulama wengi wanatofautisha baina ya siku maalum na siku za kuhisabiwa zilizotajwa katika Juz. 2 (2:203) na wanaona kuwa siku maalum ni siku kumi za mwezi wa Dhul-hijja na za kuhisabiwa ni siku za kuchinja.

**Basi kuleni katika hao na mumlishe mwenye shida aliye fukara**.

Wameafikiana mafakihi kuhusu wajibu wa kumlisha fukara mnyama wa Hijja na wakatofautina katika wajibu wa mwenyewe kula. Sisi tuko pamoja na wale wanaosema kuwa si wajibu kwa mwenyewe kula. Ni vile atavyoona, akipenda atakula na akipenda ataitoa sadaka yote. Ama kauli yake Mwenyezi Mungu: '**Kuleni katika hao**' ni kwa ajili ya kuondoa fikra ya uharamu wa kula; ambapo wakati wa jahiliya walikuwa hawali wanyama hao wawachinjao wakidai kuwa ni haramu kwao. Ndipo Mwenyezi Mungu akawazindua kosa lao hilo.

**Kisha wajisafishe taka zao**.

Haijuzu kwa aliye kwenye Hijja akiwa kwenye ihram (Vazi maalum la Hijja) kunyoa, kukata kucha au kujipaka manukato; bali mafakihi au wengi wao wamesema kuwa hata kuua vidudu vya mwilini, kama vile chawa pia ni haramu. Zikiisha zile siku za Ihram basi inakuwa ni halali kwake yale yaliyokuwa ni haramu, basi hapo atanyoa, kukata kucha n.k. Ndipo kwa hili ameshiria Mwenyezi Mungu aliposema:

**Kisha wajisafishe taka zao**.

**Na watimize nadhiri zao,** ikiwa wameweka nadhiri siku za Hijja au kabla. Kwa sababu watu wengi huweka nadhiri ya kutoa sadaka ikiwa Mwenyezi Mungu atawaruzuku Hijja.

**Na waizunguke sana nyumba ya kale**. Kwa sababu ndio nyumba ya kwanza kuwekewa watu kwa ajili ya ibada.

Mwenyezi Mungu ameleta tamko la 'sana' kwa sababu ni Sunna kufanya tawaf mara nyingi; kama ambavyo pia ni Sunna kuswali sana. Kuna Hadithi mashuhuri kutoka kwa Mtume wa rehema, aliposema: "Kuizunguka Al-Kaaba ni Swala.'

ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعَظِّمْ حُرُمَاتِ اللَّهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ عِنْدَ رَبِّهِ ۗ وَأُحِلَّتْ لَكُمُ الْأَنْعَامُ إِلَّا مَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ ۖ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ

{الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ {30

***Ndivyo hivyo! Na anayeitukuza miiko ya Mwenyezi Mungu hiyo ni kheri yake mbele ya Mola wake. Na mmehalalishiwa wanyama howa ila wale mliosomewa. Basi jiepusheni na uchafu wa mizimu na mjiepushe na kauli ya uzushi.***

حُنَفَاءَ لِلَّهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِ ۚ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ السَّمَاءِ فَتَخْطَفُهُ الطَّيْرُ أَوْ تَهْوِي بِهِ الرِّيحُ فِي مَكَانٍ
{سَحِيقٍ {31

***Kwa kumtakasia imani Mwenyezi Mungu bila ya kumshirikisha. Na anayemshrikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukampeleka mahala mbali.***

{ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ {32

***Ndivyo hivyo! Na anayezitukuza nembo za Mwenyezi Mungu. Basi hiyo ni katika takua ya nyoyo.***

{لَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُسَمًّى ثُمَّ مَحِلُّهَا إِلَى الْبَيْتِ الْعَتِيقِ {33

***Katika hao nyinyi mna manufaa mpaka muda uliowekwa kisha mahali pake ni nyumba ya kale.***

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا لِيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِنْ بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ ۗ فَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ فَلَهُ أَسْلِمُوا ۗ وَبَشِّرِ
{الْمُخْبِتِينَ {34

***Kila umma tumeujaalia mihanga ya ibada, ili wamtaje Mwenyezi Mungu katika vile alivyowaruzuku katika wanyama howa. Basi Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, Kwa hiyo jisalimisheni kwake. Na wabashirie wanyenyekevu.***

{الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَالصَّابِرِينَ عَلَىٰ مَا أَصَابَهُمْ وَالْمُقِيمِي الصَّلَاةِ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ {35

***Ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hutetemeka na walio na subira kwa yale yaliyowasibu, na wanao-simamisha Swala, na wanatoa katika tulivyowaruzuku.***

1. Kimefasiriwa kwa kiswahili kwa jina la Fiqh katika madhebu tano - Mtarjumu

# Aya 30 –35: Miiko Ya Mungu Na Nembo Zake

## Maana

**Ndivyo hivyo! Na anayeitukuza miiko ya Mwenyezi Mungu hiyo ni kheri yake mbele ya Mola wake.**

Kutukuza kuko aina nyingi kutegemea na anayetukuzwa na namna ya kutukuzwa inayokubaliana naye.

Hakuna kitu kinachokubaliana na kumtukuza muumba isipokuwa kumtii na kufuata amri yake katika kila jambo. Atakayemtii Mwenyezi Mungu na akafuata amri zake na kuacha makatazo yake, basi atakuwa ametukuza na kuadhimisha miiko yake na nembo zake. Taadhima hii au utiifu huu unamwinua aliyeutenda kwa muumba wake, sio kuwa unamwinua muumbaji, kwa sababu Yeye hawahitajii walimwengu.

Ndio maana akasema:'Hiyo ni kheri yake mbele ya Mola wake' yaani kutukuza hukumu za Mwenyezi Mungu kwa kumtii ni kheri ya huyo mtiifu.

**Na mmehalalishiwa wanyama howa ila wale mliosomewa.**

Mwenyezi Mungu amemharamishia anayehiji kuwinda akiwa katika Ihram yake, pengine anaweza akadhania kuwa ameharamishiwa kula nyama ya wanyama wa kufugwa. Ndio akabainisha kuwa hakuna uhusiano baina ya mawili hayo; na kwamba walioharamishwa ni mfu na waliochinjiwa mizimu. Angalia Juz. 6 (5:3).

**Basi jiepusheni na uchafu wa mizimu.**

Jiepusheni nayo na msiiabudu, kama mnavyojiepusha na uchafu, kwa sababu yote ni uchafu, ndio maana ikafasiriwa uchafu wa mizimu, ingawaje kuna herufi *min*, ambayo hapa imekuwa ya kueena na sio ya baadhi, kama inavyokuwa mara kwa mara.

**Na mjiepushe na kauli ya uzushi.**

Kauli ya uzushi inachanganya kila lilioharamishwa; iwe ni uongo, kusengenya, shutuma na ufyosi. Uzushi mbaya zaidi ni kuleta ushahidi wa uongo, kwa sababu unanyima haki ya Mungu na ya watu. Mtume (s.a.w.) anasema: "Uzushi umelinganishwa na kumshirikisha Mwenyezi Mungu," kisha akasoma Aya hii.

**Kwa kumtakasia imani Mwenyezi Mungu bila ya kumshirikisha.**

Yaani kushikamana na dini ya haki na kuachana na dini potofu. Bila ya kumshirikisha ni msisitizo wa hayo. Tumelizungumzia hilo kwa ufafanuzi zaidi katika Juz. 15 (17:107).

**Na anayemshrikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukampeleka mahala mbali**.

Hiki ni kinaya cha dhambi ya shirki kwamba haifanani na dhambi yoyote, na kwamba adhabu ya mshirikina haishindwi na adhabu yoyote. Mwenye kufuatilia Aya za Qur'an na Sunna za Mtume ataona kuwa mshirikina ana dhambi kubwa zaidi kuliko mlahidi mbele ya Mwenyezi Mungu.

Inawezekana siri ya hilo ni kuwa mlahidi hathibitishi upungufu wa muumba, kwa sababu yeye hakubali kabisa kuwa yuko. Hii pia ni dhambi kubwa, hilo halina shaka, lakini dhambi ya mshirikina ni kubwa zaidi, kwa sababu ni kumshirikisha muumba kwa upande mmoja na ni kuthibitisha upungufu kwa muumba kwa upande wa pili.

**Ndivyo hivyo**! **Na anayezitukuza nembo za Mwenyezi Mungu**. **Basi hiyo ni katika takua ya nyoyo**.

Nembo za Mwenyezi Mungu na miiko yake zina maana moja. Tumezungumzia kuhusu miiko katika Aya iliyotangulia. Hakuna mwenye shaka kwamba hawatii amri za Mwenyezi Mungu isipokuwa wenye takua na ikhlasi.

Miongoni mwa kutukuza nembo za Mwenyezi Mungu na kutii hukumu yake ni kuchinja mnyama aliyenona asiye na kasoro yoyote siku za Hijja. Mtume (s.a.w.) anasema: "Hafai aliye kiguru, wala aliyekonda, wala aliyetobolewa sikio wala aliyekatwa sikio wala aliyevunjika pembe."

**Katika hao nyinyi mna manufaa mpaka muda uliowekwa**.

Katika hao ni hao wa kuchinjwa kwenye Hijja. Muda uliowekwa ni wakati wa kuchinjwa. Maana ni kuwa mwenye kuhiji anaruhusiwa kunufaika na maziwa na mgongo wa mnyama wa kuchinja mpaka wakati wa kuchinja.

Katika *Tafsiru-Razi* imeelezwa kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpitia mtu akimkokokota mnyama na yeye mwenyewe amechoka. Mtume akamwambia: "Mpande." Yule mtu akasema: "Huyu ni wa kuchinja kwa ajili ya Hijja ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!" Akasema Mtume: "Ole wako, mpande!"

Anaendelea kusema Razi: "Abu Hanifa hajuzishi hilo, akatoa hoja kuwa haijuzu kumkodisha kwa hiyo haijuzu kumpanda." Razi akamjibu Abu Hanifa kwamba hoja hii ni dhaifu, kwa sababu, mjakazi aliyezaa na mmiliki wake hauzwi, lakini inajuzu kunufaika naye.

**Kisha mahali pake ni nyumba ya kale**.

Yaani mahali pake pa kuchinjwa ni nyumba ya Mwenyezi Mungu takatifu na makusudio yake ni haram yote ikiwemo Mina. Katika Hadith imeelezwa. Mina yote ni machinjioni.

**Kila umma tumeujaalia mihanga ya ibada.**

Makusudio ya mihanga ya ibada hapa ni kuchinja wanyama kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu, **Ili**

**wamtaje Mwenyezi Mungu katika vile alivyowaruzuku katika wanyama howa**, iliyokuja moja kwa moja. Maana ni kuwa hakuna bid'a (uzushi) katika kuchinja mnyama, ilikuweko katika dini zilizotangulia.

**Basi Mungu wenu ni Mungu mmoja tu.** Kwa hiyo msimtaje mwengine katika dhabihu zenu.

**Kwa hiyo jisalimisheni kwake.** Yaani fuateni amri yake na mumfanyie ikhlasi katika kauli na vitendo.

**Na wabashirie wanyenyekevu, ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hutetemeka, na walio na subira kwa yale yaliyowasibu, na wanaosimamisha Swala na wanatoa katika tulivyowaruzuku.**
Mpe habari njema ya Pepo, ewe Muhammad, yule anayemnyenyekea Mwenyezi Mungu, akamwogopa akawa na uthabiti kwenye dini wakati wa raha na dhiki, akamwabudu bila ya unafiki wala ria na akatoa mali yake katika kumtii Mungu na kutaka radhi yake. Hakuna shaka kwamba mwenye kukusanya sifa hizi atakuwa na daraja ya juu mbele ya Mwenyezi Mungu na ya watu.

وَالْبُدْنَ جَعَلْنَاهَا لَكُمْ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ لَكُمْ فِيهَا خَيْرٌ ۖ فَاذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا صَوَافَّ ۖ فَإِذَا وَجَبَتْ جُنُوبُهَا فَكُلُوا
مِنْهَا وَأَطْعِمُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ ۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرْنَاهَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ {36}

***Na ngamia wa kunona tumewafanyia kuwa ni miongoni mwa nembo za Mwenyezi Mungu, kwao mna kheri. Basi litajeni jina la Mwenyezi Mungu juu yao wanaposimama safu. Na wanapoanguka ubavu, basi kuleni na mlisheni aliyekinai na aombaye. Kama hivyo tumewafanya hawa wawe dhalili kwenu ili mpate kushukuru.***

لَنْ يَنَالَ اللَّهَ لُحُومُهَا وَلَا دِمَاؤُهَا وَلَٰكِنْ يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنْكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَاكُمْ ۗ وَبَشِّرِ
الْمُحْسِنِينَ {37}

***Nyama zao hazimfikii wala damu zao, lakini inamfikia takua kutoka kwenu. Kama hivyo tumewafanya hawa wawe dhalili kwenu ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa alivyowaongoa. Na wabashirie wenye kufanya mema.***

# Aya 36 –37: Ngamia Wanono

## Maana

**Na ngamia wa kunona tumewafanyia kuwa ni miongoni mwa nembo za Mwenyezi Mungu, kwao mna kheri.**

Neno '*Budna'* ni ngamia hasa; kama ilivyoelezwa katika *Tafsiri Razi*, na *Baydhawi.* Hufananishwa naye ng'ombe katika hukumu si katika jina.

Hali yoyote iwayo, mtu ni natija ya mambo mengi, yakiwemo mazingira anayoishi. Waarabu, kwa karne nyingi, wakati wa jahiliya na baadaye, wameishi pamoja na ngamia na alikuwa ni sehemu ya maisha yao; wakila nyama yake, kunywa maziwa yake , kuvaa manyoya yake, kubebea mizigo kutoka mji mmoja hadi mwingine n.k. Tazama Juz. 14 (16: 6).

Kwa ajili hii ndio maana Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akamtaja kwenye Aya kadha, kwa tamko la kiujumla; kama vile wanyama howa, au kwa tamko mahususi; kama ilivyo katika Sura 88 na hii Aya tuliyo nayo.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amewaneemesha waja wake kwa ngamia na akamfanya ana manufaa mengi; yakiwemo kujikurubisha mja kwa Mwenyezi Mungu kwa kumchinja katika nyumba yake takatifu. Kuleta ibara ya nembo kwa dhabihu hii ni kufahamaisha kuwa hiyo ni twaa na ibada bora zaidi.

**Basi litajeni jina la Mwenyezi Mungu juu yao wanaposimama safu.**

Katika masharti ya kuchinja ni kusoma *Bismillah* na kuelekezwa chinjo upande wa Qibla, na ngamia kuwa na aina yake ya kuchinjwa (*nahr*) ambayo ni maalum kwa ngamia:
Anachomwa kisu au kitu chochote chenye ncha kwenye maungio ya shingo na kifua, akiwa ngamia amesimama au kupiga magoti au amelala ubavu, kwa sharti ya kuwa sehemu zote za mbele ya mwili wake zielekee Qibla.

Njia bora ni kumchinja ngamia kwa namna ilivyoelezwa katika Riwaya ambayo ni kusimamishwa ngamia na kufungwa mmoja wa miguu yake ya mbele na asimame mchinjaji kuelekea Qibla vile vile kisha amchome kwenye maungio ya shingo na kifua. Riwaya hii inaweza kufaa kuwa ni tafsiri ya neno 'wanaposimama safu.'
**Na wanapoanguka ubavu,** yaani wanapoanguka chini na kukata roho, **basi kuleni na mlisheni aliyekinai na aombaye.**

Aliyekinai ni yule anayeridhia unachompa bila ya kuomba.**Kama hivyo tumewafanya hawa wawe dhalili kwenu ili mpate kushukuru.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amewafanya wanyama tuwatumie, hata kuwachinja pia. Kwa hiyo ni wajibu wetu kushukuru.

**Nyama zao hazimfikii wala damu zao.**

Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mwenye kujitosha na walimwengu, hawahitajii, sikwambii nyama zilizochinjwa na damu; bali haihitajii chochote. Imesemekana hii ni kuwarudi washirikina ambao walikuwa wakitapakaza damu ya dhabihu kwenye masanamu yao na kuta za Al-Kaaba.

**Lakini inamfikia takua kutoka kwenu.**

Unaweza kuuliza kuwa maana ya takua ni kumcha Mungu katika yale aliyoyaharamisha; ambapo thawabu yake na manufaa yake yanarudi na kumfikia mtendaji tu. Sasa nini maana ya kuwa inafika kwa Mungu?

Jibu: Makusudio ya takua hapa ni kumridhisha Mwenyezi Mungu, na radhi ya Mwenyezi Mungu haiepukani na mwenye takua, zinakwenda sambamba. Kwa hiyo maana ni kinachomfikia Mwenyezi Mungu katika dhabihu zenu ni kule kuridhiwa na Mungu sio kukasirikiwa. Inafanana na kumwambia mwanao: kufaulu kwako darasani kunanifanya ni kupende na kukuridhia, na haya ndiyo ninayoyapata kutokana na masomo na kufaulu kwako.

**Kama hivyo tumewafanya hawa wawe dhalili kwenu ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa alivyowaongoa**.

Amewadhalilisha wanyama kwa waja wake na akawaongoza kujikurubisha kwake kwa kuwachinja ili wamsifu kwa sifa zake njema, wamuad- himishe kwa ujuzi wake na uweza wake, wahofie adhabu yake na kutumai thawabu zake.

**Wabashirie wenye kufanya mema** wote; wawe wamefanya mema kwa kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kuchinja au kwa jambo jinginelo. Kwani aina za wema hazina idadi. Bora zaidi ni kupigana jihadi na madhalimu na wapotevu japokuwa kwa tamko la haki na uadilifu.

{إِنَّ اللَّهَ يُدَافِعُ عَنِ الَّذِينَ آمَنُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٍ كَفُورٍ {38

***Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamini. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila haini, mwenye kukufuru sana.***

{أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَاتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا ۚ وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ {39

***Wameruhusiwa*** (***kupigana***) ***wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa. Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia.***

الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَهُدِّمَتْ صَوَامِعُ
{وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسَاجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا اسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا ۗ وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ {40

***Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila tu kwa kuwa wanasema Mola wetu ni Mwenyezi Mungu. Na lau Mwenyezi Mungu asingeliwakinga watu kwa watu, basi yangelivunjwa mahekalu na makanisa na*** (***sehemu***) ***za kuswalia na misikiti ambayo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi. Na hakika Mwenyezi Mungu humnusuru yule anayemnusuru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mtukufu.***

الَّذِينَ إِنْ مَكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ وَلِلَّهِ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ
41}}

***Wale ambao tukiwamakinisha katika ardhi husimamisha Swala na wakatoa Zaka na wakaamrisha mema na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote.***

# Aya 38 – 41: Mwenyezi Mungu Huwakinga Walioamini

## Maana

**Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamini. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila haini mwenye kukufuru sana.**

Aya hii inafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anazuia ukafiri na utaghuti kwa waumini katika maisha haya na siku ya mwisho. Aya iliyo wazi zaidi katika hilo ni: "Hakika bila shaka tutawanusuru Mitume wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku watakaposimama mashahidi." (40:51).

Pamoja na hayo Mwenyezi Mungu ameashiria kwenye Aya kadhaa, kwamba mayahudi walikuwa wakiwaua manabii bila ya haki. Miongoni mwazo ni: Juz.3 (3: 21), Juz. 4 (3:112, 181) na Juz 6 (4:154). Kuongezea Historia ya mwanadamu, tangu zamani na sasa, imejaa dhulma na kufanyiwa uadui wale wenye takua na ikhlasi.

Sasa je, kuna wajihi wa kukusanya baina ya zinazofahamisha kuuliwa watu wema na zile zinazofahamisha kunusuriwa watu wa haki?

Jibu: Kwanza: Aya za nusra zinawahusu baadhi ya mitume; kama vile: Nuh, Hud, Swaleh, Lut na Muhammad. Hayo yanaashiriwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na Mwenyezi Mungu humuunga mkono kwa nusra yake amtakaye." Juz.3 (3:13).

Na Aya hii tuliyo nayo inafahamisha kuwa Muhammad (s.a.w.) na maswahaba ndio wanokusudiwa kwenye kauli yake 'Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamni.' Kwa sababu wao ndio waliotolewa majumbani mwao si kwa lolote ila ni kwa kuwa wamesema: 'Mola wetu ni Mwenyezi Mungu."

Katika vitabu vya Hadith (*As-sihah*) imeelezwa kwamba Aya hizi zilishuka wakati Mtume alipofanya hijra (kuhama) kutoka Makka kwenda Madina.

Pili: Mwenye haki na ikhlasi hawezi kukosa wa kumuunga mkono na kumsaidia kwa mkono wake, mali

yake au ulimi wake. Wala hatujawahi kusikia jamii ambayo kwa pamoja imekuwa dhidi ya mwenye kutamka tamko la haki na uadilifu.

Ndio, ni kweli kwamba watetezi wa haki wengi wameuawa, wakatekwa na wakafukuzwa, lakini Mwenyezi Mungu anawapa wasaidizi wanotangaza misimamo yao na kuwatukuza na wakiwakabili maadui zao kwa hoja na dalii mkataa. Hii ni aina ya nusra. Kusema kwake Mwenyezi Mungu: 'Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila haini' ni sababu ya kauli yake: 'Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamni.'

Sababu hii inafahamisha kuwa ni wajibu kwa anayemwamini Mwenyezi Mungu kumsaidia mumin kwa kila alichonacho kinachoweza kumsaidia, angalau kumtetea anapotajwa kwa ubaya; vinginevyo atakuwa ni mhaini mwingi wa kukanusha. Kuna Hadith sahih isemayo: " Mwenye kuinyamazia haki ni shetani bubu.

Tatu: Lau ingekuwa mtu akiamini tu, basi anaondokewa na muadui na matatizo, basi wangeliamini watu wote imani ya kibiashara; kama vile anayeiuza dhamiri yake kwa kila mwenye kutoa thamani.

Nne: Imani ya haki ni kumtii Mwenyezi Mungu katika maamrisho yake na hukumu zake zote. Na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ametuamrisha, tukitaka kufanya jambo, tufuate sababu za kimaumbile ambazo amezifanya zitekeleze matakwa yetu. Ameziweka sababu za ushindi kuwa ni umoja na kuandaa nguvu, akasema: "Wala msizozane, msije mkavunjika moyo na zikapotea nguvu zenu." Na akasema: "Na waandalieni nguvu vile muwezavyo." Juz. 10 (8: 46, 60).

Katika *Futuhatul-Mkkiya*, Ibnul A'arabiy ameziletea sababu hizi ibara ya mkono wa Mungu. Ameichukua ibara hii katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Je, hawaoni kwamba tumewaumbia kutokana na iliyofanya mikono yetu wanyama wa mifugo wakawa wenye kuwamiliki." (36:71). Tazama maelezo kwa anuani ya 'Dini haioteshi ngano' katika Juz.3 (8: 1-4).

**Wameruhusiwa (kupigana) wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa. Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia.**

Waislamu kule Makka walikuwa ni wanyonge, wakipata kila aina ya maudhi na ukandamizwaji kutoka kwa washirikina; na walikuwa hawawezi kujitetetea. Walikuwa wakimjia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) na wakimshitakia dhulma, naye akiwa hana lolote la kuwaambia isipokuwa kuwausia subra. Miongoni mwa aliyokuwa akiwaambia ni: "Mimi sijaamriwa kupigana."

Mtume alikatazwa kupigana na washirikina katika zaidi ya Aya 70, alipokuwa Makka. kwa sababu kupigana wakati huo ilikuwa ni sawa na kujimaliza. Tazama Juz.5 (4:77).

Baada ya Mtume na Waislamu kuhamia Madina, wakawa na nguvu, ndipo ikashuka Aya hii. Inasemekana kuwa ndio Aya ya kwanza kushuka kuhu- siana na vita.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amebainisha sababu ya kutoa ruhusa hii; kwamba washirikina

wamewachokoza waislamu, wakawatoa kwenye miji yao kwa dhulma na kwa uadui na akawaahidi waislamu ushindi kwa maadui zao, pale aliposema: "Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia."

**Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema Mola wetu ni Mwenyezi Mungu**.

Dhahiri ya Aya inaonyesha kuwa kosa pekee la Mtume na swahaba zake kwa washirikina ni kule kusema: "Hakuna Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu." Dhahiri hii ndio walioichukua wafasiri wote; bali mmoja wa wafasiri wapya alisema, ninamnukuu: "Hakuna upinzani kuliko kupinga maisha haya yaliyojikita kwenye tamaa, kupingana masilahi, kutofautiana mielekeo na kugongana matamanio."

Mara nyingi tumeashiria huko nyuma kwamba utaghuti wa kishirikina uli– upiga vita ujumbe wa Muhammad na neno la Tawhid si kwa lolote isipokuwa linataka kuondoa manufaa, matamanio, masilahi yao na kuwe– ka usawa baina ya watu. Angalia tuliyoyaandika kwa anuani ya 'Masilahi ndio sababu' katika Juz. 1 (2: 92–96).

**Na lau Mwenyezi Mungu asingeliwakinga watu kwa watu, basi yangelivunjwa mahekalu na makanisa na (sehemu) za kuswalia na misikiti ambayo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi**.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kuwaruhusu waumini, wanaochokozwa, kupigana na washirikina, sasa anabainisha sababu ya ruhusa hiyo; kwamba lau si kuweko na nguvu ya upinzani, basi ingeenea vurugu na ufisadi katika ardhi kwa sababu ya unyang'nyi, uporaji na kumwagika damu; hasa baina ya vikundi na watu wa dini.

Mwenyezi Mungu ameielezea fitna baina ya mataifa kwa ibara ya kuvunjwa sehemu zake za kuabudu. Kwa sababu ndio sehemu muhimu kwa mataifa; na zina alama maalum zinazotofautiana na nyingine. Mahekalu ni ya mayahudi, makanisa ni ya wanaswara (wakiristo), na sehemu za kuswalia ni zamataifa mengineyo. Msikiti unatofautiana na sehemu nyingine kwa kuwa Swala humo ni mara tano, usiku na mchana.
Kundi la wafasiri wamesema kuwa makusudio ya Aya ni kuwa Mwenyezi Mungu anawazuwiya waumini na makafiri. Kama itakuwa ni sawa tafsiri hiyo, haiwezi kufaa kila wakati. Usahihi hasa ni tuliouelezea, kuwa ili kuhifadhika amani na nidhamu ni lazima kuweko na nguvu ya upinzani; ni sawa nguvu hiyo iwe mikononi mwa waumini au makafiri.

Imam Ali (a.s.) anasema: "Hapana budi watu wawe na kiongozi mwema au muovu, atatumiwa na mumin na kafiri, Mwenyezi Mungu atafikisha kwaye muda. Watu watajikusanya kwake waweze kumpiga adui, nia zitakuwa na amani kwaye, mwenye nguvu atakamatwa kwa ajili ya kumuonea mnyonge ili astarehe na kila muovu."

Kauli hii ya Imam Ali, ilikuwa ni kuwarudi Khawariji waliposema: "Hakuna hukumu isipokuwa ya

Mwenyezi Mungu." Angalia tuliyoyaandika kwa anuani hii, kwenye Juz. 12 (12:40).

**Na hakika Mwenyezi Mungu humnusuru yule anayemnusuru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mtukufu.**

Hiki ni kichocheo cha kupigana jihadi ya kuinusuru haki na watu wake.

**Wale ambao tukiwamakinisha katika ardhi husimamisha Swala na wakatoa Zaka na wakaamrisha mema na wakakataza mabaya.**

Makusudio ya kumakinishwa hapa ni utawala. Mwenyezi Mungu ameapa kwa msisitizo kwamba Yeye atawasaidia watawala, kwa sharti ya kuweko mambo mawili:

Kwanza, wao wenyewe watekeleze haki ya ibada kwa ukamilifu; kama vile Swala, Saumu na kuamrisha mema na kukataza maovu. Ibada ya kimwili ameileta kwa ibara ya Swala na ibada ya kimali kwa Zaka.

Jambo la pili, ni kufanya uadilifu baina ya watu, kuisimamisha haki na kuibatilisha batili. Hayo ndio makusudio ya kuamrisha mema na kukataza maovu. Akivunja moja tu ya mawili haya, Mwenyezi Mungu humpuuza na humwacha.

Unaweza kuuliza: Tumewaona watawala wengi wasiomwamini Mungu kabisa, sikwambii kumwabudu kwa kuswali na kutoa Zaka, lakini pamoja na hayo utawala wao umestawi na kufuatwa na raia kwa vile wametimiza malengo ya raia na kuwatumikia, wala raia hawaangalii imani yao. Kwa hiyo, inaonyesha, suala la imani sio sharti la kudumu utawala na ustawi wake?

Jibu: Makusudio ya nusra ya Mwenyezi Mungu, katika Aya, ni kuustawisha utawala katika dunia na thawabu za akhera; bali hii ndio nusra ya kiuhakika. Kwa sababu ufalme wa dunia unaondoka, lakini neema za akhera ni za kudumu bila ya kuwa na ukomo na ni msafi na wa raha kwa pande zake zote. Mtawala wa dunia anaweza kuustawisha utawala wake duniani akiwa mwadilifu, lakini Akhera akapata adhabu ya kuungua kwa kukufuru kwake dalili za kilimwengu ambazo zinaonyesha kuweko mtengenezaji.

**Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote.**

Yeye peke yake ndio Mfalme wa wafalme, huumpa ufalme amtakaye na humnyima ufalme amtakaye, na yeye ni Muweza wa kila kitu.

{وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَعَادٌ وَثَمُودُ {42

***Wakikukadhibisha, basi wamekadhibisha kabla yao kaumu ya Nuh na kina A'd na Thamud.***

{وَقَوْمُ إِبْرَاهِيمَ وَقَوْمُ لُوطٍ {43

*Na kaumu ya Ibrahim na kaumu ya Lut.*

{وَأَصْحَابُ مَدْيَنَ ۖ وَكُذِّبَ مُوسَىٰ فَأَمْلَيْتُ لِلْكَافِرِينَ ثُمَّ أَخَذْتُهُمْ ۖ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ}44

*Na watu wa Madyan na Musa alikadhibishwa. Nikawapa muda makafiri kisha nikawatia mkononi, basi kulikuwaje kukanya kwangu?*

{فَكَأَيِّنْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ فَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَبِئْرٍ مُعَطَّلَةٍ وَقَصْرٍ مَشِيدٍ}45

*Na miji mingapi tuliyoiangamiza iliyokuwa ikidhulumu. Ikaangukiana mapaa yake na visima vilivyoachwa na makasri yaliyo madhubuti?*

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَتَكُونَ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا أَوْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا ۖ فَإِنَّهَا لَا تَعْمَى الْأَبْصَارُ وَلَٰكِنْ تَعْمَى
{الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ}46

*Je, hawatembei katika ardhi ili wapate akili za kuzingatia na masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayopofuka, lakini zinazopofuka ni nyoyo zilizomo vifuani.*

{وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَلَنْ يُخْلِفَ اللَّهُ وَعْدَهُ ۚ وَإِنَّ يَوْمًا عِنْدَ رَبِّكَ كَأَلْفِ سَنَةٍ مِمَّا تَعُدُّونَ}47

*Wanakuharakisha ulete adhabu na hakika Mwenyezi Mungu hakhalifu miadi yake. Na hakika siku moja kwa Mola wako ni kama miaka elfu mnavyohisabu.*

{وَكَأَيِّنْ مِنْ قَرْيَةٍ أَمْلَيْتُ لَهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ ثُمَّ أَخَذْتُهَا وَإِلَيَّ الْمَصِيرُ}48

*Ni miji mingapi nimeipa muda na hali ilikuwa imedhu- lumu, kisha nikaitia mkononi? Na kwangu mimi ndio marejeo yote.*

{قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّمَا أَنَا لَكُمْ نَذِيرٌ مُبِينٌ}49

*Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni muonyaji kwenu niliye dhahiri.*

{فَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ}50

*Basi wale ambao wameamini na wakatenda mema, watapata maghufira na riziki za heshima.*

{وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي آيَاتِنَا مُعَاجِزِينَ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ }51

***Na wanaojitahidi kuzipinga Aya zetu hao ndio watu wa motoni***

# Aya 42 –51: Wakikukadhabisha

## Maana

**Wakikukadhibisha, basi wamekadhibisha kabla yao kaumu ya Nuh na kina A'd na Thamud na kaumu ya Ibrahim na kaumu ya Lut na watu wa Madyan na Musa alikadhibishwa.**

Makuraishi walimkadhibisha Muhammad (s.a.w.) na wakamtoa nyumbani kwake, Mwenyezi Mungu akamwambia Mtume wake, kwa kumtuliza na kumpoza moyo, kwamba hakuna la ajabu katika yanayokutokea. Kila Nabii alipambana na hayo uliyopamabana nayo.

Kisha akamtajia idadi ya manabii, kwa njia ya mfano tu; akiwemo Hud na watu wake walioitwa A'd, Swaleh na watu wake walioitwa Thamud. Ama watu wa Madyana hao ni watu wa Shuayb. Umetangulia mfano wake katika Juz. 7 (6:34).

**Nikawapa muda makafiri kisha nikawatia mkononi, basi kulikuwaje kukanya kwangu?**

Makusudio ya kukanya hapa ni adhabu, kwa maana ya kukanya kwa vitendo sio kwa maneno. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliwacheleweshea makafiri adhabu mpaka ulipofika muda wake, akawapatiliza kwa upatilizo wa mwenye uweza asiyeshindwa. Aya inaashiria kwamba mwenye akili hatakikani kuharakisha mambo kabla ya kufikia muda wake.

**Na miji mingapai tuliyoiangamiza iliyokuwa ikidhulumu.**

Baada ya Mwenyezi Mungu kusema kuwa anawapa muda makafiri mpaka wakati maalum, sasa anaishiria kuangamia kwa miji ambayo watu wake wamedhulumu, ambayo ni mingi, kama inavyoashiria kauli yake: 'Miji mingapi?' Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 (7:4).

**Ikaangukiana mapaa yake?**

Umetangulia mfano wake katika Juz. 3 (2:259) na Juz. 15 (18:42).

**Na visima vilivyoachwa na makasri yaliyo madhubuti.**

Yote haya yameachwa bila watu; yaani miji ya madhalimu imekuwa mahame, haina watu, ambapo hapo zamani ilikuwa imesheheni wenyeji na wageni wanaoitembelea.

**Je, hawatemebei katika ardhi ili wapate akili za kuzingatia na masikio ya kusikilia?**

Wanaambiwa wale waliomkadhibisha Muhammad (s.a.w.). Yaani hawapati funzo kwa waliyowafikia wakadhibishaji na kuona jinsi miji yao ilivyokuwa mitupu? Umetangulia mfano wake katika Juz. 4 (3:137) na Juz. 14 (16: 36).

**Kwani hakika si macho yanayopofuka, lakini zinazopofuka ni nyoyo zilizomo vifuani**.

Kuna faida gani ya kusikia na kuona ikiwa moyo umepofuka? Kwa sababu masikio na macho ni nyenzo na akili ndio asili.

**Wanakuharakisha ulete adhabu**.

Wanaohimiza ni washirikana na anayehimizwa ni Muhammad (s.a.w.). Mtume alikuwa akiwapa kiaga cha adhabu ikiwa watang'ang'ania ushirikina.

Walikuwa wakisema yale waliyosema waliowatangulia kuwaambia mitume kila wanapowakataza ushirikina: "Tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni mkweli."

**Na hakika Mwenyezi Mungu hakhalifu miadi yake**.

Kuharakisha au kuchelewesha si muhimu madamu ahadi itakuwa. Kuwa hakika ni kuwa ahadi ya Mwenyezi Mungu kuwapa thawabu watiifu ni haki ya wale watiifu, hawezi kuihalifu.

Ama ahadi yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ya adhabu kwa waasi, hiyo ni haki yake Mwenyezi Mungu, akitaka anaweza kuitekeleza na akipenda anaweza kusamehe, ila ikiwa imetanguliwa na neno 'Hatahalifu' kama ilivyo katika Aya hii tuliyo nayo; ambapo amekanusha kutotekeleza aliyowaahidi makuraishi kutokana na msimamo wao kwa Mtume wa rehema.

**Na hakika siku moja kwa Mola wako ni kama miaka elfu mnavyohis- abu**.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anawaambia washirikina; kuna haja gani ya kuharakisha adhabu ya Akhera na siku moja kwake ni kali kwenu kuliko adhabu ya miaka elfu katika miaka ya kiduniani? Kwa ufupi ni kuwa miaka elfu ni fumbo la vituko vya siku ya mwisho.

**Ni miji mingapi nimeipa muda na hali ilikuwa imedhulumu, kisha nikaitia mkononi? Na kwangu mimi ndio marejeo yote**.

Umetangulia mfano wake katika Juzuu hii na Sura hii tuliyo nayo Aya 45 na pia sehemu hii tuliyo nayo. Mwenyezi Mungu amerudia kwa kusisitiza na kutoa hadhari.

**Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni muonyaji kwenu niliye dhahiri**.

Huu ndio umuhimu wa mitume, kufikisha ujumbe na kutoa onyo kwa yule mwenye kuupinga. Maana haya yamekaririka kwa mifumo mbalimbali.

**Basi wale ambao wameamini na wakatenda mema, watapata maghufira na riziki za heshima.**

Maana yako wazi, na yametangulia kwenye Aya kadha, ikiwemo Juz. 1 (2:25).

**Na wanaojitahidi kuzipinga Aya zetu hao ndio watu wa motoni.**

Yaani washirikina wataingia motoni kwa muda usiokuwa na ukomo kwa sababu ya kumfanyia inadi Mtume na kujitahidi kumpinga kufikisha ujumbe wa Mola wake na kuwazuilia nao watu.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ وَلَا نَبِيٍّ إِلَّا إِذَا تَمَنَّىٰ أَلْقَى الشَّيْطَانُ فِي أُمْنِيَّتِهِ فَيَنْسَخُ اللَّهُ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ ثُمَّ يُحْكِمُ اللَّهُ آيَاتِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ {52}

***Na hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii anaposoma ila shetani hutumbukiza katika masomo yake. Lakini Mwenyezi Mungu huyaondoa anayoyatumbukiza shetani; kisha Mwenyezi Mungu huzi- makinisha Aya zake na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, mwenye hekima.***

لِيَجْعَلَ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ فِتْنَةً لِلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ وَالْقَاسِيَةِ قُلُوبُهُمْ ۗ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ {53}

***Ili alifanye lile alilolitumbu iza shetani ni mtihani kwa wale wenye maradhi katika nyoyo zao na wale ambao nyoyo zao zimesusuwaa. Na hakika madhalimu wamo katika uasi wa mbali.***

وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَيُؤْمِنُوا بِهِ فَتُخْبِتَ لَهُ قُلُوبُهُمْ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَهَادِ الَّذِينَ آمَنُوا إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ {54}

***Ili wajue wale ambao wamepewa elimu kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wako na zinyenyekee kwake nyoyo zao. Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye awaongozaye wale ambao wameamini kwenye njia iliyonyooka.***

وَلَا يَزَالُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي مِرْيَةٍ مِنْهُ حَتَّىٰ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً أَوْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابُ يَوْمٍ عَقِيمٍ {55}

***Na wale ambao wamekufuru hawataacha kuwa katika wasiwasi katika hilo mpaka saa iwafikie ghafla au iwafikie adhabu ya siku tasa.***

الْمُلْكُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ ۚ فَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ {56}

***Ufalme siku hiyo ni wa Mwenyezi Mungu. Atahukumu baina yao. Basi wale ambao wameamini na wakatenda mema, watakuwa katika Bustani zenye neema.***

{وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَأُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُهِينٌ {57

***Na wale ambao wamekufuru na wakazikadhibisha ishara zetu watapata adhabu ifedheheshayo.***

# Aya 52 –57: Kusoma Kwa Mtume Na Kujiingiza Shetani

## Maana

**Na hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii anaposoma ila shetani hutumbukiza katika masomo yake.**

Wametofautiana wafasiri kuhusu neno Nabii na Mtume, (*Nabiy* na *Rasul*)[1] kuwa je, ni ibara zenye maana moja au kila moja ina maana yake?

Kauli iliyo karibu zaidi ni ile isemayo kuwa hakuna tofauti baina yake; kwa vile kila mmoja kati yao anatanabahishwa na Mwenyezi Mungu kwa lile analolitaka. Kwa hiyo akitanabahishwa na kuamrishwa kufikisha yale aliyotanabahishwa, huyo anaitwa Nabii kwa sababu Mwenyezi Mungu amemtanabahisha na pia anaitwa Mtume kwa sababu Mwenyezi Mungu amemtumma kufikisha.

Ikiwa amemtanabahisha tu bila ya kumwamuru kufikisha, basi huyo atakuwa ni Nabii tu. Hiyo ni kusema kuwa kila Mtume ni Nabii, lakini sio kila Nabii ni Mtume.

Kuna riwaya inayosema kuwa sababu ya kushuka Aya hii ni kwamba Mtume (s.a.w.) aliwasomea makuraishi Sura Najm, alipofikia kwenye Aya isemayo:

{أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ {19

{وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ {20

***"Je, mmewaona Lata na Uzza na Manata mwingine wa tatu"*** (***53: 19 – 20***)

basi shetani aliingiza katika kisomo cha Mtume maneno haya: "Hao ni wazuri watukufu na kwamba maombezi yao bila shaka yanatarajiwa," yani haya masanamu ni mazuri na uombezi wao unatarajiwa kwa Mwenyezi Mungu.

Maulama wahakiki wamekanusha riwaya hii na wakakata kauli kuwa hiyo ni miongoni mwa uzushi wa wazandiki wanaotaka kukitia ila Kitabu cha Mwenyezi Mungu na utume wa Muhammad (s.a.w.).

Wametegemea, katika hilo, kwenye dalili mkataa za kiakili na kinakili. Mtume ambaye ametumwa na Mwenyezi Mungu kupiga vita ushirikina na kuabudu mizimu, halafu huyo huyo arudi kuisifia kwa sifa za ukamilifu! Vipi iwe hivyo na ulimi wa Mtume unamtarjumu na kumbainisha Mwenyezi Mungu? Shetani anaweza kupata nafasi kwenye ubainifu na tafsiri hii ya kimungu?

Usahihi wa maana ya Aya ni kuwa ukomo wa usomaji wa Mtume yeyote, ni kuwafahamisha watu uhakika wa risala yake ili waweze kuifahamu na kuongoka nayo, lakini wenye tamaa wanaingilia kati kwa kuvungavunga na kueneza kila aina ya propaganda.

Haya tumeyashuhudia na kuyaona hasa. Haya ndio maana ya kutumbukiza shetani katika usomi wa Nabii. Nabii anawatakia heri watu na shetani muharibifu anawazuia wasiipate.

**Lakini Mwenyezi Mungu huyaondoa anayoyatumbukiza shetani; kisha Mwenyezi Mungu huzimakinisha Aya zake na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, mwenye hekima.**

Wabatilifu wanaunda njama na kuzitangaza, lakini Mwenyezi Mungu huondoa ubatilifu wao na kuufedhehi uwongo wao kwenye ndimi za wakweli na mikononi mwa wapigania jihadi. Aya nyingine yenye maana hii ni ile isemayo:

{يُرِيدُونَ أَنْ يُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَيَأْبَى اللَّهُ إِلَّا أَنْ يُتِمَّ نُورَهُ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ {32

***"Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywavyao. Na Mwenyezi Mungu amekataa isipokuwa kuitimiza nuru yake, ijapokuwa makafiri wamechukia." Juz. 10 (9:32).***

**Ili alifanye lile alilolitumbukiza shetani ni mtihani kwa wale wenye maradhi katika nyoyo zao na wale ambao nyoyo zao zimesusuwaa.**

Wenye maradhi katika nyoyo ni wezi wanaoishi kwa unyang'anyi, uporaji, ghushi na utapeli. Ama waliosusuwaa nyoyo zao ni wale ambao ni bendera hufuata upepo. Maana ni kuwa kampeni za uwongo hazina nafasi isipokuwa kwa wezi na walio na bendera.

Popote utakapoelekea utakuta picha hii waziwazi; hasa kwenye magazeti, idhaa, vitabu, michezo ya kuigiza na katika mazungumzo ya vibaraka na wale wanaodanganywa ambao wanaamini kila wanayoambiwa bila ya kuchunguza; tena ni wengi.

Kisha kampeni za uwongo, hata kama zitakuwa zina madhara kwa upande fulani, lakini zina manufaa kwa upande mwingine. Kwa sababu zinamtambulisha muhaini na mwenye ikhlasi, vile vile mjinga na mjuzi. Haya ndio makusudio ya neno mtihani.

**Na hakika madhalimu wamo katika uasi wa mbali.**

Kila mwenye kuvungavunga na akafanya uzushi basi ni dhalimu, na kila mwenye kuusadikisha uwongo na uzushi bila ya kuuchuunguza pia huyo ni dhalimu.

**Ili wajue wale ambao wamepewa elimu kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wako na zinyenyekee kwake nyoyo zao.**

Neno 'hiyo' hapa ni hiyo Qur'an. Pia inaweza kufasirika 'huyo' kwa maana ya huyo Nabii. Maana ni kuwa, ikiwa mtu atasadikisha uwongo juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi wenye maarifa na ikhlasi, wanajua hakika ya uwongo na uzushi huo; jambo ambalo linawazidishia imani na mshikamano kwa Mwenyezi Mungu, mitume yake na vitabu vyake na pia unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu.

**Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye awaongozaye wale ambao wameamini kwenye njia iliyonyooka.**

Anawaongoza Mwenyezi Mungu kwenye njia yake na kuifuata kwa kujikurubisha kwake hata kukiwa na kampeni za uwongo na vikwazo kiasi gani.

**Na wale ambao wamekufuru hawataacha kuwa katika wasiwasi kati- ka hilo mpaka saa iwafikie ghafla au iwafikie adhabu ya siku tasa.**

Makusudio ya saa ni ile saa ya kutoka watu kuelekea kwa Mola wao wakitokea makaburini (Kiyama). Siku tasa ni siku ya hisabu. Utasa ni kinaya cha makafiri kukata tamaa ya kuokoka.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kueleza, katika Aya iliyotangulia, kuwa wenye elimu wanaamini Qur'an na utume wa Muhammad (s.a.w.), kwenye Aya hii anasema kuwa makafiri wako katika shaka kuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu na watendelea kuwa katika shaka hiyo mpaka siku ya kufufuliwa kwao makaburini au siku ya kusimama kwao mbele ya Mwenyezi Mungu kwa hisabu.

Na hapo ndipo itawafichukia hakika yao na watajua kuwa wao walikuwa kwenye upotevu.

**Ufalme siku hiyo ni wa Mwenyezi Mungu** peke yake, hakuna kadhi au amiri wala raisi au waziri; kama ilivyo katika maisha haya ya duniani. **Atahukumu baina yao.** Yaani baina ya makafiri na waumini.

**Basi wale ambao wameamini na wakatenda mema, watakuwa katika Bustani zenye neema. Na wale ambao wamekufuru na wakazikadhibisha ishara zetu watapata adhabu ifedheheshayo.**

Hawa watapata hizaya na moto na wale watapata Pepo na raha. Mfano wa Aya hizi umekwishatangulia mara nyingi.

{وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ قُتِلُوا أَوْ مَاتُوا لَيَرْزُقَنَّهُمُ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا ۚ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ {58

***Wale ambao wamehajiri katika njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakuawa au wakafa, bila shaka***

*Mwenyezi Mungu atawaruzuku riziki njema. Na hakika Mwenyezi Mungu ni mbora wa wanaoruzuku.*

{لَيُدْخِلَنَّهُمْ مُدْخَلًا يَرْضَوْنَهُ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَعَلِيمٌ حَلِيمٌ {59

*Bila shaka atawaingiza mahali watakapoparidhia, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mpole.*

{ذَٰلِكَ وَمَنْ عَاقَبَ بِمِثْلِ مَا عُوقِبَ بِهِ ثُمَّ بُغِيَ عَلَيْهِ لَيَنْصُرَنَّهُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَعَفُوٌّ غَفُورٌ {60

*Ndivyo hivyo. Na anayelipiza mfano wa alivyoadhibiwa, kisha akadhulumiwa, bila shaka Mwenyezi Mungu atamnusuru. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa maghufira.*

{ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَأَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ {61

*Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu huuingiza mchana katika usiku na huuingiza usiku katika mchana na kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, mwenye kuona.*

{ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ {62

*Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye wa kweli, na kwamba wale wanaowaomba badala yake ni batili, na hakika Mwenyzi Mungu ndiye aliye juu, Mkubwa.*

{أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَتُصْبِحُ الْأَرْضُ مُخْضَرَّةً ۗ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ {63

*Je huoni kwamba Mwenyezi Mungu huteremsha maji kutoka mbinguni na mara ardhi inakuwa chanikiwiti. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mwenye habari.*

{لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ {64

*Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kujitosha, Mwenye kusifiwa.*

1. Neno nabiy linamaana ya kutanabaishwa na rasul lina maana ya kutumwa – Mtarjumu.

# Aya 58 – 64: Waliohajiri

## Maana

**Wale ambao wamehajiri katika njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakuawa au wakafa, bila shaka Mwenyezi Mungu atawaruzuku riziki njema. Na hakika Mwenyezi Mungu ni mbora wa wanaoruzuku.**

Hijra (kuhama) katika njia ya Mwenyezi Mungu ziko aina nyingi. Miongoni mwazo ni hizi zifuatazo:-

● Kuhama mtu kwao kwenda kupigana jihadi na madhalimu na wapotevu.

● Kukimbia mtu na dini yake kuepuka vikwazo vya kumzuia kutekeleza wajibu wake.

● Kuhama kwa ajili ya kutafuta elimu ya dini kwa ajili ya dini, kutafuta riziki halali au kutekeleza faradhi ya Hijja.

Yeyote miongoni mwa hawa na mfano wao, akiuawa au akifa katika kuhama kwake huko, basi atastahiki, mbele ya Mwenyezi Mungu, kupata malipo na riziki njema, kama wanavyostahiki mashahidi. Tumezungumzia Hijra kwa ufafanuzi zaidi katika Juz. 4 (3: (190 -195) na Juz.5 (97-100).
**Bila shaka atawaingiza mahali watakapoparidhia, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mpole.**

Makusudio ya mahali hapa ni Peponi. Kwa dhahiri ni kuwa mwenye kuiingia hataridhia pengine zaidi ya hapo.

**Ndivyo hivyo.**

Yaani hivyo alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kwamba mwenye kuhama katika njia yake na akuawa au akafa, kuwa atapata yanayomrid- hisha kutoka kwa kwa Mola wake.

**Na anayelipiza mfano wa alivyoadhibiwa,** yaani mwenye kupigana kujikinga. **Kisha akadhulumiwa,** si kwa lolote isipokuwa amekataa kudhulumiwa na kuchokozwa, **bila shaka Mwenyezi Mungu atamnusuru.** Yaani Mwenyezi Mungu atamsaidia mwenye kudhulumiwa na atamlipizia kisasi.

**Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa maghufira.**

Hapa kuna ishara kuwa msamaha kwa mkosaji ni jambo linalopendeza kwa Mwenyezi Mungu ikiwa mtu amemkosea Mwenyezi Mungu hasa, lakini haki ya umma haina msamaha.

**Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu huuingiza mchana katika usiku na huuingiza usiku katika mchana na kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, mwenye kuona.**

Umetangulia mfano wake katika Juz. 3 (3:27).

Wafasiri wametaja njia nyingi za kuunganisha Aya hii na iliyo kabla yake, lakini hawakuleta jambo la kutuliza moyo. Katika utangulizi wa Juzuu ya kwanza tulidokeza kwamba Qur'an si kitabu cha fani cha kuwa na milango maalumu ya maudhui; isipokuwa ni kitabu cha uongofu na mawaidha.

Kinakugurisha kutoka jambo hili hadi jingine. Imam Ali (a.s.) anasema: "Hakika Aya inakuwa na jambo mwanzoni mwake na mwisho wake inakuwa na jambo jingine."

**Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye wa kweli, na kwamba wale wanaowaomba badala yake ni batili, na hakika Mwenyzi Mungu ndiye aliye juu, Mkubwa.**

Mwenyezi Mungu ni haki kwa kudumu dhati yake na utukufu wa sifa zake, Yuko juu kwa vile hakuna mtawala zaidi ya utawala wake na ni Mkubwa ambaye amekienea kila kitu kiujuzi na kihuruma.

Makusudio ya kutaja sifa zote ni kuwa Mwenyezi Mungu huwanusuru wenye takua na huwafedhehesha wale waliokufuru na kufanya ufisadi ardhini.

**Je huoni kwamba Mwenyezi Mungu huteremsha maji kutoka mbinguni na mara ardhi inakuwa chanikiwiti. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mwenye habari.**

Umetangulia mfano wake katika Aya ya 5 ya Sura hii na pia kwenye Juz.2 (2: 164).

**Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kujitosha, Mwenye kusifiwa.**

Hahitajii walimwengu na ni msifiwa wa wanaosifiwa. Katika *Najul-bal-agha* imesemwa: "Yeye ni mwenye kujitosha bila ya kutaka kufaidika," yaani kwamba utajiri wake ni wa kidhati sio wa kunasibishwa na kwamba yeye lau angelihitajia kitu asingelikuwa ni Mungu. Ibn Al-Arabi anasema, katika kitabu *Futuhatul-makkiyya:*

"Hakuna wa kusifiwa isipokuwa anayesifiwa na mwenye sifa." Yaani Mwenyezi Mungu ndiye mwenye sifa; kwamba hakuna mwenye kustahiki sifa ila aliyesifiwa na Mungu au kuridhia asifiwe."

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ وَالْفُلْكَ تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ وَيُمْسِكُ السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ {65}

***Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu amewadhalilishia vilivyomo ardhini na majahazi yapitayo baharini kwa amri zake. Na anazizuia mbingu zisianguke juu ya ardhi isipokuwa kwa idhini yake. Hakika Mwenyezi Mungu kwa watu ni Mpole, Mwenye kurehemu.***

وَهُوَ الَّذِي أَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ۗ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ {66}

***Naye ndiye ambaye amewahuisha kisha atawafisha kisha atawahuisha. Hakika mtu ni mwenye kukufuru sana.***

{لِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا هُمْ نَاسِكُوهُ ۖ فَلَا يُنَازِعُنَّكَ فِي الْأَمْرِ ۚ وَادْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ ۖ إِنَّكَ لَعَلَىٰ هُدًى مُسْتَقِيمٍ {67

***Kila umma tumeujalia sharia wanazozifuata. Basi wasizozane nawe katika jambo hili. Na lingania kwa Mola wako; hakika wewe uko katika uongofu ulionyooka.***

{وَإِنْ جَادَلُوكَ فَقُلِ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ {68

***Na wakikujadili, basi sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi mnayoyatenda.***

{اللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ {69

***Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu siku ya Kiyama katika hayo mnayohitilafiana.***

{أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ {70

***Je, hujui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na ardhini? Hakika hayo yamo kitabuni. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.***

# Aya 65 – 70: Anazuia Mbingu

## Maana

**Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu amewadhalilishia vilivyomo ardhini na majahazi yapitayo baharini kwa amri zake.** Umetangulia mfano wake katika Juz. 13 (14: 32) na Juz. 14 (16: 14).

**Na anazizuia mbingu zisianguke juu ya ardhi isipokuwa kwa idhini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye huruma kwa watu.**

Mwenyezi Mungu amezizuia kwa 'nguvu ya mvutano'; kama anavyowazuia ndege kwa mbawa zao. Ametegemeza kwake Mwenyezi Mungu kuzuia, kwa sababu yeye ndiye muumba wa ulimwengu na msababishaji wa sababu. Katika baadhi ya Aya, Mwenyezi Mungu, ameleta ibara ya sababu hizo kwa neno, mikononi mwa Mwenyezi Mungu; kama vile:

{أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا خَلَقْنَا لَهُمْ مِمَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَامًا فَهُمْ لَهَا مَالِكُونَ {71

***“Je, hawaoni kuwa tumewaumbia katika vile ilivyofanya mikono yetu, wanyama nao wanawamiliki”* (*36:71*)**

{قَالَ يَا إِبْلِيسُ مَا مَنَعَكَ أَنْ تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ ۖ {75

***“Akasema tena: Ewe Iblis! Ni kipi kilichokuzuia kumsujudia yule niliyemuumba kwa mikono yangu?”* (*38:75*).**

Kwa vyovyote iwavyo ni kwamba lengo la kauli yake Mwenyezi Mungu: ‘Na anazizuia mbingu…’ ni kuashiria kwamba ni lazima mtu afikirie sana katika kuumbwa ulimwengu, na jinsi Mwenyezi Mungu alivyoupangilia kwa uweza wake na hekima yake. Lau si hekima na mpangilio huu, ulimwengu ungeliharibika na sayari zote zingekuwa bure tu.

**Naye ndiye ambaye amewahuisha kisha atawafisha kisha atawahuisha. Hakika mtu ni mwenye kukufuru sana.**

Umepita mfano wake katika Juz. 1 (2: 28) kifungu cha ‘Mauti na uhai mara mbili.’ Ama wasifu wa mtu kuwa ni mwenye kukufuru sana, dhalimu sana, mwenye kujifaharisha sana n.k. sio kuwa ni kuelezea hakika yake yote ilivyo, isipokuwa ni kutafsiri silika yake katika baadhi ya misimamo yake. Angalia Juz.12 (11:9).

**Kila umma tumeujalia sharia wanazozifuata.**

Makusudio ya umma ni watu wa dini. Neno sharia tumelifasiri kutokana na neno *mansaka*, ambalo lina maana mbalimbali; miongoni mwazo ni: Mnyama anayechinjwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kama ilivyo katika Aya 34 ya Sura hii tuliyo nayo.

Maana nyingine ni mahali pa ibada. Pia lina maana ya sharia na njia, ambayo ndiyo yaliyokusudiwa hapa, kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu iliyokuja moja kwa moja baada ya neno hilo:

**Basi wasizozane nawe katika jambo hili.**

Yaani maadamu kila watu wa dini wana sharia zao na njia wanzozifuata, basi watu wa dini nyingine wasikuletee mzozo kwenye Uislamu na sharia yake. Sharia ya Tawrat na inajili ni kwa ajili ya waliopita, lakini sharia ya Qur’an ni kwa ajili ya watu wa sasa na watakaofuatia hadi siku ya ufufuo.

**Na lingania kwa Mola wako** wala usijishughulishe na upinzani wa wapinzani wala mizozo.

**Hakika wewe uko katika uongofu ulionyooka.**

Na atakayefuata muongozo wako hatapotea wala kuwa muovu.

**Na wakikujadili, basi sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi mnayoyatenda. Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu siku ya Kiyama kati- ka hayo mnayohitilafiana.**

Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume wake aendelee na mwito wake, aachane nao wenye mizozo na inadi na awaambie kuwa Mwenyezi Mungu anajua matendo yetu na yenu na yupi aliyeongoka kati yetu sisi na nyinyi. Na Yeye ndiye hakimu siku ya hukumu. Huko mtajua ni yupi mwenye haki na mwenye batili.

**Je, hujui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na ardhini? Hakika hayo yamo kitabuni.**

Maneno yanaelekezwa kwa Mtume (s.a.w.). Makusudio ni kuwakemea makafiri kwamba waliyoyasema na wanayoyadhamiria katika kufuru na vitimbi kwa Nabii wa Mungu yamesajiliwa na yako kwake, atahisabu na atawalipa wanayostahiki.

**Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.**

{وَيَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَمَا لَيْسَ لَهُمْ بِهِ عِلْمٌ ۗ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ نَصِيرٍ }71

***Na wanaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ambavyo hakuviteremshia dalili na ambavyo hawana ujuzi navyo. Na madhalimu hawatakuwa na wa kuwasaidia.***

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ تَعْرِفُ فِي وُجُوهِ الَّذِينَ كَفَرُوا الْمُنْكَرَ ۖ يَكَادُونَ يَسْطُونَ بِالَّذِينَ يَتْلُونَ عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا ۗ قُلْ
{أَفَأُنَبِّئُكُمْ بِشَرٍّ مِنْ ذَٰلِكُمُ ۗ النَّارُ وَعَدَهَا اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ }72

***Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi utaona chuki katika nyuso za waliokufuru; hukaribia kuwavamia wale wanowasomea Aya zetu. Sema: Je, niwaambiye yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni moto wa Mwenyezi Mungu aliowaahidi waliokufuru, na ni marudio mabaya hayo.***

يَا أَيُّهَا النَّاسُ ضُرِبَ مَثَلٌ فَاسْتَمِعُوا لَهُ ۚ إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ يَخْلُقُوا ذُبَابًا وَلَوِ اجْتَمَعُوا لَهُ ۖ وَإِنْ
{يَسْلُبْهُمُ الذُّبَابُ شَيْئًا لَا يَسْتَنْقِذُوهُ مِنْهُ ۚ ضَعُفَ الطَّالِبُ وَالْمَطْلُوبُ }73

***Enyi watu! Umepigwa mfano, basi usikilizeni. Hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu hawatoum- ba nzi wajapojumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika atakaye na anayetakiwa.***

{مَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ }74

***Hawakumkadiria Mwenyezi Mungu haki ya kadiri yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.***

{اللَّهُ يَصْطَفِي مِنَ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا وَمِنَ النَّاسِ ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ} 75

***Mwenyezi Mungu huteua wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.***

{يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ} 76

***Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Na kwa Mwenyezi Mungu yatarejeshwa mambo yote.***

# Aya 71 – 76: Wanaabudu Asiyekuwa Mungu

## Maana

**Na wanaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ambavyo hakuviteremshia dalili na ambavyo hawana ujuzi navyo.**

Kujua kitu chochote ni lazima kuwe ama kwa msingi ulio wazi, ambako mtu anapata kujua, kwa kiasi tu cha kuleta picha yake; kwa mfano kujua kuwa pembe tatu sio mraba na mraba sio mduara. Au kuwe kwa nadharia; mfano kuwa ardhi inazunguka kandokando ya jua.

Kwa hiyo makusudio ya dalili hapa ni dalili za nadharia na makusudio ya ujuzi ni misingi iliyo wazi. Yaani washirikina wameabudu masanamu na mengineyo bila ya kutegemea nadharia yoyote au kwenye msingi wowote.

Wamemdhulumu Mwenyezi Mungu kwa kuabudu masanamu kwa kum– fanyia washirika na wamejidhulumu wenyewe kwa kujiweka kwenye ghadhabu za Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

**Na madhalimu hawatakuwa na wakuwasaidia** siku ya hisabu na malipo.

**Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi utaona chuki katika nyuso za waliokufuru. Hukaribia kuwavamia wale wanowasomea Aya zetu.**

Wanaosomewa ni wale wanoabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Walikuwa wanapomsikia Mtume (s.a.w.) au waumini wakiwasomea Qur'an au hoja nyinginezo basi nyuso zao zinageuka kwa chuki na

wanakusudia kuwavamia wale wanaowasikia.

**Sema: Je, niwaambiye yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni moto Mwenyzi Mungu aliowaahidi waliokufuru, na ni marudio mabaya hayo.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alimwamuru Mtume wake mtukufu, kuwaambia hao wenye hasira, ikiwa ni uzito kwenu kusikiliza haki, basi moto wa Jahannam kwenu ni mkali na mkubwa zaidi.

## Wajihi Na Mtazamo Wa Macho

Hakuna kitu kizito kwa mvunjifu kuliko tamko la haki, na ushindi wa watu wa haki; hasa pale anaposhindwa mvunjifu kuizuwia haki. Atanyamaza huku akijifanya hajali, lakini dalili zinazoakisi usoni mwake na mtazamo wa macho yake zinamfedhehesha.

Mtu anaweza kuwa muongo na kuwadanganya watu katika kauli yake na vitendo vyake, kwa sababu ana uwezo wa kuufanya ulimi wake na kuuzunguusha vile atakavyo. Vilevile mikono yake na miguu yake na huipeleka vile atakavyo. Ingawaje harakati za ulimi kwake ni jambo jepesi, lakini kuna kitu kimoja tu, hawezi kukihukumu vile atakavyo.

Kitu chenyewe ni moyo, uwe mzima au mbovu. Akipenda au kuchukia, athari yake hudhihiri usoni na machoni waziwazi. Haziwezi kufichwa na tabasamu la kutengeneza wala maneno ya kutiwa asali. Ndio maana ikawa kipimo sahihi cha undani wa binadamu sio maneno na vitendo.

**Enyi watu! Umepigwa mfano, basi usikilizeni. Hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu hawatoumba nzi wajapojumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake.**

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kutaja kwamba washirikina wameya- pa masanamu yao sifa za uungu, bila ya dalili, ametaja katika Aya hii, dalili za kihisia kukanusha sifa hii, ambazo anaweza kuzifahamu mjinga na hata mtoto pia: kwamba nzi ni kiumbe dhaifu, lakini lau nzi atachukua kitu kutoka kwenye masanamu, kisha masanamu hayo yakusanyike na yatangaze vita dhidi ya nzi kutaka kurudisha yalichonyang'anywa, nzi angelikuwa ni mshindi; sikwambii tena kuweza kuumba huyo nzi au hata kuumba ubawa wake.

**Amedhoofika atakaye** naye ni sanamu **na anayetakiwa** ambaye ni nzi. Kwa hiyo vipi yatakuwa masanamu ni Mungu.

Unaweza kuuliza kuwa masanamu hayo yenyewe tayari ni dalili kuwa sio Mungu, sasa vipi Qur'an imejishughulisha kuyaletea dalili?

Jibu: Ni kweli kuwa kukanusha uungu wa masanamu ni katika mambo yaliyo wazi kiakili, lakini wale walioyaabudu hawakuyaabudu kwa msukumo wa kiakili; isipokuwa ni kwa misukumo mingine; kama vile

malezi, uigaji, maslahi na mingineyo ambayo haikubali kukosolewa kwa namna yoyote ile.

## Kuhusu Itikadi Ya Tawhdi

Wakati nikifasiri Aya za Qur'an yenye hekima, nimetambua kwamba kila ninapoendelea kufasiri, Mwenyezi Mungu hunifungulia milango mingine ya maarifa ya siri za Qur'an na maajabu yake isiyokuwa na kiasi.

Kuna Aya nyingi zinazokaririka, katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kimatamshi na kimaana ambazo mara ya kwanza ninazifafanua kwa nilivyofahamu kutokana na tamko lenyewe au mfumo wa maneno n.k. Mara ya pili ninaunganisaha Aya iliyokaririka na ile iliyopita huku nikitaja namba yake na Sura yake au ninaifasiri kwa mfumo mwingine.

Ninapoifasiri mara ya pili au ya tatu huwa ninagundua upande ambao ulifichika kwangu hapo mwanzo na kwa wafasiri wengine wote niliowaangalia.

Aya nyingi zaidi zinazokaririka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni zile zinazofahamisha umoja wa Muumba na kupinga ushirikina na watu wake. Hayo Mwenyezi Mungu ameyataja kwa kila mfumo na kwa sura mbalimbali.

Nimezungumzia Tawhid na kukanusha ushirikina katika Juz. 5 (4: 48 – 50) kwa anuani ya 'Dalili ya umoja na utatu.' Kisha nikarudia maudhui hayo kwa mfumo mwingine katika Juz. 13 (13: 16), kwa anuani ya 'Akili za watu haziwatoshelezi.' Vilevile nimeleta mfumo wa tatu katika Aya ya 31 ya Sura hii tuliyo nayo. Na nitaleta mfumo mwingine wa nne na tano kulingana maudhui yatakavyokuwa. Hivi sasa narudia kwa ubainifu ufuatao:

Hakika lengo kuu la Uislamu ni kumuunganisha Muumba na kiumbe chake, kwa kupata muongozo katika yale anayoyaitakidi na kuyafikiri, kuyasema na kuyafanya na kuelekea kwake katika yote hayo.

Ndio maana Uislamu ukapinga ushirikina na kuuzingatia kuwa ni miongoni mwa madhambi makubwa na kosa lisilosameheka. Kama ambavyo umeichukulia ria na kufanya amali kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni shirk; na ukawapa washirikina adhabu kubwa na kali zaidi.

Hapana mwenye shaka kwamba watu wote wakiamini Mungu mmoja na wakawa na harakati kwa utashi mmoja, basi lazima wote watakuwa kwenye dini na sharia moja; isiyo na mifundo ya kidini wala kelele za utaifa au kuifanyia biashara dini na madhehebu.

Lakini kuweko na miungu wengi na kila mtu na lake, basi matokeo yake ni mfarakano na mvurugano baina ya watu. Kwa hiyo Uislamu unalingania kwenye itikadi ya Tawhid itakayomungoza kwenye misingi ambayo yatajengeka mapenzi, udugu, amani na raha.

Kuongezea kwamba huyo Mungu mmoja, ambaye uislamu unatoa mwito aabudiwe na kufutwa sharia

zake, ndiye Mungu wa ulimwengu Mwenye hekima, Mwadilifu na Mwingi wa rehema anayewapenda watu wote kwa usawa. Anachukia aina zote za sharia, atawalipa wema waliotenda mema na atawalipa ubaya kwa yale waliyoyafanya.

**Hawakumkadiria Mwenyezi Mungu haki ya kadiri yake** kwa vile walimwabudu mwingine wakaasi amri yake.

**Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda**.

Atawaadhibu na hawatapata mlinzi wala msaidizi zaidi yake.

**Mwenyezi Mungu huteua wajumbe miongoni mwa Malaika,** kama vile Jibril, kutemsha wahyi kwa manabii.

**Na miongoni mwa watu** vilevile huteua wajumbe wanaotoa mwito wa yale yanayomridhisha.

**Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona**.

Anasikia kauli zao na anajua yaliyo katika dhamiri zao na yale wayafanyao.

**Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao**.

Ni kinaya cha kuwa hakifichiki chochote mbele yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na ni ufafanuzi wa kauli yake Mwenyezi Mungu: ‘Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.’

**Na kwa Mwenyezi Mungu yatarejeshwa mambo yote**.

Kwake ndio mwanzo na ndio mwisho. Kwa maneno mengine: “Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.”

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ارْكَعُوا وَاسْجُدُوا وَاعْبُدُوا رَبَّكُمْ وَافْعَلُوا الْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ۩ {77

***Enyi ambao mmeamini! Rukuuni na sujuduni, na muabuduni Mola wenu, na fanyeni kheri huenda mkafaulu.***

وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ ۚ هُوَ اجْتَبَاكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ۚ مِلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ ۚ هُوَ سَمَّاكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ وَفِي هَٰذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ ۚ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ {وَاعْتَصِمُوا بِاللَّهِ هُوَ مَوْلَاكُمْ ۖ فَنِعْمَ الْمَوْلَىٰ وَنِعْمَ النَّصِيرُ {78

***Na fanyeni jihadi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu jihadi inayomstahiki. Yeye ndiye ambaye amewachagua. Wala hakuweka juu yenu uzito katika dini. Ni mila ya baba yenu Ibrahim. Yeye aliwaita waislamu tangu zamani na katika hii. Ili Mtume awe shahidi juu yenu na nyinyi muwe***

***mashahidi juu ya watu. Basi simamisheni Swala na toeni Zaka na shikamaneni na Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mlinzi wenu, Mlinzi bora na Msaidizi bora kabisa.***

# Aya 77 – 78: Fanyeni Kheri Ili Mfaulu

## Maana

**Enyi ambao mmeamini! Rukuuni na sujuduni, na muabuduni Mola wenu, na fanyeni kheri huenda mkafaulu. Na fanyeni jihadi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu jihadi inayomstahiki.**

Hapa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anawaambia wale walimwamini Yeye na Mtume wake, kwamba kuamini tu hakufai kitu; ila kukiweko mambo mane:

1. Kuchunga Swala kwa ajili yake tu. pale aliposema: 'Rukuuni na sujuduni.'

2. Kujiepusha na yale aliyoyaharamisha, kama hiyana, unafiki, kuleta fitna, kuwazuilia watu wema na kupanga njama kuleta uharibifu na ufisa- di. Hayo ndio makusdio ya kusema kwake: 'Na muabuduni Mola wenu.'

3. Kufanya mambo ya kheri, kama kuwakoa wenye kuangamia, kusu- luhisha, na kusaidia kwenye masilahi ya umma. Ndio makusudio ya kuse- ma: 'na fanyeni kheri.'

4. Kupigana jihadi na maadui wa Mwenyezi Mungu na wa ubinadamu kwa hali na mali.

Yakipatikana mambo haya kwa mtu basi yeye ni katika waliofaulu na watu wema. Yametangulia maelezo kwamba neno 'huenda,' kwa Mwenyezi Mungu, linamaanisha uhakika wa kuwepo, lakini likitumika kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, basi linakuwa na maana ya kuweko uwezekano na matarajio.[1]

**Yeye ndiye ambaye amewachagua.**

Yeye ni Mwenyezi Mungu na maneno yanaelekezwa kwa waislamu. Wajihi wa kuwa wamechaguliwa ni kule kuhusika kwao na Bwana wa Mtume aliye mwisho wa manabii na sharia yake ya kudumu.

**Wala hakuweka juu yenu uzito katika dini.**

Huu ndio msingi katika misingi ya sharia za kiislamu, kudhihiri upana, kuwa mororo na ulaini wake. Kuna Hadith isemayo: "Hakika dini ya Mwenyezi Mungu ni nyepesi," haina uzito wala mashaka na ndiyo dini ya maumbile.

Ni kutokana na msingi huu ndio mafakihi wametoa fatwa na hukumu katika milango yote ya fiqh. Katika

ndimi zao na vitabu zimeenea kanuni hizi zifuatazo:

● Dharura huondoa vizuizi.

● Dharura hupimwa kwa kiwango chake.

● Dharura kali huondolewa na dharura hafifu.

● Huvumiliwa dharura binafsi kwa kuondoa dharura ya umma.

Miongoni mwa yanayoonyesha kuwa Uislamu ni mwepesi, ni kule kutokuwako kipingamizi chochote baina ya mtu na muumba wake; kama zilivyo dini nyingine.

**Ni mila ya baba yenu Ibrahim**.

Makusudio ya mila ni dini. Dini ya Ibrahim inaingia katika Uislamu kwa misingi yote na sharia zake nyingi na tanzu zake. Ibrahim (a.s.) ndiye baba wa hakika wa manabii na roho ya watu wa dini za mbinguni kwa kuangalia kutangulia kwake, na kuafikiana wote juu ya unabii wake na ukuu wake.

**Yeye aliwaita waislamu tangu zamani na katika hii**.

Imesemekana kuwa yeye, hapa ni Ibrahim, na kwanye neno 'hii ' kuna maneno ya kukadirwa kuwa 'na katika hii kuna utukufu wenu.'

Pia imesemekana kuwa yeye hapa ni Mwenyezi Mungu na 'katika hii' ni Qur'an; kwa maana ya kuwa Mwenyezi Mungu aliwaita nyinyi umma wa Muhammad waislamu katika vitabu vilivyotangulia, na vilevile amewaita waislamu katika hii Qur'an.

Tafsri zote mbili zinfaa, kwa sababu Ibrahim (a.s.) anazungumza mazungumzo ya Mwenyezi Mungu. Tazama Juz. 3 (3:19) kifungu cha 'Hakika dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu.'

**Ili Mtume awe shahidi juu yenu na nyinyi muwe mashahidi juu ya watu**.

Kesho hakimu ni Mwenyezi Mungu, shahidi wa kwanza ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) na shahidi wa pili ni ulama.

Mtume atakuwa shahidi juu ya wenye elimu kwamba aliwafikishia kutoka kwa Mungu nao wafikishe kwa umma wa Muhammad (s.a.w.) na wengineo. Akizembea mmoja wa maulama kufikisha ujumbe, basi atakuwa amestahili ghadhabu za Mwenyezi Mungu na makazi yake ni Jahannam ambayo ni makazi mabaya. Umetangulia mfano wake katika Juz. 2 (2:143).

**Basi simamisheni Swala na toeni Zaka**.

Huu ni msisitizo wa yaliyopita katika Aya ilyotangulia.

**Na shikamaneni na Mwenyezi Mungu**.

Shikamaneni na twaa yake na mjiweke mbali na kumwasi katika *Nahjul- balagha* imesemwa "Kujiepusha na maasi ni katika aina za isma."

**Yeye ndiye Mlinzi wenu,** ikiwa mtamtii na mkawa na msimamo.

**Mlinzi bora na Msaidizi bora kabisa** kwa yule atakayemfanya ni mlinzi wake na akamtegemea yeye tu, si mwingine.

1. Ndio maana mara nyingine tunafasiri 'ili', kama wafanyavyo wafasiri wengi wa kiswahili -Mtarjumu

---

**Source URL:**
https://www.al-islam.org/sw/al-kashif-juzuu-ya-kumi-na-saba-muhammad-jawad-mughniyya#comment-0

**Links**
[1] https://www.al-islam.org/sw/person/muhammad-jawad-mughniyya
[2] https://www.al-islam.org/sw/organization/al-itrah-foundation
[3] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/36253
[4] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/36253
[5] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/36253
[6] https://www.al-islam.org/sw/person/hassan-ali-mwalupa